Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Tano - Tarehe 15 Juni, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 40

**Uwekezaji kwa Utaratibu wa *BOT***

**MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa muda mrefu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikizungumzia utaratibu wa uwekezaji hususan katika sekta ya miundombinu kwa utaratibu wa *Build, Operate and Transfer* ili kurahisisha maendeleo. Je, Serikali inaweza kuwavutia wawekezaji wowote chini ya utaratibu huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kilichomaliza shughuli zake tarehe 23 Aprili, 2004, nilimjibu Mheshimiwa Philip Magani, Mbunge wa Ruangwa, ambaye alipenda kufahamu jinsi ya kuwavutia wawekezaji kwa njia ya *Build, Operate and Transfer (BOT).*

Mheshimiwa Spika, katika kurejea jibu langu la msingi ni kuwa, utaratibu wa *Build, Operate and Tranfer* ni mbinu ambayo Serikali imeamua kuitumia kwa kutoa vivutio maalum ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje, kuwekeza katika miundombinu ili kuipa Serikali unafuu katika gharama za uwekezaji. Chini ya utaratibu huu wawekezaji binafsi huruhusiwa kujenga, kuendesha na hatimaye kukabidhi kwa

Serikali, miundombinu waliyojenga baada ya muda wa makubaliano kumalizika kwa kuingia mikataba na Serikali.

Mheshimiwa Spika, mkataba wa namna hii humruhusu mwekezaji binafsi kutoza ushuru kwa watumiaji wote wa miundombinu aliyojenga kwa kuzingatia makubaliano ambayo yako kwenye mkataba na Serikali. Ni kwa njia ya kutoza ushuru ambapo inatarajiwa kwamba, mwekezaji ataweza kurejesha gharama na pia kutengeneza faida katika muda wa mkataba. Ujenzi wa barabara na madaraja ni baadhi tu ya miradi inayoweza kufanywa chini ya utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, chini ya utaratibu huu, Serikali imeshaanza majadiliano ya awali ya mwekezaji aliyejitokeza ikiwa ni Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF),* juu ya ujenzi wa Mradi wa Daraja la Kigamboni katika eneo lililoko mwisho wa mkondo wa bahari ili kuunganisha Dar es Salaam Kaskazini na Kusini.

Mheshimiwa Spika, miaka ya karibuni imejitokeza Kampuni ya wageni na wazawa ya *PRODECO,* ambayo imefanya mazungumzo ya awali na Wizara ya Ujenzi, kwa lengo la kujenga barabara kuunganisha Mji wa Dodoma na Nzega kupitia Tabora ya km. 487 na matarajio ya kuunganisha Tabora na Kigoma km. 690. Pia barabara nyingine iliyopendekezwa kujengwa kwa utaratibu huu ni ile inayounganisha Mji wa Bagamoyo na eneo la utalii la Sadani km. 40 na uwezekano wa kuendelezwa hadi Tanga Mjini kupitia Pangani. Miradi mingine inayofikiriwa ni pamoja na ule wa *Mtwara Development Corridor.*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kuwa utaratibu huu wa uwekezaji katika miundombinu kwa njia ya *Build, Operate and Transfer,* utaweza kuwavutia wawekezaji wengi ili kuboresha sekta ya usafiri nchini.

**MHE. DR. LAWRENCE M. GAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo: Kwa kuwa huu utaratibu ni mzuri sana na unaweza kuleta manufaa makubwa sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Je, Serikali inaweza ikaongeza juhudi kidogo katika kuwashawishi hawa wawekezaji ili wawe wengi zaidi kuliko ilivyokuwa sasa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Lawrence Gama kwamba, utaratibu huu ni mzuri sana hasa katika kuboresha miundombinu yetu na ndiyo maana hata katika hotuba yetu ya bajeti ya mwaka huu, tumeweka msisitizo wa kutumia utaratibu huu katika kujenga baadhi ya miradi yetu nchini. Lakini vile vile kwa sababu utaratibu huu ni mpya na bado hatujaanza kuutumia hapa Tanzania, ni kweli kabisa Serikali sasa inabidi iweke nguvu zaidi katika kuwavutia wawekezaji kwa mpango wa *Build, Operate and Transfer.*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja kama ifuatavyo: Ni dhahiri kabisa Serikali ina

mpango wa kubinafsisha miundombinu yake na mashirika yake. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba mpango huu unajipinga wenyewe? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, Serikali inabinafsisha mashirika yaliyokuwa yakimilikiwa na Shirika la Umma kwa maana ya ubinafsishaji, unafanyika kwa yale mashirika yaliyokuwa yakimilikiwa na Serikali. Mpango wa *Build, Operate and Transfer,* kama tutakavyouona ni mpango ambao unavutia wawekezaji binafsi baada ya kufanya mchanganuo na kuona watapata faida gani ndipo wanapoingia katika mradi huo. Kutokana na hilo utaratibu wa ubinafsishaji na *BOT* haupingani. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea ningependa kuwaarifu Watanzania wanaofuatilia mambo yanayotokea ndani ya Bunge kwamba, kuanzia leo wale wanaopata matangazo ya *television* ya *Star TV* wanaweza kutuona tukifanya kazi hapa Bungeni moja kwa moja kutoka kwenye Ukumbi huu. Mitambo imeshakamilika, wenye *television* hizo wanaweza kuzifungua sasa na watatuona tunafanya kazi kwa niaba yao. Tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi. *(Makofi)*

Na. 41

**Upatikanaji wa Hati ya Nyumba na Ardhi Asili**

**MHE. MEJA JESSE J. MAKUNDI** aliuliza:-

Kwa kuwa kabla ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1974 inayohusu mtu kuwa na Hati ya Shamba na Nyumba, barabara zinazounganisha Vijiji, Wilaya, Mikoa hadi nchi jirani zilikuwa njia za miguu na hatimaye barabara ndogo za kupitisha magari madogo na sasa zimejengwa kwa kiwango cha Kimataifa na nyumba za wanavijiji zilizoko kwenye mashamba asili *(vihamba)* kuwekwa alama ya "X" kuashiria kuvunjwa:-

(a) Je, Serikali itawalipa kabla fidia/stahili wanavijiji na nyumba/vihamba vilivyomalizwa kwa ajili ya upanuzi wa barabara hizo ambazo ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa letu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa ni muhimu na ni busara kutoa semina/mihadhara na vipeperushi vya kuelimisha wanavijiji juu ya upatikanaji wa hati ya nyumba na mashamba ili iwe rahisi kwa fidia endapo hapo baadaye italazimika kupitisha barabara kwenye nyumba au shamba *(vihamba)* vya wanavijiji?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makazi, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Meja Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Tanzania haijawahi kuwa na Sheria ya Ardhi ya mwaka 1974. Sheria za Ardhi zinazotumika sasa ni Sheria ya Ardhi Na. 4 na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5, ambazo zilitungwa na Bunge lako Tukufu mwaka 1999. Kabla ya kutungwa kwa sheria hizo kulikuwa na Sheria ya Ardhi *(Land Ordinance),* Sura Na. 113 ya mwaka 1923.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Meja Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, suala la ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathirika kutokana na upanuzi wa barabara nchini, linategemea maelezo yanayowasilishwa Wizarani kwangu na mamlaka husika kuhusu upana stahili wa barabara inayohusika. Baada ya kupata maelezo hayo, ndipo wathamini wanaweza kufanya kazi ya kuthamini ardhi na mali zingine zilizoko na kuandaa taarifa inayoonyesha wananchi wanaostahili kulipwa au kutolipwa fidia. Hivyo, kinachowezesha ardhi ya wanavijiji, nyumba zao na mali zingine kulipwa fidia ni sharti ijulikane mipaka ya eneo la upimaji wa barabara na kama ilivyojibiwa na Serikali kwenye swali Na. 13 la Mheshimiwa Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, tarehe 9 Juni, 2004.

(b) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu inawajibika kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera ya Taifa ya Ardhi na Sheria mpya za ardhi juu ya matakwa yake ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa hati za kumiliki ardhi kimila au kisheria. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara yangu imekuwa ikitoa elimu kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupitia vyombo vya habari kama redio, televisheni, kuandika makala kwenye magazeti, kusambaza vipeperushi, semina na kushiriki kwenye maonyesho ya sabasaba, mwaka 2003 tulishiriki.

Aidha, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imekwishatoa elimu kwa umma kuhusu Sheria hizo kwa Maafisa Watendaji wa Kata wasiopungua 2,408 na Viongozi 72,000 kutoka Kamati mbalimbali za vijiji katika mikoa yote 21 ya Tanzania Bara.

Natoa wito kwa asasi zisizo za Kiserikali na wadau wengine, washirikiane na Wizara yangu kutoa elimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi na Sheria za Ardhi ili kuwafikia wananchi katika vijiji vyote nchini. *(Makofi)*

**MHE. MEJA JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza angalau swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa kwa mujibu wa *Hansard* ya tarehe 9 Juni, 2004, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, wakati akijibu swali la Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, alisema kwamba, Wabunge na Madiwani watawajibika kama Serikali itakapopata fedha itakuta wananchi hawajaondoka katika maeneo yaliyowekwa alama ya "X" na kwamba watasukumizwa pembeni mwa barabara na kwamba sijui wataliwa na simba kama ilivyokuwa *operation* ya Serikali ya Awamu ya Kwanza.

**SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. MEJA JESSE J. MAKUNDI:** Je, kwa tamko hili haoni kwamba amevunja Katiba ya Nchi na kwamba amewafanya Wabunge na Madiwani watakaogombea mwaka 2005 hasa wa CCM, kukosa nafasi katika sehemu zao na kuwafagilia Upinzani, wanaowatetea wanyonge ili hatimaye *TLP* inayoongozwa na Mheshimiwa Augustino L. Mrema, Rais Mtarajiwa wa Awamu ya Nne, atakapoingia madarakani? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Swali lako limeeleweka litajibiwa na Waziri wa Ujenzi kwa sababu hili halihusu ardhi. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi majibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, siamini kama ni kweli yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Meja Jesse Makundi, ndiyo yaliyozungumzwa na Mheshimiwa Naibu Waziri. Siamini kama katika *Hansard* kuna neno simba kama alivyozungumza Mheshimiwa Meja Jesse Makundi.

Mheshimiwa Spika, kupitia Sheria Namba 167 ya mwaka 1967 ambayo ilikuwa *gazatted* kwenye Gazeti la Serikali tarehe 5 Mei, 1967, Sheria ambayo imeanza kutumika tangu mwaka 1932 ikafanyiwa *amendment* mwaka 1938, ikifanyiwa tena *amendment* mwaka 1954 na ikafanyiwa *amendment* ya mwisho kwenye mwaka 1967, inazungumzia kuhusu hifadhi ya barabara. Katika hifadhi ya barabara inaeleza kwamba, upana wa barabara, kwa mfano, barabara kuu upana wake ni futi 75 au mita 22.5. Kwa barabara za mikoa upana wake ni futi 75 au mita 22.5. Kwa barabara za wilaya upana wake ni futi 33. Sasa kwa sababu hiyo ni sheria na bahati nzuri Mheshimiwa Makundi, ameapa hapa Bungeni kulinda sheria, ni matumaini yangu kwamba, ataendelea kuilinda hii sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kwamba *TLP* watashinda, hifadhi ya barabara inapotengwa vizuri na bahati nzuri barabara huwa zinatengenezwa na wananchi na Watanzania wengi wanahitaji barabara nzuri na hii ni kuifagilia CCM iweze kushinda katika mwaka 2005. *(Makofi)*

**SPIKA:** Muda wa swali hilo umekwisha nasikitika Waheshimiwa Wabunge. Maswali kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 42

**Uimarishaji wa Ofisi ya Uhamiaji - Rusumo Ngara**

**MHE. GWASSA A. SEBABILI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mpaka wa Tanzania na Rwanda upo Mto Kagera na daraja kubwa la Rusumo linaloheshimika kutokana na muungano wa Mito ya Kagera na Rambu; na kwa kuwa pia pana ofisi ndogo sana ya uhamiaji kwa zaidi ya miaka 40 imekuwa ikitumiwa na Uhamiaji, Polisi na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA);* na kwa kuwa

Kituo cha Uhamiaji Rusumo ndio mlango wa kwenda Rwanda, Burundi, Uganda, *Congo DRC* na Magharibi na kwamba pale yanapita magari makubwa na madogo na yale yanayobeba mizigo mizito na mengine ya hatari; na kwa kuwa pia hupita wasafiri wa Kimataifa kutoka Tanzania kwenda Uganda, Kenya, Sudan, Malawi, Somalia na kadhalika na wakati wa mauaji ya Rwanda ya mwaka 1994, kituo kilipitisha zaidi ya wakimbizi 700,000 kwa saa 30 hivi; na kwa kuwa kutokana na athari ya vita vya Rwanda na Burundi kumefanya shughuli katika kituo hicho kuongezeka na kufanyika kwa saa 24 huku kikiwa hakina huduma ya umeme, mawasiliano *(Radio Call),* usafiri (gari) na kituo kiko umbali wa zaidi ya km. 50 toka Makao Makuu ya Wilaya na kiko bondeni ambako kinafikiwa kwa barabara ngumu sana kupitika hasa nyakati za mvua na mafuta yanayodondoka kwenye magari kuifanya barabara hiyo kuwa na utelezi wakati wote na kutokana na hali hiyo jengo linakuwa halina usalama kwa watumiaji na mali zake:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi zenye hadhi na za kutosha kwenye eneo salama pale Rusumo?

(b) Je, Serikali iko radhi kupeleka jenereta ya umeme, *radio call* na magari kituoni hapo ili kuimarisha na kukabiliana na kazi nyingi zilizopo na hatimaye kuleta ufanisi mzuri wa kazi ikiwemo ile ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa mamilioni ya fedha kwa siku na ulinzi imara mipakani mwa nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Kituo cha Mpakani cha Rusumo, ndio mlango mkubwa kutoka Tanzania kwenda Rwanda, Burundi, Uganda na *Congo DRC.* Kituo hicho hupitisha magari mengi na wageni wengi wa Kimataifa wanaoingia na kutoka Tanzania. Ni kweli pia kwamba, Kituo cha Rusumo kina jengo moja linalotumiwa na Idara ya Forodha, Polisi na Uhamiaji. Jengo hilo ni dogo hivyo halikidhi mahitaji ya idara hizo.

Hata hivyo, ninatofautiana na maelezo ya Mheshimiwa Mbunge, yenye kutoa sura kana kwamba, Idara za Serikali, zilizopo katika Kituo cha Rusumo hazina kabisa vitendea kazi pamoja na umeme. Ukweli ni kwamba, Idara ya Forodha inalo jenerata kubwa linalotoa umeme unaotumiwa na Idara zote. Aidha, Idara za Uhamiaji na Forodha zina magari yanayotumiwa na idara zote kufanya doria ya mpakani na pia ipo *radio call* ya Idara ya Uhamiaji na nyingine ya Idara ya Polisi, zinazotoa huduma ya mawasiliano katika kituo hiki. Huduma hizi za usafiri, mawasiliano na umeme, zitaendelea kuboreshwa kadri Bajeti ya Serikali inavyozidi ubora kila mwaka. Hii ni pamoja na ujenzi wa jengo la kisasa litakalokidhi mahitaji ya Idara zote tatu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Mbunge, kwa kutoa msukumo huu, wenye lengo la kuboresha huduma za kituo hiki.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba, kwa kuwa kumekuwa na matukio ya mara kwa mara ya ajali pale karibu na jengo la kituo hicho kutokana na mteremko mkali na kituo chenyewe kujengwa chini ya mlima, sasa umefika wakati kwamba kituo hicho kihamishwe pale mapema zaidi ili kuokoa maisha ya wasafiri wanaopita pale, maisha ya watumishi wa Serikali na kuwepo kwa mali za Serikali ili kuleta amani katika eneo hilo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, inao mpango wa kujenga jengo jipya kubwa litakalokidhi mahitaji ya idara zote tatu. Sasa katika ujenzi huo wa jengo jipya, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, utazingatiwa, hilo jengo jipya tena lisijengwe katika eneo lenye mteremko mkali na yeye mwenyewe tutamshirikisha wakati tunatafuta eneo muafaka katika kujenga hilo jengo jipya la kituo hicho. *(Makofi)*

Na. 43

**Kituo cha Polisi Mkokotoni - Unguja**

**MHE. KIJAKAZI KHAMIS ALI** aliuliza:-

Kwa kuwa majengo ya Vituo vya Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja yako katika hali ya uchakavu pamoja na majengo ya nyumba wanazoishi hasa Kituo cha Polisi Mkokotoni - Unguja kilichopo kwenye Wilaya ya Kaskazini "A"; na kwa kuwa jengo hilo lililojengwa wakati wa enzi za mkoloni likiwa linatumika kwa kazi nyingine lakini Polisi wamehamia kwenye jengo hilo ambalo vijana wa miaka 50 hawalifahamu; na kwa kuwa hata nyumba wanazoishi ni chakavu sana, hazitoshi na hivyo husababisha baadhi ya Polisi kuondoka kazini mapema kwa kutumia magari ya abiria kwenda Gamba katika nyumba za kupanga ambapo ni mbali sana na Kituo chao hasa kwa wakati huu ambapo kuna vitisho vya hapa na pale Zanzibar:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba iko haja ya kuongeza fedha katika bajeti ili kipindi kijacho ujenzi wa nyumba za Polisi na Kituo hicho cha Mkokotoni uanze?

(b) Kwa kuwa Mkokotoni mpaka sasa ndio Makao Makuu ya Polisi Mkoa wa Kaskazini Unguja, je, Serikali haioni kwamba ni vizuri kujenga jengo linalofanana na hadhi ya Kimkoa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kijakazi Khamis Ali, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua uchakavu wa nyumba za kuishi askari katika Kambi ya Kituo cha Polisi cha Mkokotoni kule Unguja na makambi ya vituo vya mikoa mingine hapa nchini. Kwa sababu hiyo, hatua zimeanza kuchukuliwa kujenga nyumba za kuishi askari katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa mfano, mwaka 2003 ujenzi wa nyumba 53 umekamilika katika Kambi ya Polisi ya Mfikiwa huko Chake Chake Pemba. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005 jumla ya shilingi 255,000,000/= tutaziomba katika Bunge hili kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari huko Unguja na Pemba. Kwa kuwa fedha hizi ni kidogo, ujenzi utafanywa kwa awamu. Nawaomba askari wa Mkokotoni wawe na subira wakati wakisubiri awamu yao. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Makao Makuu ya Polisi ya Mkoa wa Kaskazini Unguja yanastahili kuwa na jengo la ofisi lenye hadhi. Napenda ieleweke pia kwamba, bado tunayo mikoa mingi nchini ambayo haina majengo yenye hadhi. Mikoa hiyo ni pamoja na Morogoro, Kilimanjaro, Mara, Tabora, Mwanza, Kigoma, Mbeya, Iringa, Ruvuma, Mtwara, Singida, Dodoma, Kusini Unguja na Kusini Pemba. Kwa kutambua tatizo la kutokuwepo kwa majengo yenye hadhi ya Ofisi za Makamanda wa Polisi wa Mikoa, Serikali imekuwa inajenga majengo hayo kwa awamu kwa kuzingatia uwezo wa bajeti. Katika mwaka wa fedha huu wa sasa unaokwisha, Serikali imeanza kujenga majengo hayo katika Mikoa ya Tabora na Iringa. Ujenzi wa majengo hayo unatarajiwa kukamilishwa katika mwaka wa fedha wa 2004/2005. Baada ya hapo ndipo mikoa mingine itafikiriwa pamoja na Mkoa wa Kaskazini Unguja. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, nimefurahi kupata nafasi ya kuuliza swali moja kama ifuatavyo: Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amezungumza kwamba zimejengwa nyumba 53 katika Kijiji cha Mfikiwa katika Jimbo la Wawi. Ni kweli kwamba nyumba hizo zimejengwa, ni nzuri sana, lakini haoni kwamba sasa nyumba hizo hazikaliki kwa sababu ya kukosekana umeme? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli nimesema kwamba katika mwaka uliopita wa 2003, tumekamilisha kujenga kambi ya kisasa pale Mfikiwa, hii ni moja ya kambi nzuri sana kimajengo kuliko kambi zote nchini. Ningependa kambi zote za polisi kwa miaka ijayo ziwe kama Kambi ya Wawi. Hii ni hatua kubwa sana kujenga zile nyumba. Kwa hiyo, suala la umeme Mheshimiwa Mbunge, litakuja tu kazi kubwa ilikuwa kujenga zile nyumba. Kwa hiyo, hiyo kazi ya umeme inakuja, uwe na subira na tunakushukuru kwamba mara kwa mara umekuwa unasukuma sana utekelezaji wa suala hili katika jimbo lako.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa niulize swali kama ifuatavyo: Kwa kuwa katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri, amekiri kuwa vituo vya polisi vingi na nyumba za polisi ni chakavu. Kwa kuwa katika Kituo cha Matangatuwani pana kituo cha polisi ambacho zamani kilikuwa kikubwa na sasa kimechakaa mno kiasi kwamba Serikali imefikiria kuhamishia kituo hicho Finya, lakini bado utakuta kuna askari mmoja au wawili ambapo mimi kwa mawazo yangu hata la kufanya pale kwenye kituo hawana. Je, haoni ni wakati maridhawa

wa kuihamisha rasmi ile kambi na sasa ihamie kwenye Kambi ya Finya kwa ajili ya kuimarisha kazi za polisi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza Kituo cha Matangatuwani hatuna mpango wa kukihamishia Kituo cha Finya, kitabaki pale pale Finya na mwaka huu kimo katika utaratibu wa kukiboresha zaidi na Matangatuwani kitabaki jinsi kilivyo na chenyewe vile vile tutakiboresha ili kuimarisha hali ya ulinzi na usalama katika eneo la Pemba. *(Makofi)*

Na. 44

**Aina ya Mafuta inayopatikana Tanzania**

**MHE. LEONARD N. DEREFA** aliuliza:-

Kwa kuwa mafuta ya *petroleum* hupatikana katika aina tatu (i) *crude oil* kutoka ardhini (ii) *bitumious sand (tar sands)* ambayo huweza kutengenezwa mafuta ya *petroleum* na (iii) *oil shale* ambayo huchemshwa na kutoa mafuta ya *petroleum:-*

(a) Je, nchi yetu katika hali ya utafiti wa kutafuta mafuta tunatafuta mafuta ya aina moja tu ama tunatafuta aina zote za mafuta ya *petroleum?*

(b) Kwa kuwa katika ramani za *hydrocarbon* hakuna visima vya mafuta kote katika mwambao wa *Indian Ocean* katika Afrika isipokuwa mwambao wa *Indian Ocean* huko Australia na Visiwa vya Brunei na Indonesia. Je, kwa nini basi jitihada za kutafuta mafuta zisifanywe ndani ya nchi kama wenzetu wa Uganda ambao wamedai kupata mafuta maeneo ya *Lake Kioga?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard Derefa, Mbunge wa Shinyanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Nchi yetu katika utafiti wa mafuta, mwelekeo upo zaidi katika kutafuta mafuta ghafi yanayopatikana katika mazingira asilia *(Crude Oil).* Utafiti uliokwishafanyika haujaonyesha viashiria vya kuwepo kwa hazina kubwa ya *tarsands* na *oil shale* nchini mwetu.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa kutafuta mafuta kwenye maeneo ya nchi kavu. Hata hivyo, kuanzia miaka ya 1990 teknolojia ya utafutaji mafuta hususan katika maeneo ya vilindi vya bahari *(Deep Sea)* imekuwa kwa haraka sana hivyo kupelekea kampuni za mafuta kuanzia kuelekeza mahitaji yao katika maeneo hayo. Nchi ambazo zimefanikiwa kugundua mafuta kwa teknolojia hii kwa Afrika ni pamoja na Mauritania, Guinea Bissau, Angola na Nigeria na kwa upande wa *Latin America* ni pamoja na Ghuba ya Mexico na Brazil. Kutokana na matunda haya ya kukua kwa teknolojia, Serikali imekamilisha majadiliano na Kampuni

ya *Shell* toka Uholanzi ili kampuni hiyo ije kutafuta mafuta katika maeneo ya vilindi vya Bahari ya Hindi Mashariki ya Kisiwa cha Unguja. Taratibu za kusaini mkataba na kampuni hiyo ya *Shell* zinaandaliwa. Aidha, Serikali imesaini mkataba na kampuni ya *Petrobras* ya Brazil tarehe 5 Juni, 2004 ili kampuni hiyo ianze shughuli ya kutafuta mafuta katika maeneo ya vilindi vya Bahari ya Hindi Mashariki ya Kisiwa cha Mafia.

Pamoja na jitihada ya kutafuta mafuta katika maeneo ya vilindi vya Bahari ya Hindi, Serikali imekuwa pia inaendelea na jitihada za kushawishi kampuni za mafuta kutoka nje ya nchi kuja kutafuta mafuta katika maeneo ya ndani ikiwemo ukanda wa mwambao wa Bahari ya Hindi na maeneo ya Bonde la Ufa. Shughuli za utafutaji mafuta katika maeneo ya Bonde la Ufa zilianza katika miaka ya 1980, ambapo Chuo Kikuu cha Duke toka Marekani chini ya Mradi wa *Probe* kilikusanya taarifa za tetemo yaani *(Seimic Data)* kiasi cha kilomita 6,000. Kupatikana kwa taarifa hizo za kijiofizikia kulivutia kampuni ya *AMOCO* toka Marekani, ambayo mwaka 1987 ilichimba visima viwili Galula - 1, Ivuna - 1. Visima vyote havikuwa na mafuta wala gesi

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize moja kama ifuatavyo: Kutokana na mfumuko wa bei ya mafuta, je, Serikali inasemaje, inaweza vile vile ika-*subsidize* kama vile wanavyo-*subsidize* umeme? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la upandaji bei ya mafuta ni suala ambalo Serikali imekuwa ikilifuatilia kwa karibu na tumewahi kutoa taarifa juu ya sababu kubwa ikiwa ni hali ya kisiasa katika maeneo ya Mashariki ya Kati na Ghuba hasa nchini Iraq na Saudi Arabia.

Kama tunavyofahamu, suala la biashara ya mafuta nchini mwetu ni suala ambalo ni la kibiashara, liko katika mfumo wa soko na ni suala ambalo tunataraji hali ya kisiasa ikitengemaa katika maeneo ambayo tumesema ndiyo sababu yenyewe ya kupanda kwa bei, basi bei hizi huenda zikashuka. Lakini kwa sasa hivi bei ya mafuta iko juu na kwa kweli Serikali inaendelea kufuatilia tuone ni nini ambacho kinawezekana. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeingia mikataba na makampuni mbalimbali kwa ajili ya kufanya utafiti wa mafuta katika mwambao wa Bahari ya Hindi na mikataba hii ni ya muda mrefu kama vile zaidi ya miaka 15 au 20.

Je, Serikali haioni kuwa mikataba hii kuwa ni mirefu sana, inazuia wawekezaji wengine kuja kufanya utafiti labda mzuri zaidi kuliko hawa ambao tumeingia nao mkataba na hawafanyi jambo lolote? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, shughuli ya kutafuta mafuta ni ya gharama kubwa na inahitaji uwekezaji mkubwa. Kwa hiyo, katika shughuli za kutafuta mafuta wale wanaokuja kuwekeza kuna taratibu zinazotumika za kuwapa maeneo kwa muda fulani fulani na kila muda unapofika, suala hili la utafutaji wa mafuta huwa linapitiwa upya. Kwa mfano, kuchimba kisima kimoja tu cha mafuta na

kutoweza kutafuta kama yapo mafuta au sivyo, uwekezaji unafikia kati ya dola milioni 10 hadi milioni 15.

Ni dhahiri kabisa kutokana na gharama kubwa iliyopo ni muhimu hawa wawekezaji wapewe muda wa kutosha kwa sababu suala zima la utafutaji mafuta linahitaji muda mrefu ili kuweza kugundua kama yapo mafuta hayapo na Serikali inajitahidi katika shughuli hizi kuhakikisha kwamba, tunavutia wawekezaji na tunakuwa tukifanikiwa katika kuvutia wawekezaji katika utafutaji mafuta.

Na. 45

**Umeme Vijiji vya Jimbo la Rungwe Magharibi**

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini ya mwaka 2001/2002 ni Kijiji cha Ngopyolo peke yake kilichoorodheshwa kati ya Vijiji 12 vya Jimbo la Rungwe Magharibi kupatiwa umeme katika mwaka huo wa fedha; na kwa kuwa Serikali kupitia Shirika lake la *TANESCO* iliahidi kuwa Kijiji cha Isyonje kwenye Jimbo hilo kingepatiwa umeme ifikapo Agosti, 2002 na kwamba vijiji hivyo hadi leo havijapatiwa umeme:-

(a) Je, kwa nini Serikali haijatimiza ahadi zake kwa wananchi na ni lini sasa umeme utafikishwa kwenye Vijiji nilivyovitaja?

(b) Kwa kuwa umeme wa Gridi ya Taifa umefika katika Kiwanda cha Chai Musekera km. 3 kutoka Kijiji cha Bajela, je, ni lini wananchi wa Kijiji hicho na Kata ya Bajela wataunganishiwa umeme huo?

(c) Je, ni lini Shule za Sekondari za Mporoto na Kinyala zitafikishiwa umeme ili ufundishaji katika taasisi hizo uendane na zama hizi za sayansi na teknolojia ikiwa ni pamoja na matumizi ya kompyuta?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme Ngopyolo na Isyonje inaendelea kama ifuatavyo:-

(a) Ngopyolo: Kazi inahusisha ujenzi wa laini ya kilovoti 11 yenye urefu wa kilomita 1.7, kujenga *transforma* ya ukubwa wa *50 KVA,* kujenga laini za umeme mdogo za urefu wa kilomita moja na kuunganisha wateja. Hadi sasa kazi ya kujenga laini ya

kilovoti 11 imekamilika kwa asilimia 80, *transforma* tayari iko Tukuyu na matayarisho ya kuijengea yanaendelea.
Kuendelea na ujenzi wa laini ndogo ya umeme, kati ya nguzo ishirini zinazohitajiwa nguzo kumi zimesimamishwa au zimeshajengewa. Nguzo nyingine kumi zilizobaki ziko *site* na kazi za kuzisimamisha zinaendelea. Kazi ya kuvuta waya itaanza bada ya kusimamisha nguzo zote ishirini kwani vifaa vyote vikiwemo vikombe na nyaya vimekwishawasilishwa Ofisi ya *TANESCO* Tukuyu toka *TANESCO* Mkoani Mbeya.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizosalia kama nilivyoeleza awali, zinataratijiwa kukamilika ifikapo 30 Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Isyonje: Kazi inahusisha ujengwaji wa *transforma* ya *100 KVA,* ujenzi wa kilometa moja ya umeme mdogo *(Low Voltage)* na kuunganisha wateja. Kazi ya kusambaza umeme mdogo imekamilika na *transforma* itapelekwa *site* baada ya ukaguzi unaofanywa kiwandani *TANALEC* Arusha kukamilIka. Ukaguzi unaohusisha *order* nzima ya *transforma* utakamilika kabla ya tarehe 20 Juni, 2004 na *transforma* ya Isyonje inatarajiwa kufikishwa huko na kujengewa kabla ya mwisho wa Juni, 2004.

(b) Mheshimiwa Spika, ili umeme uweze kufikishwa Bujela lazima njia ya umeme ya kilovoti 11 ijengwe yenye umbali wa kilomita 10, *transforma* moja yenye uwezo wa *50 KVA* ifungwe na njia ndogo ya umeme ya umbali wa kilomita 10 pia zijengwe. Kazi hii itahitaji jumla ya shilingi 118.5 milioni.

(c) Mradi wa kupeleka umeme Sekondari za Mporoto na Kinyala utahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa *11 KVA* umbali wa kilomita 8, ufungaji wa *transforma* na ujenzi wa njia ndogo za umeme. Utekelezaji wa kazi hii unahitaji jumla ya shilingi 117 milioni.

Mheshimiwa Spika, kazi za kupeleka umeme huko Bujela na Sekondari za Mporoto na Kinyala zitasubiri kidogo kutokana na matatizo ya kifedha ambayo *TANESCO* imekuwa nayo, yaliyosababishwa na ukame. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mara uwezo huu wa fedha utakapopatikana, basi kazi hiyo itakamilika.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu ya matumaini ingawa siyo mapya. Nimekuwa nikiahidiwa na tutafuatilia kwa karibu.

Miezi miwili iliyopita Mheshimiwa Naibu Waziri alitembelea mgodi kule kwetu ambao unazungukwa na vijiji vya Lutete, Lubanda, Ilima na Busone na wananchi wa maeneo hayo ndiyo wanaochimba na kuzalisha umeme na huo umeme unaingizwa kwenye gridi ya Taifa. Hawa wananchi hawapati umeme. Je, haoni kwamba atakuwa anawatendea haki kama tutawawekea *transforma* na wao wafaidike na jasho lao?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, masuala ya upelekaji umeme kwenye vijiji ambavyo tumevitaja ni masuala ambayo tunayafuatilia kwa karibu. Naye tunamshukuru kwa kweli kwa ufuatiliaji wake na namwomba avute subira, kama nilivyoeleza awali kazi hii itafanyika. Kuhusu vijiji ambavyo amevitaja na kwa sababu ndiyo amevitaja hivi sasa, mimi napenda niungane naye kwamba, popote pale ambapo inawezekana kuwavutia umeme wananchi, kwa kweli umeme ni kitendo cha maendeleo na inavutia maendeleo. Kwa hiyo, si dhamira ya Serikali kwamba isiweze kuvuta umeme pale ambapo inawezekana. Kwa kuwa maeneo haya ameyataja hivi punde, basi ninadhani nitachukua nafasi kuweza kuyafuatilia tuone kipi kinawezekana ili wananchi hawa walioko kando kando ya Mgodi wa Kiwira, unaozalisha umeme na unaouzwa kwenye gridi ya Taifa na wao uwezo utakapopatikana waweze kufungiwa umeme.

**MHE. FRANK G. MAGHOBA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la umeme liko maeneo mengi ya nchi likiwemo Jimbo la Kigamboni na hasa ukizingatia kwamba sasa hivi Jimbo la Kigamboni na maeneo mengi ya baharini kuna mahoteli makubwa ya kitalii na ambayo yanachukua watalii wengi. Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme maeneo hayo ili kuinua uchumi zaidi na kuvutia watalii?

**SPIKA:** Naona hilo ni swali jipya, liletwe kwa njia za kawaida litapata majibu tu.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Vijiji vya Ngopyolo na Isyonje katika Jimbo hilo la Rungwe Magharibi, viliahidiwa kupata umeme ifikapo Agosti, 2002 na sasa ni mwaka 2004 yaani miaka miwili zaidi imepita. Ina maana kwamba, hata ahadi yako Mheshimiwa Waziri uliyoitoa kwamba ifikapo mwaka 2005 umeme utakuwa ukwishaingia katika Jimbo la Nkansi kupitia Vijiji vya Mkundi, Kipande, Kamtawa, Chala, Mji wa Namanyere pamoja na Kirando nayo hiyo haitaweza kutekelezwa inapofika mwaka huo na je, Serikali sasa inasema nini kuwaambia wananchi kikamilifu majibu ambayo ni sahihi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, wakati wote ambao tumekuwa tukijibu maswali hapa Bungeni, tumekuwa tukijibu maswali kwa usahihi kwa mazingira ya wakati ule na tumekuwa tukijibu maswali kutokana na matarajio ya Bajeti na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Pansiano Nyami kwamba, pale ambapo miradi haikutekelezwa haikuwa kabisa dhamira ya Serikali kutoa taarifa ambazo imejua kwamba, hapo baadaye haziwezi kutekelezwa, hapana. Ni kutokana na kwamba, kwa mtiririko wa upatikanaji wa fedha kupitia Bajeti au kupitia Ufadhili ambao tunaupata katika usambazaji umeme nchi nzima kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Fedha hizo inakuwa zinachukua muda mrefu kupatikana.

Kuhusu vijiji hivi, kwa mfano mzuri ni vijiji hivi ambavyo amevitaja. Yeye mwenyewe amesema kwamba vilitajwa kupata umeme mwaka 2002, lakini vimepata 2004. Kwamba sasa hivi vinashughulikiwa kupata umeme, inaonyesha dhamira thabiti

ya Serikali kwamba pale ambapo fedha zinapatikana basi miradi inatekelezwa. Kwa hiyo, kwa mtiririko huo huo tuwe na matumaini kwamba tutakapopata fedha za kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya mbalimbali, umeme huo utafikishwa kama ambavyo kazi hiyo hivi sasa inafanywa kwa maeneo mengi nchini ikiwemo Wilaya ya Ukerewe, Serengeti, Urambo na kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

Na. 46

**Ujenzi wa Gati za Nkoma na Muharamba**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa usafiri wa majini ni muhimu sana na Serikali iliona hilo na kuanzisha ujenzi wa gati za Kiwesi, Bukondo na Chato katika Ziwa Victoria na kwa kuwa Serikali imeshawahi kuahidi kuwa itaendelea kujenga gati nyingine hasa gati la Nkoma na Muharamba. Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa gati hizo ili kurahisisha usafiri katika ziwa hilo?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ernest Gakeya Mabina, Mbunge wa Geita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gati ni kiungo muhimu sana katika uchukuzi. Hakika gati ni daraja kati ya uchukuzi wa nchi kavu na ule wa majini. Kwa upande wa mwambao wa Pwani na visiwa vilivyo kwenye maziwa makuu na maeneo ya bahari, hatuwezi tukazungumzia kuondoa umaskini bila kuwa na programu ya kujenga gati. Inatubidi tutoe umuhimu katika kujenga magati kama ambavyo tunatoa umuhimu kwa barabara za vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Serikali imepanga kuendeleza usanifu, ujenzi na ukarabati wa magati ya Kasanga na Karema kwenye Ziwa Tanganyika, Kiamkwikwi, Shirati, Maisome, Ziwa Victoria na kukamilisha ujenzi wa magati ya Bukondo, Kinesi, Shirati na Nansio katika Ziwa Victoria. Aidha, Serikali itaendeleza ujenzi wa magati ya *Mbamba Bay* na Manda katika Ziwa Nyasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gati la Nkoma, gati hili lina urefu wa mita 15 na upana wa mita 5. Kina cha maji kuzunguka daraja hilo ni meta 1.0 tu hivyo linatumiwa na meli ndogo na mitumbwi tu. Lilijengwa na wananchi kama gati la muda. Nawashukuru sana wananchi wa Geita kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Nafurahi kumhakikishia Mheshimiwa Mabina na wananchi wa Geita kwamba, gati la Nkoma limewekwa katika mpango wa utekelezaji wa ukarabati wa magati kwa mwaka 2004/2005. Uendelezaji wa gati la Muharamba utafanywa baada ya kukamilika ujenzi wa gati la Nkoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa James Musalika na Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Wabunge kutoka Geita, wamekuwa mstari wa mbele katika kutatua matatizo ya wananchi wa Geita. Wametusaidia sana katika kuendeleza na kuimarisha mawasiliano na uchukuzi Geita na nchi nzima. *(Makofi)*

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Nashukuru sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, gati ni kiungo kizuri katika usafirishaji na sasa hivi nimesikia kwamba, Serikali imefanya mpango wa kuleta meli za *speed* katika Ziwa Victoria na ili ziweze kusafiri na kwenda katika maeneo mbalimbali lazima kuwe na magati hayo. Je, Serikali itamaliza lini kwa sababu hata yale Magati ya Kimesi na Bukondo bado hayajamalizika na sasa hivi tunafanya mpango wa kuongeza magati mengine, je, Serikali itayamaliza lini hayo magati au tunasubiri mpaka mwaka 2005 uishe?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, gati la Kimesi litamalizika mwezi wa nane. Gati la Shirati litamalizika mwisho wa mwezi wa sita. Gati la Bukondo litakwisha mwisho wa mwezi wa kumi. Kwa maana hiyo, tunatekeleza programu kama tulivyopanga. Matumaini yetu ni kwamba, Gati la Nkoma linaweza likaisha katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu. Vile vile ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mabina kwamba, pale ambapo fedha zinatengwa na Serikali katika Bajeti huwa tunajitahidi sana kutekeleza mipango ya ujenzi wa gati kama tulivyopanga. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na uamuzi huu mzuri na wenye hekima na busara uliofanywa na Serikali kwamba, Mamlaka ya Bandari ichukue gati pamoja na ya Kasanga na Karema na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri mwenyewe alifika pale Kasanga na akakuta kuna jengo limejengwa juu ya gati lenyewe na ile gati sasa inaanza kuharibika kutokana na kuelemewa. Je, anaweza akatueleza hatua za Serikali zinazochukuliwa hivi sasa kwamba gati litaanza kujengwa lini na lile jengo lililo juu ya gati litabomolewa lini ili kutoa nafuu kwa gati ambalo sasa linaanza kuharibika?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2003/2004, shilingi milioni 50 zilitengwa kwa ajili ya ukarabati wa Gati la Kasanga. Hivi sasa *Marine Services Company* inawasiliana na Mhandisi wa *TANROAD* wa Mkoa wa Rukwa ili kuangalia jinsi gani Mhandisi huyo anaweza kuwa Wakala wa kusimamia ujenzi au ukarabati wa Gati ya Kasanga. Matumaini yetu ni kwamba, hitilafu zote zilizojitokeza zitarekebishwa katika mpango huu wa ujenzi na ukarabati wa Gati la Kasanga mwaka huu na mwaka kesho.

Na. 47

**Simu - Tarafa ya Umba**

**MHE. CHARLES H. KAGONJI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipojibu swali langu Na. 384 kuhusu kupeleka huduma ya simu Mnazi ilisema kuwa Tarafa ya Umba bado wana hisa hawajakubaliana kuhusu ukaguzi wa hesabu za mwaka 2000 na kwa kuwa sasa muafaka umefikiwa kuhusu ukaguzi wa hesabu hizo:-

(a) Kwa kuwa *survey* tayari imekamilika; je, ni lini sasa kwa muda mfupi wananchi wa maeneo husika wategemee kupatiwa simu?

(b) Je, usambazaji huo wa simu utavihusisha vijiji gani na vingapi kuanzia Mtae, Mbaramo hadi Mnazi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Charles Kagonji, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL),* imeeneza huduma za simu bila waya *(Wireless Local Loop)* katika Wilaya ya Lushoto ikiwa ni pamoja na Lushoto Mjini, Soni, Bumbuli, Mtae, Magamba, Mazinde Juu na Mlalo yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa simu za mkononi maeneo yanayopata huduma za *Celtel* ni Lushoto Mjini na maeneo ya karibu yaani Kifungilo, Mombo na Soni. Kampuni hiyo, imekamilisha tathmini ya soko ya kiufundi ya maeneo ya Mlalo na Lukozi wakizingatia pia masuala ya kijamii na kimazingira. Utafiti umeonyesha kwamba, maeneo haya yanafaa kupatiwa huduma.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *VODACOM* inayo mawasiliano katika baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Lushoto kama vile Mombo na Bwiko ila hawana mawasiliano katika Mji wa Lushoto. *VODACOM* wanatarajia kufika Mjini Lushoto hivi karibuni baada ya kukamilisha maandalizi.

Mheshimiwa Spika, mpango wa sasa wa *TTCL* ni kutoa kipaumbele katika kuondoa mitambo ya zamani ya simu za kukoroga na kuweka mitambo ya kisasa. Maeneo yenye mitambo hiyo nchini ni pamoja na Kibiti, Utete, Ikwiriri, Mafia, Mtera, Mvumi, Tunduma, Mwakaleli, Kiwira, Litembo, Namtumbo, *Mbamba Bay,* Peramiho, Liuli, Itigi, Kiomboi, Misungwi, Ngudu, Malya, Nassa, Urambo, Bukene, Sikonge, Malampaka, Namanyere, Ruangwa, Nachingwea, Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje na Sirari.

Mheshimiwa Spika, baada ya mpango huo wa *TTCL*, mpango utakaofuata ni kupeleka huduma za simu sehemu za miji midogo na sehemu zenye wakazi wengi. Ni matumaini yangu maeneo ya Mbaramo na Mnazi yaliyo katika Jimbo la Mlalo yatapata huduma ya simu za *TTCL* katika mpango huo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Charles Kagonji na Mheshimiwa Henry Shekiffu, Wabunge wa Wilaya ya Lushoto, wamekuwa mstari wa mbele katika

kusukuma maendeleoya Lushoto kwa ujumla na hasa sekta ya mawasiliano, nawashukuru. *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi sana kwa majibu mazuri ya Waziri. Kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ni kubwa na ina watu wengi na katika maeneo ambayo yamekwishafanyiwa *survey* yako maeneo ya jirani. Naibu Waziri alipotembelea Lushoto aliahidi kwamba maeneo zaidi yatafanyiwa *survey.* Nilitaka kupata ufahamu katika maeneo ambayo ni jirani na Lukozi na Mlalo yako maeneo kama Mlola, Kwekanga, Mkuzi ambayo ni jirani. Haionekani kwamba ni muhimu na maeneo haya ya Kwekanga, Malibwi, Milola, pamoja na Bumbuli yakapatiwa nayo huduma za simu ?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, maeneo yote aliyoyataja nimeyaorodhesha na yatafanyiwa uchunguzi au utafiti ili kuona kama inawezekana tukapeleka hizo huduma mapema iwezekanavyo. Lakini nilitaka kumhakikishia Mheshimiwa Shekiffu kwamba, nia yetu ni kwamba ikiwezekana katika kipindi cha mwaka mmoja unaokuja, huduma za simu za mkononi ziwe zimefika katika kila Wilaya na ikiwezekana katika kila Tarafa nchini. Kwa hiyo, maeneo aliyoyataja nayo yatafikiwa.

Mheshimiwa Spika, teknolojia ya mawasiliano imeendelea sana kiasi cha kwamba uwezekano huo ni mkubwa sana. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Nashukuru sana kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri. Lakini ningependa kujua kwa kuwa *Celtel* walishaleta dodoso kwenye eneo la Bumbuli na limejazwa kuhusiana na wanaohitaji simu na vigezo vyote vimetimizwa. Je, si sawa kwamba iliunganishwa na sehemu za Lukozi na nyingine hizo kwa maelezo niliyopata, maana hakuitaja mwanzoni katika maeneo ambayo yalipewa umuhimu wa kwanza?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba niiongeze Bumbuli katika orodha ya yale maeneo ambayo tayari yamefanyiwa utafiti au maeneo ambayo vile vile tunafikiria kuyapatia huduma za simu za mkononi hivi karibuni.

Na. 48

**Ubinafsishaji wa Kiwanda cha Pareto - Mafinga**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilipobinafsisha Kiwanda cha Pareto - Mafinga ilitoa maelezo kuwa mwekezaji aliyepatikana alikuwa na uwezo wa kifedha na kiteknolojia na wananchi wa Mikoa ya Iringa, Mbeya, Arusha na kadhalika, ambao wanalima zao hilo walikuwa na matarajio makubwa ya kufufua zao hilo na kwa kuwa ni kipindi kirefu sasa tangu

mwekezaji alipokabidhiwa kiwanda hicho hajaonyesha uwezo wowote na zao hilo linazidi kuporomoka:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza kwa nini ilikitoa kiwanda kwa mwekezaji ambaye uwezo wake wa kukiendesha ni mdogo sana kiasi cha kumfanya ahitaji msaada wa Serikali kupata fedha za kuendesha kiwanda hicho?

(b) Kwa kuwa tatizo la soko la bidhaa inayozalishwa kiwandani hapo lilikuwepo hata kabla mwekezaji huyo hajapewa kiwanda, je, aliieleza vipi Serikali katika kulitatua tatizo hilo kabla ya kupewa kiwanda?

(c) Kwa kuwa jibu la matatizo ya bidhaa iliyopo kiwandani hivi sasa ni kuwa na kiwanda cha kutengeneza dawa za kuulia wadudu, je, ni lini mwekezaji huyo atafanya hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufundi Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kiwanda cha kuzindua maua ya pareto cha Mufindi kilibinafsishwa kwa kampuni ya *International Chemicals Producer* ya Afrika Kusini mwaka wa 1998 baada ya kampuni hiyo kutimiza masharti yote muhimu yaliyowekwa ikiwa ni pamoja na kuwa na uwezo wa kukinunua kiwanda hicho, kukikarabati, kufufua uzalishaji na kununua maua yote ya pareto kutoka kwa wakulima.

Kabla ya kubinafsishwa, uzalishaji wa pareto ulikuwa umeshuka kutoka tani 2,500 mwaka wa 1991/1992 hadi tani 138 mwaka 1997/1998. Kushuka kwa uzalishaji kulitokana na wakulima kukopwa pareto yao kwa muda mrefu na kutokuwa na uhakika na soko. Baada ya mnunuzi kukabidhiwa kiwanda, aliongeza usindikaji wa pareto kutoka tani sita kwa siku katika mwaka wa 1997/1998 hadi tani kumi na tatu kwa siku katika mwaka wa 2003/2004. Kufuatia ongezeko hilo la usindikaji, uzalishaji wa maua ya pareto uliongezeka kutoka tani 138 mwaka 1997/1998 hadi tani 4,000 mwaka 2000/2001. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba, mnunuzi wa kiwanda alikuwa na uwezo wa kukiendesha kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, wakati mnunuzi alipokabidhiwa kiwanda mwaka 1998, Soko la Dunia la Pareto lilikuwa zuri na aliweza kuuza tani 160,187 za sumu ghafi ya pareto kwa dola za Kimarekani 9,773,390. Soko la Dunia liliporomoka ghafla kati ya mwaka 2001 na 2003 kutokana na uzalishaji wa pareto kuongezeka katika nchi wazalishaji. Aidha, matumizi ya dawa igizi yaliongezeka na kufanya hali kuwa mbaya zaidi. Mambo hayo mawili yalisababisha mlundikano wa sumu ghafi kiwandani hadi kufikia tani 40, hali ambayo ilisababisha mwekezaji aache kununua maua ya pareto kutoka kwa wakulima. Kutokana na hali hiyo, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi iliona ni busara kuingilia kati kwa kumdhamini mwekezaji huyo ili kumwezesha kupata mkopo wa

shilingi bilioni 1.48 wa kumwezesha kununua pareto iliyokuwa mikononi mwa wakulima.

(b) Wakati mwekezaji anakabidhiwa kiwanda, Soko la Dunia lilikuwa zuri na ndiyo maana aliweza kuuza nje tani 160,187 za sumu kati na kujipatia dola za Kimarekani 9,773,390. Tatizo la soko lilijitokeza baada ya mwekezaji kukabidhiwa kiwanda.

(c) Ni kweli kuwa ili kupata soko la sumu ya pareto la uhakika ni muhimu kuwa na mtambo wa kuchuja sumu hiyo. Mwekezaji wa kiwanda cha pareto kwa sasa ana mpango wa kujenga mitambo ya kuchujia sumu ya pareto na wawekezaji wengine wameonyesha nia ya kufanya hivyo. Serikali inafuatilia kwa karibu utekelezaji wao lakini ni vigumu kusema kwa uhakika mipango hiyo itakamilika lini kwa kuwa inategemea mipango ya wawekezaji hao.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, anasema kwamba ni vigumu kutabiri sasa mwelekeo mzima kwa zao la pareto nchini. Sasa kauli hii ni vizuri tukauliza Serikali inachukua hatua gani kwa wakulima wa pareto katika nchi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, inawezekana kutabiri lakini ukishatabiri huna uhakika kama ulichotabiri kitatekelezeka kwa 100%. *(Kicheko)*

Sasa nieleze tu kuhusu suala hili, soko la pareto lipo hasa baada ya kuona Wamarekani na Ulaya hawapendi tena kununua dawa zenye igizi wanataka kununua dawa kama ilivyo. Kwa hiyo, kwa sasa soko linatabirika na lipo. Lakini kama unavyojua, soko linategemea *supply and demand,* hatuwezi kusema kwa hakika kama ghafla kila mtu ataanza kulima tena kwa wingi kama hapo nyuma, ni vigumu kusema kitatokea nini lakini soko sasa lipo kwa sababu dawa igizi haziwavutii sana wawekezaji.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa huyo mwekezaji alipowekeza mlidhani ana hela za kutosha zilipomuishia akawaomba mumsaidie mkopo na kwa kuwa sasa hamuwezi kutabiri kama atawekeza na atapata faida na iwapo ataendelea kupata hasara bado na hizo mlizomsimamia kukopa hamwoni kwamba mtapata hasara?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, hatutarajii kupata hasara kwa sababu bado pareto inatakiwa soko halijafungwa na hicho alichokopa ana uwezo wa kukilipa kwa sababu *assets* zote za kiwanda ni zaidi kuliko hiyo pesa ambayo amekopa na tunamfuatilia. Hatujamkopesha tu na kumwachia, hapana amepewa mkopo huo na ananunua pareto iliyopo na ikiisha tunamwongezea tena pesa.

Sio sisi peke yetu tunaoshughulika na suala hili ni Wizara au Serikali na Benki ya *Standard Charter,* kwa hiyo, tupo wabia wawili kufuatilia suala hili ili tusipate hasara kwa mkopo huu.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, ooh, samahani, Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu ya nyongeza.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuongezea jibu la nyongeza kwa jibu la Naibu Waziri. Huyo mwekezaji hakudhaminiwa na Serikali, ametumia utaratibu wa *Export Guarantee Scheme.* Kwa hiyo, isije kudhaniwa kwamba, Serikali imemdhamini mtu binafsi, hapana, ametumia utaratibu wa kawaida wa *Export Guarantee Scheme* na Benki iliyompa mkopo, dhamana ambayo Benki imeikubali ni kiwanda chake ambacho anacho hicho cha pareto.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Kuna tangazo moja tu la kikao limetoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Katibu wa Kamati ya Wabunge Wanawake wa CCM, ananiomba niwaarifu Waheshimiwa Wabunge wa CCM Wanawake kwamba, leo tarehe 15 Juni, 2004 baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge saa saba kutakuwa na kikao cha Wabunge hao Chumba Na.133, ghorofa ya kwanza.

La pili, Waheshimiwa Wabunge, jana Wasaidizi wangu walighafirika kubandika orodha ya wasemaji wa siku ya jana, leo tunasahihisha upungufu huo, orodha hii ya wasemaji wa leo itakuwa kwenye ubao wa matangazo ili kila mtu ajue kama yuko kwenye zamu ya leo au ya baadaye. Kwa maana hiyo, wasemaji wanne wa kwanza watakuwa Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Goerge Mlawa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, ndio watajaza saa ya kwanza ya mjadala.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005 na Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2003 na Mwelekeo wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2004/2005

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nichangie hoja mbili zilizoko mbele yetu, hoja ya Waziri wa Fedha na hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Kama kawaida yangu, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hizi kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii ni nzuri na ina lengo la kuwasaidia wananchi wa Tanzania. Nampongeza sana Mheshimiwa Basil Mramba, Manaibu wake na watendaji wake wote. Sina wasiwasi nao, kwani kwa haya machache tutakayowashauri watayazingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naanza na mishahara ya Walimu. Naomba Mheshimiwa Waziri, atuambie Walimu na watumishi wengine wengi waliambiwa wafungue akaunti zao *NMB* na mishahara yao ingeanza kupita huko mapema iwezekanavyo, mambo haya yamefikia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukichukua Walimu, wanapata taabu sana. Mwalimu ni lazima atumie zaidi ya siku tano kufuata mshahara wake Wilayani na Wilayani haupati siku hiyo hiyo na bado gharama anazotumia kwa nauli, kulala Wilayani, hazilipwi. Jana Mheshimiwa Omar Kwaangw', wakati anachangia alizungumzia juu ya madeni ya Walimu. Haya madeni yanayosemwa siyo yote bado Walimu wengi hawajui haki zao, wanatumia nauli zao, lakini hawalipwi. Kule Wilayani kumekuwa na wajanja wengi ambao wanadhulumu haki za Walimu. Nashauri sasa kwa makusudi Serikali iunde Tume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi Kamati ya Huduma za Jamii walikuwa na mkutano wao na bahati nzuri walinikaribisha, kuna mambo mengi sana Walimu wanadhulumiwa. Naomba Serikali iliangalie suala hili kwa uzito wake.

Mheshimiwa Spika, hapa hapa ndani ya Bunge hili, niliomba Walimu na wafanyakazi wengine wa Iramba ya Mashariki akaunti zao zihamishiwe Singida Mjini, ambako wanaweza kwenda asubuhi wakachukua mshahara na karudi kituo cha kazi, zikiendelea kubaki *NMB* Kiomboi ni lazima watumie siku tano na hiyo ni hasara kwa watoto wetu wanaosoma shule, *syllabus* haiishi kila mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nije upande wa kuondoa umaskini. Awamu ya kwanza ya kuondoa umaskini wananchi wetu hata hawakuiona walikuwa wanasikia tu sasa tuko awamu ya pili. Kuondoa umaskini ni kuwasaidia wale wananchi wetu wanaokaa vijijini sio hawa wengine ambao hawataki kukaa shamba, wanakaa mijini na kazi hawana. Ninashauri hii Sera ya Kuondoa Umaskini ianzie chini kwenda juu, tusianzie juu kwa semina za ajabu ajabu, hapana, twende kule vijijini. Kuwaondolea wananchi wetu umaskini ni kuwapa uwezo wa kuweza kulima mashamba ya kutosha bila hivyo kwa kweli tutakuwa hatujafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nalishukuru sana Shirika la *PAS,* ambalo liko Morogoro, ambalo linashughulika na kuwasaidia wakulima wadogo wadogo. Nimetembelea Morogoro na Iringa, kwa kweli kazi yao ni nzuri, wao ndio wanawasimamia wananchi kupata mikopo kutoka Benki ya *CRDB.* Naomba sana shirika kama hilo lipewe nguvu na Serikali iwawezeshe wananchi kupitia Shirika hilo na lienee Mikoa yote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda Kilosa, Morogoro Vijijini na Iringa, mashamba wanayolima wananchi wetu kwa kweli ni ya kuridhisha. Naomba shirika hili lienee

Tanzania nzima, Mikoa yote iwe na shirika kama hilo na mashirika mengine yaige mfano wa *Private Agricultural Sector Support (PASS). (Makofi)*

Mheshimiwa Waziri mhusika, nimeshaanza kuongea na shirika hili wameonyesha nia ya kuja Iramba Mashariki, naomba sasa Serikali inisaidie. Mwaka huu walikuja kutembelea na kuona jinsi wananchi wa Iramba Mashariki wanavyojituma kulima alizeti na mazao mengine.

Mheshimiwa Spika, hatuwatendei haki wakulima wetu, mwaka 2003 humu humu ndani ya Bunge mliahidi kwamba fedha zitakwenda kwa wakulima, hakuna fedha zilizokwenda. Naomba mwaka huu jambo hili lipewe kipaumbele na shughuli zianze mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokuwa natembelea Morogoro nilipita Msamvu nikakuta majengo ya *TANSEED,* hayo majengo yako kwenye hali mbaya sana, wananchi wetu wanahitaji mbegu lakini hakuna kinachofanyika hapo. Nashangaa kwa nini mpaka leo Serikali inakataa kuuza shirika hilo hasa lililopo Morogoro, ikinunua kampuni au mtu binafsi atazalisha mbegu za kutosha. Morogoro iko katikati ya Mikoa ya Iringa, Dodoma, Morogoro yenyewe, Singida mpaka Tabora, watapata mbegu kutoka hapa. Hebu tuache ubabaishaji. Sasa hivi Serikali inajitoa kwenye biashara, kwa nini shirika hili mpaka leo haliuzwi, majengo pale yanaoza hakuna kinachofanyika? Hapo nimemaliza na nitafuatilia kuhakikisha kwamba, kwa kweli Serikali inampa shirika hili mtu anayeweza kuliendesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Waziri kwenye hotuba yake, amesema sasa hivi *Passport* zetu zitapewa *stickers* badala ya ule mtindo uliokuwa unatumika zamani ambapo fedha nyingi sana zilikuwa zinaliwa na wajanja huko kwenye Balozi zetu za nje, ni wachache walikuwa wanawasilisha fedha. Naipongeza sana Serikali kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni ununuzi wa vifaa vya Serikali. Sasa hivi hapa ndani ya nchi tuna viwanda vizuri sana vinavyotengeneza *furniture* mbalimbali na vyombo vingine, kwa nini tung’ang’anie kuagiza vyombo hivi kutoka nje? Hayo ni matumizi mabaya ya hela za Serikali. Kama kitu kinapatikana hapa, kinunuliwe hapa na wale wanaotengeneza wapewe uwezo wa kutengeneza vingi zaidi na vizuri zaidi kutosheleza mahitaji yetu. Kwa hiyo, naomba sana Serikali izingatie kwa sababu tunakokwenda ni kubaya mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara zimepewa fedha za kutosha, Wizara ya Kilimo hatujaona makucha yake kama vile Wizara ya Maji, naipongeza sana Wizara ya Maji sasa hivi kila mahali tunapata maji na wananchi wameridhika, malambo yanachimbwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa kazi anayoifanya, nina imani hata visima vyangu viwili tutamalizia kipindi hiki. Vile vile nimpongeze sana kwa maji ya kutoka Ziwa Victoria. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Waziri wa Ujenzi, kwa kweli nitakuwa sina fadhila nisipompongeza kwa sababu barabara zangu Jimboni kwangu wanatengeneza Wachina, ni nzuri kuliko barabara za lami, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Mawasiliano naye nampongeza, mnara umeshasimama Iramba lakini kazi haijaanza. Alituahidi kupata simu Iguguno, Nkungi na Kinampanda toka mwaka 2000, tunaomba atimize ahadi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikija kwa Waziri wa Nishati na Madini, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha. Tuliahidiwa umeme toka wakati wa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda mwaka 1995 mpaka leo ulikuwa haujafika lakini Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha amesimama kidete sasa hivi kazi hiyo inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aliyeshughulikia suala hili alikuwa ni Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa hiyo, namtaja kwa jina. Najua alikuwa anaagizwa na Mheshimiwa Daniel Yona lakini niwashukuru sana wote. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia niende TAMISEMI, kwa kweli Wizara yetu inajitahidi lakini kuna watumishi ambao wanazorotesha maendeleo ya Halmashauri zetu. Wabunge mbalimbali wameandika mpaka leo utekelezaji hakuna. Mimi na Mbunge mwenzangu wa Iramba Magharibi, tumeandika barua zaidi ya nne, kuna watumishi watatu pale wameshakaa muda mrefu sana Wilaya ya Iramba wamekuwa ni mzigo na kero kubwa, tunaomba waondolewe waende kutoa huduma sehemu nyingine. Hii ni pamoja na Wilaya nyingine ambazo hazifuati taratibu za Serikali. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi TUMITAA ilishafutwa iko Tume ya Utumishi, naomba kabla hawajaanza kazi zao, wasafishe wale watumishi ambao ni mzigo. Kuna watumishi Wilayani ambao hawawezi kuhamishwa bila kibali cha Waziri wa TAMISEMI. Tunamshauri Waziri atoe vibali wale watu waondoke na ikiwezekana kama hawawezi kuhamishwa wabaniwe matumizi kwa sababu ni hasara kubwa kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema Wizara ya Elimu ifuatilie hela za MMEM zinazokwenda kwenye Halmashauri nyingi hazifiki au zinawekwa kwenye *General Fund* zinafanya kazi nyingine. Fuatilieni sana juu ya hilo. Mifano ipo na tunashukuru Hazina wanatoa *allocation* na wanaonyesha kabisa hela ngapi wamepeleka wapi, kama ni hela za uhamisho wanaonyesha, hela za MMEM wanaonyesha, lakini kuna wakorofi kule kwenye Halmashauri naomba hao washughulikiwe sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie kumpongeza sana Waziri wa Fedha, Wasaidizi wake na Watendaji wake, kwa kazi nzuri wanayofanya, waendelee na moyo huo, nashukuru. *(Makofi)*

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie katika hoja hizi mbili za Mipango na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, kabla sijachangia, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kusimama hapa kama Mbunge wa Kisarawe, napenda nitoe rambirambi zangu kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na kwa Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kuondokewa na baba mpenzi. Namwomba Mwenyezi Mungu, aiweke mahali pema peponi roho ya marehemu na awape subira kuvumilia maumivu haya. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, pia napenda nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga, Chama cha Mapinduzi na wananchi wa Bariadi Mashariki, kwa ushindi mkubwa uliopatikana katika uchaguzi uliopita. Namwambia mwanangu Makanga, karibu tena Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Rais wetu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Profesa Anna Tibaijuka, kwa kuteuliwa kwao na Waziri Mkuu wa Uingereza, kuwa Makamishna katika Tume ya Kutathmini Vikwazo dhidi ya Maendeleo ya Afrika. Uteuzi wao umeiletea sifa nchi ya Tanzania na ninaamini kwamba, utakuwa na manufaa makubwa katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu, naanza kuwapongeza kwa dhati kabisa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Waziri wa Fedha, ndugu yangu Mheshimiwa Basil Mramba, kwa bajeti nzuri sana. Bajeti hizi ni nzuri hakuna sababu yoyote ya kutokuziunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, Wabunge tunao wajibu wa kutoa maoni yatakayowawezesha Mawaziri hawa kuboresha mipango ya Serikali na kama alivyosema Waziri wa Fedha katika Ibara ya 53 ya hotuba yake, ametuomba Wabunge tuchangie ili tuweze kumsaidia. Nafikiri hili tunalifanya kama wajibu wetu.

Mheshimiwa Spika, ili tuweke sawa mipango yetu ya mwaka unaofuata kama walivyofanya watoa hoja, hapana budi tuone tumejifunza nini katika bajeti tunayomaliza kuitekeleza. Kwa mujibu wa hotuba zote mbili, tumeshindwa kufikia lengo la 6.3% la kukua kwa uchumi na tumeshindwa kudhibiti mfumuko wa bei kwenye lengo letu la 4% tulilojiwekea. Sababu kubwa ambazo zimetolewa pale ni ukame na bei za mafuta hasa ya kuendeshea mitambo ya *TANESCO.* Lakini mimi nasema hizi sio sababu tu pekee. Kama anavyokiri Mheshimiwa Mramba katika vifungu vya 29 na 53, uwezo wetu wa utendaji kazi katika maeneo mengi ni duni na kwamba huko nyuma ni wazi kabisa tulikuwa hatuzingatii dhana isemayo ‘kupanga ni kuchagua’. Hapanabudi kuweka vipaumbele katika sekta zitakazotuletea tija kubwa, tena katika muda mfupi na tayari tuweze kubadilisha vipaumbele hivyo jinsi muda unavyobadilika.

Kwa maoni yangu, tutapata maendeleo ya haraka tukiweka uzito kule vijijini waliko Watanzania wengi. Kwa hiyo, sekta ambazo zitatuletea mafanikio ya haraka vijijini kwangu mimi naona ni kilimo, maji, mifugo, nishati, ujenzi kwa maana ya ujenzi wa barabara vijijini na Tawala za Mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huko nyuma bajeti zeti zilikuwa zinatawanya nguvu na raslimali zetu kwenye maeneo mengi bila kuweka uzito katika maeneo ambayo yanaweza

kutupeleka haraka. Nafurahi kusema kwamba, katika Bajeti hii sasa tumeanza kuweka uzito mahali panapostahili. Kwa mfano, ukiangalia bajeti ya maendeleo, kati ya shilingi bilioni 771,949 zilizotengwa, sekta hizi nilizozitaja zimepewa karibu asilimia 57.6. Naipongeza sana Serikali kwa kuliona hili, naamini kwamba tutavuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiwa hapa kwenye shughuli za vijijini labda nitoe shukrani zangu za dhati kabisa katika sekta mbili kati ya hizo nilizozitaja. Kwenye sekta ya ujenzi, namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kwa kutujengea barabara yetu ya lami mpaka Kisarawe na ni mategemeo yangu kwamba, ataongeza ili kusudi ifike mwisho wa barabara hiyo ambayo ni kilomita 195 kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Vile vile namshukuru Mheshimiwa Edward Lowassa, kwa jitihada kubwa sana ya kueneza maji vijijini katika Wilaya yangu hususan kwa mara ya kwanza kutupatia malambo. Ninaamini kwamba, sasa nguvu ya wananchi wa Kisarawe, hasa akina mama, itatumika zaidi katika kuzalisha badala ya kwenda kutafuta maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine inayotusibu katika uchumi wetu ni kushindwa kuwadhibiti wafanyabiashara wadanganyifu. Pamoja na kuwa soko la ushindani ndilo ambalo linatawala bei, lakini bado wapo wafanyabiashara ambao wanatumia mianya ya usimamizi mbovu kuwatapeli wananchi. Kwa mfano, tumepata tatizo la mafuta kupanda bei lakini baada ya Saudi Arabia kuongeza uzalishaji wa mafuta hivi karibuni, bei za mafuta duniani zimeanza kushuka. Kwa ajabu, hapa Tanzania bei za mafuta ndio zinazidi kupanda. Kwa hiyo basi, kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba jinsi bei zinavyoteremka kule kwenye Soko la Dunia na hapa kwetu zishuke ili wananchi wafaidike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa vile mafuta yametugharimu sana hususan kuendesha mitambo ya *TANESCO* na kwa kuwa katika bajeti hii tunaambiwa kwamba, Mradi wa Songosongo utaanza kutoa gesi kuanzia mwezi ujao, naishauri Serikali iisimamie vizuri *TANESCO* ili badala ya kutumia pesa nyingi katika kununua mafuta, sasa tuelekeze nguvu zetu katika kutumia gesi ya Songosongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuvuka lengo la ukusanyaji mapato na kuwashukuru wahisani kwa kutimiza ahadi zao. Kama tulivyoelezwa kwamba katika kipindi cha miezi sita tayari 90% ya ahadi zao imetolewa. Huko nyuma miradi mingi ilikuwa ikichelewa kwa sababu ya wahisani kutotimiza ahadi zao na matokeo yake ni kushindwa kuitekeleza. Sasa hali hii imegeuka, ni juu yetu kuongeza kasi ya utekelezaji ili miradi yetu iweze kutekelezwa kwa wakati na uchumi ukue kama tulivyopanga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tanzania kukosa uhuru wa kuelekeza misaada hiyo, hapana budi tatizo hili litatuliwe kwani linatunyima fursa ya kufanya mambo mengi yakiwemo kutotekeleza dira yetu, kushindwa kutekeleza matakwa ya wananchi na kuichonganisha Serikali na wananchi wake kwa kuona kwamba, kuna maeneo maalum yanayopendelewa kumbe si hivyo. Haya ni matakwa ya wahisani. Kama tukishindwa kuwashawishi ili watupe uwezo huo wa sisi kuamua, basi dawa pekee kwa kweli ni kuachana na bajeti tegemezi.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kusema kwamba, katika bajeti hii inaelekea kwamba tunaelekea huko kwani kama tulivyoelezwa, mwaka tunaoumaliza ni kwamba, utegemezi wetu umekuwa wa asilimia 45 na hivi sasa tunalenga kushuka mpaka asilimia 41. Mategemeo yangu ni kwamba, baada ya kupata maoni haya ya Wabunge, Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba, tunazidi kupunguza utegemezi ili tuweze kuamua utekelezaji wa mipango yetu kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, niipongeze pia Serikali kwa kukamilisha muhula wa kwanza wa mkakati wa kupunguza umaskini na kuweza kuchapisha taarifa ya tatu ya utekelezaji wake. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ameorodhesha katika kifungu cha 31 cha hotuba yake, vikwazo vinavyokwamisha sekta ya kilimo katika bajeti hii hasa chini ya vifungu 32 mpaka 34 vya hotuba yake, kuna maelezo kuwa hatua mbalimbali zinachukuliwa kupunguza makali ya vikwazo hivyo. Napenda kuishauri Serikali kuwa pamoja na hatua zilizoorodheshwa hapo, Serikali iendeshe kampeni ya kila mtu afanye kazi ili kukuza idadi ya wafanyakazi hasa wa kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa Serikali wa kudhamini wakulima wadogo wadogo ili waweze kukopa kutoka katika benki za biashara, napenda ieleweke kuwa wakulima wadogo wadogo hawataweza kuitumia fursa hiyo ya mikopo iwapo hakutakuwa na kampeni maalum ya kuwaelimisha namna gani wanaweza kuifikia mikopo hiyo, wengi watakuwa wamekaa tu lakini hawajui namna gani wanaweza kupata mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye matumizi ya bajeti tunayoijadili, nakubaliana na vigezo vilivyotumika katika mgao vinavyoelezwa katika kifungu cha arobaini cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Lakini kuhusu kigezo cha sita kinachozungumzia ujenzi wa barabara, kama nilivyokwishasema hapo awali, sasa ni wakati wa kutoa kipaumbele kwa barabara za Vijijini ambako ndiko walipo wananchi wengi na wakulima wenyewe.

Kwa kufanya hivyo, tutarahisisha ufikishaji wa pembejeo kwa wakulima, uenezaji wa huduma za ugani na usafirishaji wa mazao yao ili yafike kwenye masoko.

Mheshimiwa Spika, napenda niipongeze Serikali kwa kuanza kutumia utaratibu wa *BOT* kuanzia na Jengo la Bunge. Lakini niseme tu kwamba, utaratibu huu ingawa inasemekana unataka uingie kwenye barabara, basi ni vizuri Serikali iutumie zaidi katika barabara kuu badala ya barabara za Vijijini, kwani barabara za Vijijini hazitakuwa na uwezo wa kumudu gharama za kurejesha kwa hawa watu watakaokuwa wanapewa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza kuwa, nakubaliana na mapendekezo yote ya Waziri wa Fedha kuhusu muundo wa kodi tena nampongeza sana kwa kuona kwamba, sasa hivi bajeti hii imefanya marekebisho ya kodi kuwaondolea mzigo mkubwa watu wa hali ya chini. Lakini sikubaliani na uamuzi wa kupandisha kodi ya vinywaji baridi. Kwanza ongezeko la shilingi mbili na nusu kwa lita halitaisaidia bajeti ya Serikali.

Lakini itakuwa kero kubwa sana kwa walala hoi. Namshauri Mheshimiwa Waziri, afute ongezeko hili kwani angalau sisi wa Pwani kule tunaweza kuhamia kwenye madafu lakini Wasukuma wangu na Wanyamwezi tutawalazimisha waende wakanywe pombe za kienyeji na mimi sioni kama hilo litakuwa jambo la busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Basil Mramba, kama nilivyokwishasema, ameomba ushauri wetu Wabunge na sisi tumempatia. Kwa hiyo, ni mategemeo yangu kuwa ushauri huo yeye na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, watauchukua.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumaini kwamba haya yatafanyika basi sina sababu ya kutokuunga mkono hoja hizi. Naziunga mkono mia kwa mia na ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE F. MLAWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hizi mbili za Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha. Kwanza kabisa, ningependa nami nitoe pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao na namwomba Mwenyezi Mungu amweke mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa tena na kurudi Bungeni. Mheshimiwa Makanga amedhihirisha umuhimu wa dhana ya demokrasia ndani ya Chama kwa uhai na maendeleo ya Chama chochote kile cha siasa. Chama chenye demokrasia ya ndani hukubalika na kuaminika na wananchi, vinginevyo hukataliwa na wananchi kama ilivyotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja hizi mbili bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa nitoe mchango wangu hasa nikijielekeza katika suala la kilimo ambacho ndicho hutegemewa na wananchi wengi wenye kipato cha chini ikiwa ni pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Kalenga, Iringa. Suala la kwanza juu ya kilimo ni mbolea, kutokana na matatizo yaliyojitokeza msimu uliopita baada ya bajeti ya mwaka 2003, nashauri kwamba safari hii tuhakikishe mbolea ya kutosha inaagizwa nje ya nchi na *Tanzania Fertilizer Company* na iagizwe sasa ili ipatikane mapema na vile vile iagizwe mbolea nyingine kutoka Minjingu, nayo ipatikane mapema ili msimu wa mvua unapoanza mbolea hizo ziwe Vijijini.

Vile vile kuwa na usimamizi madhubuti ili kuhakikisha kuwa, mbolea inayomfikia mkulima inakuwa ya bei nafuu kama inavyopitishwa na Bunge la Bajeti, yaani *whether* tunaweka ruzuku kwa ajili ya kulipia gharama za usafirishaji na kadhalika, sasa ule unafuu kweli mkulima auone.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nashauri Serikali iweke utaratibu unaotekelezeka kuhakikisha kuwa mbolea inafikishwa Vijijini siyo Mikoani. Hili linawezekana kama *Tanzania Fertilizer Company (TFC),* inaweza kuwa na Mawakala wake Vijijini, kwa mfano, kama Vyama vya Ushirika, wafanyabiashara na wengine, lakini *TFC* ihakikishe mbolea hii imefika Vijijini kwa walengwa. Sasa kama *TFC* inaweza kufikisha mbolea hii Vijijini vilevile wafanyabiashara wakubwa kutokana na ushindani huo watapeleka mbolea Vijijini na hiyo italeta unafuu kwa wakulima ambao ndio walengwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikopo au mitaji kwa wakulima, imeelezwa katika hoja hizi mbili azma ya Serikali kuongeza uwezo wa Mfuko wa Pembejeo wa Taifa, kukopesha pembejeo kupitia mabenki na Vyama vya Ushirika kwa Mikataba na vile vile kupitia *SCCULT*. Mimi naamini kwa dhati sana kwamba, tutaweza kuendeleza kilimo ikiwa wakulima wadogo hawa walio wengi watapewa fursa au kuwezeshwa kupata mitaji kwa kupewa mikopo kwa utaratibu unaoeleweka na ulio wazi. Mwaka 2003 au msimu uliopita, Vyama vya Ushirika kadhaa katika Jimbo langu la Kalenga, vilipewa mikopo kutoka Mfuko wa Pembejeo kupitia *SCCULT* kwa mara ya kwanza na kwa kweli mikopo hiyo imeleta msisimko mkubwa na wa ajabu kwa wakulima hawa na wamelima na wamezalisha mahindi kwa wingi sana. Unakuta kuna misitu ya mahindi katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa shukrani zangu kwa Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa na *SCCULT,* kwa kuwezesha hawa wanavijiji waliojiunga katika Vyama vya Ushirika, ambao baadaye tunategemea watakuwa *transformed* kuwa *SACCOS* imara kwamba waliweza kupewa mikopo hii na naomba hali hii iendelee. Kwa kweli wajibu wa kurejesha mikopo hii hawa wananchi wanaelewa sana, wala tusiwe na wasiwasi juu ya jambo hili. Sisi viongozi tuwaamini wakulima ikiwa ni pamoja na Serikali tutazame mfano wa *TASAF* na MMEM kuhakisha kwamba fedha zimekwenda huko Vijijini na zimetumika vema. Vile vile fedha zinazopelekwa kama mikopo zitatumika vema na zitarejeshwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi ningependa kuiomba Wizara ya Kilimo kwamba, *SGR* ianze kununua mahindi ambayo yapo kwa wingi sana kule Iringa ikiwa ni pamoja na Jimbo langu la Kalenga ili tuwe na soko la uhakika pamoja na hifadhi ya uhakika. Hiyo itawezesha mikopo ile iweze kurejeshwa, lakini wananchi wanakuwa na wasiwasi kwa sababu soko halieleweki na hawaelewi watauzia wapi. Kwa hiyo, *SGR* ianze sasa.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu mwanzoni tumefanya marekebisho ya Sheria ya Ardhi ambapo sasa Serikali za Vijiji zimepewa mamlaka za kutoa hati miliki za ardhi Vijijini na hivyo basi ku-*transform* ardhi Vijijini kuwa raslimali hai na hivyo basi kuweza kutumika kama *collateral* kwa ajili ya mikopo ambayo wananchi wanaweza kukopa. Sasa tungeomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kuwekwe mikakati madhubuti ya kuwezesha mabenki haya tuliyonayo yaanze kupokea hati hizo kama *collateral* na kama tukiwa na benki ya kilimo basi vile vile napendekeza kwamba, *SACCOS* za wakulima ziwe kati ya *shareholders* wa Benki hiyo ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, ningependa sasa kuzungumzia kilimo cha umwagiliaji maji. Tumeelezwa na Waheshimiwa Mawaziri kwamba, kuna hekta milioni 29.4 zinazoweza kumwagiliwa nchini. Lakini katika hizo hekta milioni 2.3, zina uwezo mkubwa wa kumwagiliwa, lakini eneo linaloendelezwa sasa hivi ni hekta 200,895. Sasa ukitazama *potential* tuliyonayo na kiwango ambacho tunamwagilia, uwiano wake ni kama utani. Kwa hiyo, lazima tufanye mabadiliko ya sera.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwanza suala la umeme, kwa vile umeme ni muhimu sana kwa wananchi, tukubaliane wazi kwamba, *source* kuu ya umeme itokane na makaa ya mawe ya Mchuchuma na gesi ya Songosongo na sehemu nyingine ambayo itapatikana kama *Mnazi Bay.* Hiyo ndiyo iwe *source* ya umeme. Maji yatumike kama kawaida kwa matumizi ya binadamu, mifugo, pamoja na kilimo cha umwagiliaji. Yaani *emphasis* iende huko juu ya utumiaji wa maji, yaani *vision* yetu huko mbele maji yaende kwenye kilimo cha umwagiliaji na kama kuna ziada katika maji hayo basi yanaweza kuongeza nguvu ya upatikanaji wa umeme. Tusigombee maji kati ya kilimo cha umwagiliaji na umeme. Kupanga ni kuchagua, tuchague *source* kuu ni makaa ya mawe. Mwenyezi Mungu, ametuwekea yapo pale *is just for the taking.* Kwa hiyo, naishauri Serikali hasa Waziri wa Mipango pamoja na Waziri wa Fedha, kubuni mipango ya dhati ili iweze kutekelezwa ipasavyo huko mbele ili maji tuliyo nayo tuyatumie kwa wingi sana kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji bila kuogopa kwamba tunaweza kuleta *shortage* ya umeme tunapotumia maji haya kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa nilizungumzie ni juu ya misamaha ya kodi kwa mashirika ya dini. Utekelezaji wa kutoa misamaha unaonekana umekuwa ni mgumu sana na wenye gharama kubwa na kwa vile Kamishana Mkuu wa *TRA* yupo, ningependa na yeye anisikilize kwa makini. Nitatoa mfano kuelezea suala hili. Katika Jimbo langu la Kalenga, kuna kituo cha Watoto Yatima kinaitwa Kituo cha Faraja. Kituo hicho kipo katika Kijiji cha Mgongo karibu na uwanja wa ndege wa Iringa wa Nduli na waendeshaji wa kituo hiki ni Wamisionari wa *Consolata Fathers,* Kanisa Katoliki Iringa. Pale kuna watoto wengi sana, watoto wachanga mpaka ambao wamemaliza shule ya msingi. Sasa wale Wamisionari wamejenga shule ya msingi kwa ajili ya watoto hawa pamoja na watoto wote wa Kijiji cha Mgongo wanasoma kwenye shule hii ambayo wamejenga wao. Vile vile wamejenga zahanati kwa ajili ya kituo hiki, lakini vile vile kwa ajili ya wananchi wa Kijiji cha Mgongo na wamejenga shule ya ufundi ambapo vijana wanajifunza taaluma mbalimbali. Pia wakitengeneza vitu mbalimbali kama vya useremala, vya vyuma na kadhalika, huweza kuviuza na hivi mbali ya kwamba ni kwa ajili ya mafunzo, lakini vile vile vinaleta hali ya kujitegemea kwa kiwango fulani kwa kile kituo kama wanapata biashara ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, sasa wale wamekuwa wanalalamika kwamba, wana kontena lina vifaa vingi vya ufundi liko bandarini kwa zaidi ya miezi mitatu. Sasa hilo ni jambo moja lakini kwa nini lipo pale kwa muda mrefu, ni kwa sababu ya *procedure* ya namna ya kuomba misamaha, kwamba misamaha lazima kwanza waende Hazina. Sasa Hazina ikishapokea maombi, huiandikia *TRA* hundi kuilipa kiwango kile ambacho kilitakiwa kilipwe na yule anayeomba msamaha, sasa kinalipwa na *Treasury*. Sasa nasema muda unaotumika toka pale wanapowasilisha maombi mpaka *Treasury* inailipa *TRA* ili uweze

kutoa mzigo bandarini, inachukua muda mrefu sana. Ikishatokea hivyo kwenda kuchukua mzigo bandarini unapambana na tatizo la *demurrage charges.* Kwa maana hiyo, mzigo kama umekaa pale bandarini kwa miezi mitatu, *demurrage charges* inakuwa ni kubwa sana na zile hazina *negotiation* lazima kulipa kama ilivyo. Kwa msingi huo, ukilipa *demurrage charges* kubwa sana hata msingi wa msamaha wa kodi unafutika, inakuwa kana kwamba hakuna ulazima tena wa kuomba misamaha hiyo, ni vema tu ukabiliane na kodi yote ili uweze kutoa mapema na usipambane na tatizo la *demurrage charges.*

Mheshimiwa Spika, sasa inaonekana hii *procedure* pamoja na kwamba, naelewa nia yake ni nzuri, lakini basi iwe *very efficient, very speedy.* Baada ya kupokelewa na kukubalika kwamba jambo hili linafaa kutolewa msamaha, basi liwe *expedited* ili hawa wanaoomba misamaha hii waweze kunufaika na manufaa yenyewe kwa kweli ni kwa ajili ya watoto wetu kama hicho kituo cha watoto yatima cha Faraja kule Iringa. Naomba basi Waziri wa Fedha pamoja na Kamishna Mkuu wa *TRA* pengine mngetazama tu hii *procedure* kama inaweza kurekebishwa ili kuongeza *efficiency* ili tatizo hili la kupambana na *demurrage charges* lisiwepo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili kutoa maoni yangu na ningependa niseme wazi kwamba, sina matatizo na hoja hizi mbili na naunga mkono bila matatizo yoyote. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hizi mbili za makadirio na mapato ya matumizi ya Serikali kwa mwaka 2004/2005 na pia hali ya uchumi na mwelekeo wa mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwanza niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, kwa kuwasilisha na pia sitazungumzia sana maneno mazuri waliyoyazungumza kwa sababu kawaida kwa kipindi ambacho mimi nimekuwa humu Bungeni sasa hivi nafikiri bajeti ya tatu na kipindi ambacho nimekuwa nafuatilia bajeti zote tangu huko nyuma, sijawahi kusikia bajeti ambayo haikupitishwa, sijawahi kusikia bajeti ambayo imeitwa mbaya na sijawahi kusikia bajeti ambayo haipitishwi mia kwa mia na wazungumzaji walio wengi. Kwangu mimi ningependa zaidi nipate kipimo cha bajeti nzuri kwa ku-*reflect* wadau wakuu au walengwa wakuu wa bajeti hizo ambao kwangu mimi ni wale asilimia kubwa ya Watanzania ukiacha wale watu ambao naweza kusema ni *high class* na *middle class*. Zaidi nitajielekeza kwa watu ambao ni *lower class.*

Mheshimiwa Spika, sisi wote tunatoka mashambani, wengi tumezaliwa huko na wengine sisi wachache tumebahatika kuzaliwa Mjini na tunatawala Majimbo ya Mijini lakini tunakwenda na Vijijini na hali za wananchi wetu Vijijini siyo siri kila mmoja anazitambua. Sasa tunapozungumzia bajeti nzuri, mimi ningefurahi kwamba bajeti nzuri iji-*reflect* na hali halisi ya ndugu zetu na wazazi wetu wanaoishi Vijijini. Bajeti nzuri kwangu mimi nitaiona ni nzuri iwapo nitakwenda kule Kashai au Bakoba nikakuta mwananchi ambaye mwaka 2003 nyumba yake alikuwa ameweka mti kwenye ukuta sasa amevunja akaweka matofali mawili, matatu na akaanza kuishi kwenye nyumba ambayo

ni bora. Lakini nikikuta ule ukuta umeanguka ameweka gunia, mimi naamini kwamba, huyu mtu hali yake inazidi kuwa mbaya mwaka hadi mwaka na kwamba bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na mipango mizuri ya maendeleo ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwangu mimi sioni kigezo chochote ambacho kinaweza kunipa imani kwamba, huyu mtu ameguswa na bajeti. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa utakuta tunaendelea kupitisha bajeti za kunufaisha watu au kundi fulani la watu wachache lakini walio wengi wanaendelea kuumia na wanaendelea kuwa mafukara.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nitashukuru kama wakati Waheshimiwa Mawaziri wote wawili wakiwa wana-*wind up* ni vizuri wakajaribu kutueleza kwa kweli kwamba hizi bajeti zinagota wapi? Kwa nini hali za watu walio wengi hazibadiliki na watu wanazidi kuwa maskini? Kwa kiasi kikubwa nitaomba watoe kabisa kwa ufasaha maelezo ambayo yatakidhi haja ya maneno aliyoyazungumza au aliyoyasoma Waziri wangu Kivuli, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa kweli bado yanatupa wasiwasi na tungependa kupata maelezo mazuri. Hususan ningependa kujua hizi takwimu ambazo Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, alizizungumzia hapa ambazo zimetolewa na *Bank of Tanzania,* juu ya pato la wastani la Mtanzania kwa dola, yaani bei za tangu mwaka 1995 kwamba pato la Mtanzania limekuwa linashuka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, mwaka 1995 alizungumza kwamba ilikuwa 85.2, mwaka 1996 ilikuwa 85.5, imepanda kidogo lakini mwaka 1997 ikashuka ikawa 81.3, mwaka 1998 ikashuka mpaka 78.5, mwaka 1999 ikashuka mpaka 68.5, mwaka 2000 ikawa 64.8, mwaka 2001 ikashuka mpaka 60.7 na mwaka 2002 ikashuka mpaka 57.2. Hizi ni takwimu za *Bank of Tanzania* wala si mtazamo labda wa mashirika ya nje. Sasa takwimu hizi zinapingana na hali halisi ambayo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsihaji, anatueleza kwamba, huu uchumi unakua au kama uchumi unakua kwa watu wachache tuelezwe. Takwimu hizi tunapewa na mashirika hayo ambayo Waheshimiwa hawa nafikiri wanayasimamia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia kuhusiana na bajeti ni kwamba, kwa kweli tumekuwa na mtindo wa kila bajeti kuja na mambo mapya mapya. Yaani kila bajeti ikija, Mheshimiwa Waziri anakuja na lugha tamu tamu, mpya na tunasahau zile tamu zilizopita na wala haionyeshi ile *sustainability* ya zile lugha tamu zilizopita. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, huwa anajua kuruka ruka kweli hapa kwenye jukwaa na *especially* akiwa anawasilisha ingawa mwaka huu naona amepunguza kidogo, nafikiri na yeye ana wasiwasi na hiki kitu alichowasilisha. Sasa mimi ningeomba kujua sababu ni nini, kwa nini hatuwi na mipango endelevu? Kwa mfano, mwaka 2003 imekuja lugha nzuri ya masuala ya kufuta kodi ya maendeleo. Nashukuru kwamba hii ilikuwa sera nzuri tu ya Wapinzani, CCM ikaichukua, tunashukuru siku hizi mnajifunza vizuri, tulishangilia wote.

Lakini Mheshimiwa Spika, wakati kodi ya maendeleo imefutwa kabla hatujakaa sawa ukaanza mlipuko kwamba umeme umepanda, bei ya mafuta imepanda, Muhimbili wanaanza kulipa shilingi elfu kumi ile kuingia tu na mambo mengine mengine yakabadilika kiasi kwamba Mtanzania wa kawaida, anashindwa kuelewa umaana wa kufuta kodi lakini hapo hapo hali yake ya kimaisha kwa mambo mengine inapanda. Sasa hii inawatia wasiwasi Watanzania kwa kutoelewa hasa mantiki ya haya mambo

yanayokuja kuzungumzwa, tumewafutia sijui leseni, gharama za pembejeo, wanashindwa kuelewa mantiki yake iwapo mambo mbalimbali yatapanda.

Mheshimiwa Spika, kuna suala hili la vitu muhimu ambavyo pindi vinapopanda au Serikali inaposhindwa kuvidhibiti kwa kweli hata bajeti hata kama mmepitisha bajeti nzuri namna gani, mambo yote lazima yatabadilika *automatically.* Kwa mfano, suala la kupanda kwa *petrol* ambalo Serikali inaonekana kabisa imeshindwa namna ya ku-*control* au kusimamia, bei za *petrol* kwa mwananchi wa Bukoba Mjini na Mkoa wa Kagera kwa ujumla na Kyerwa, Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi anazungumza hapa, *petrol* pindi inapopanda mwananchi wa Kagera ambaye yupo mwisho wa Tanzania kama unatokea Dar es Salaam, umemmaliza kabisa. Wakati ambapo mwananchi wa Dar es Salaam atakuwa ananunua mfuko wa sementi kwa Sh. 7,200/= wa Kagera atanunua sementi kwa shilingi 14,000/=. Utakapozungumzia mwananchi wa Dar es Salaam analilia nauli ya Sh. 200/= na anataka hata kuandamana, lakini kwa mwananchi wa Kagera kama atakuwa anatoka Bukoba Mjini kwenda Karagwe nauli itapanda mpaka hata shilingi 6,000/=.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ningeomba tufike mahali kama tunataka kuwasaidia Watanzania, kila mmoja ni bora basi kwa nafasi ile aliyopo, Serikali iangalie namna ya kumtazama na kunufaika kwa mazingira na hali yake ya kijiografia.

Mheshimiwa Spika, mimi niliwahi kuzungumza hapa Bungeni, sisi katika Mkoa wa Kagera na Wilaya nyingi za Mkoa wa Kagera, tunapata umeme wa Uganda, umeme wa Uganda ni *cheap* wala hauna maneno ya *IPTL* na huyu mwekezaji wa *Net Group Solution* kwamba umeme wake unakuwa aghali kwa sababu ya mitambo ya *IPTL*, tunaambiwa hivyo kwamba Serikali inalipa shilingi bilioni 3. Lakini wananchi wa Bukoba kwa nini wagharimie hizo shilingi bilioni 3 eti kwa sababu *TANESCO* inahudumia Tanzania nzima, lakini umeme tunaotumia sisi Bukoba Mjini ni wa Uganda ambao ni *cheap,* wala hauna biashara na *IPTL.*

Mheshimiwa Spika, lakini linapokuja suala la sementi, mabati na bidhaa nyingine ni kwamba, sisi tuna *share problem* sawa na mwananchi wa mahali popote pale Tanzania. Lakini gharama hizi sisi zinatuumiza za sementi, mabati na za usafirishaji eti kwa sababu tuko mbali na bidhaa hizi nyingi zinatoka Dar es Saalam. Ningeomba kwa kweli kama tunataka kuwa na bajeti ya kutusaidia sisi wote, masuala haya ni ya kimsingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nataka kuzungumzia suala la rushwa. Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia hapa. Hata tufanyeje kama tunapitisha bajeti ya mamilioni mengi tu, lakini Serikali haijaweka mipango sahihi ya kusimamia mapato na matumizi, kwa kweli tutakuwa tunafanya kazi bure. Imekuwa inapita lugha kila mara kwamba, toeni ushahidi wa rushwa. Mimi nafikiri ushahidi wa kwanza ambao kuanzia Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Mawaziri, wanapaswa wautumie ni kutumia takwimu na taarifa za vyombo hivyo hivyo ambavyo vimeundwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana kwamba katika taarifa mbalimbali ambazo zimekuwa zinatolewa ni kwamba, kumekuwa na upotevu wa fedha, lakini sisi tunaona si hoja taarifa zinapita na watu tunaendelea kuwa nao wale wale na Serikali inazidi kupoteza fedha nyingi tu, lakini kigezo kikubwa inakuwa ni rushwa. Mimi huwa nina mtazamo fulani kwamba, tunapopitisha bajeti hapa au wakati tunapokuwa tunajadili bajeti, wakubwa wa kunufaika na bajeti hiyo huwa wako pembeni wanasikiliza kwa hamu tupitishe mia kwa mia ili wapate cha mbele kutokana na mafungu yatakayopitishwa, kwamba mtu anaona hapa kwa jinsi nilivyosuka mipango yangu, imepita hatua ya kwanza na ya pili mpaka kwenye Baraza la Mawaziri ikapita, sasa mwisho ngoma ni Bungeni, Waheshimiwa Wabunge waipitishe mia kwa mia, akitoka tu anamwambia yule bwana, bajeti yangu imepita wewe aandaa mambo, lakini changu cha mbele tayarisha kabisa. Sasa Mheshimiwa Mbunge hapa anauliza cha mbele ni nini? Sasa sijui yeye atajaza, wanasema *atajiju. (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kama hatusimamii mapato na matumizi hizi shilingi trilioni 3.3 *one third* yake imengojewa kwa mkao wa kuliwa kabisa. Inasikitisha Wizara ya Elimu na Utamaduni, kwa mfano, nilikuwa nafuatilia taarifa mbalimbali, mnamo mwaka 1999, Wizara ililipa jumla ya shilingi milioni 146,791,000, hii ni taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuagiza *computer* kwa ajili ya kufundishia mashuleni. Sasa tunaambiwa kabisa katika taarifa hiyo kibali wala *tender* ya kununulia havikuwepo. Hiyo *tender* ilitolewa kienyeji na ikaja kugundulika kwamba hata *computer* hizo zilizokuwa *supplied* zilikwishatumika, lakini matokeo yake mwisho wa yote wala haieleweki mambo haya yameishia wapi. Nasikia kwamba hata Katibu Mkuu aliyekuwa kwenye Wizara ya Elimu na Utamaduni alishahamishiwa Wizara nyingine. Hiyo weka pembeni. Jeshi la Polisi katika taarifa kabisa inaelezwa kwamba, wako Maafisa walioagiza magari na bwana mwuzaji wa magari hayo akalipwa shilingi milioni 374,551,374 na ununuzi wa magari hayo haukupita kwenye *Central Tender Board,* lakini bwana huyo amechukua chake. Mheshimiwa Rais, anapopewa taarifa kama hizi na vyombo ambavyo ameviweka kukagua na kutoa taarifa, anataka Watanzania sisi ambao wala hatuna taasisi wala hatuna *PCB,* tumpelekee ushahidi. Sisi tunataka kabla Watanzania hata hawajatoa ushahidi aanze hawa basi. Mheshimiwa Waziri ukiniambia utasimamiaje fedha hizi ndipo nitapitisha.

Mheshimiwa Spika, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpe pole mtani wangu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mzazi, Mwenyezi Mungu, ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali sisi kila mwaka tunaipitisha hapa, kama alivyosema Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, kila bajeti tunapokuja hapa tunatoa sifa na kila moja inakuja na jina lake, tulikuja na bajeti ya mwelekeo, tukaja na bajeti ya matumaini, leo tuna bajeti ya kusaidia maskini na zote zinapita tu. Lakini bila kuangalia

kwamba bajeti ya mwaka 2003 na ya mwaka 2002, *performance* yake ilikuwa namna gani na ya mwaka huu tukiuliza iliyopita mwaka 2003 Mheshimiwa Basil Mramba pamoja na kuniangalia vizuri ni kwamba *performance* ya bajeti ya mwaka 2003 ime-*perform* namna gani, *hundred percent* ama imekwenda mrama? Hatupati jibu.

Mheshimiwa Spika, ripoti ya *Auditor General* alivyoisema mwenzangu ndiyo dira halisi ya namna gani *Ministries* ziko *serious* na bajeti zake. Ukiangalia Wizara nyingi, ukiacha Wizara moja tu siyo kwamba nataka kuifagilia, ameweka *priorities* ya mambo yake na yanaonekana yanafanyika hata ukitumwa leo kwenda kuangalia unaweza kukuta kwamba kitu kimefanyika. Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, unaweza kuziona barabara zinatengenezwa na kiasi gani cha fedha kimetumika, ukimwuliza anaweza akakuonyesha *performance budget* ya barabara zake imefanyika namna gani. Wizara zingine zinakwenda hivi hivi tu, hakuna *priorities* wala hakuna chochote, basi ilimradi tunafika miezi 12 inaisha, tunaitwa tena kuja kupitisha bajeti ya mwelekeo, kufuta umaskini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii kuna watu wengi sana wanashangilia kule mitaani sasa hivi kwamba ni bajeti ambayo imewasaidia wamachinga, *actually* bajeti hii imetia jela wamachinga kwamba sasa watafanya biashara bila leseni. Athari yake Wamachinga kweli wanafurahia, lakini hapa tulichofanya ni kumpanulia wigo wa kufanya biashara M-Asia wa Kitumbini na Uhuru Dar es Salaam ili aweze kuwapa bidhaa wale Wamachinga waingie barabarani wauze bila kulipa *VAT,* halipi kodi ya aina yoyote ile, huyu Mhindi, sisi tunashangilia tumemsaidia Mmachinga, *actually* hapa hatujamsaidia Mmachinga kwa lolote ila tumemsaidia baniani wa Kitumbini na *Uhuru Street,* ambao kwa muda mrefu hawalipi *VAT,* hawalipi *sales tax* na hawalipi chochote kile.

Mheshimiwa Spika na hili kama mnataka kuliona tulipojaribu kupitisha Sheria ya *VAT,* nafikiri ilikuwa sijui mwaka 1998 au 1996, sikumbuki vizuri, kulikuwepo na mgomo kidogo kwa wafanyabiashara wakasema hii itatuletea matatizo. Lakini baada ya kujua kwamba pale kwenye *VAT* ndiyo mahali pa kuibiwa, leo ukisema ufute *VAT* wote watakwenda mahakamani siku hizi hawauzi chochote kile, kazi yao ni kukaa tu na kuandika *returns refund* ya *VAT,* hakuna mtu anayewakagua na sasa ndiyo tumewaongezea wigo mwingine kwamba, wale ndugu zetu Wamachinga, waende pale mlangoni kwa Mhindi, awape bidhaa waingie barabarani wauze bila leseni lakini kitanzi kinakuja.

Hapa tumetengeneza tabaka la watu wa aina gani ambao wanaweza wakapata mitaji? Tulikuwa tunategemea kwamba kumsaidia Mmachinga ni kumpa mtaji wa aina fulani, lakini sasa hapa tumetengeneza tabaka kwa watu wale ambao watakuwa na mtaji wa shilingi milioni 20 ndiyo waweze kupata leseni. Huyu Mmachinga, mimi naona angesaidiwa zaidi kama angeweza kupata leseni kwa sababu sheria zingine ambazo zinaweza kumsaidia huyu Mmachinga akapata mtaji kwa kupitia mkopo ni kuwa na leseni, ndiyo sheria inavyosema ya benki kwamba, kama ukienda kuomba mkopo benki, sharti la kwanza utakaloombwa ni leseni na Mmachinga hayumo, sasa hiki ni kitanzi.

Lakini pia ni kitanzi kwamba, huyu Mmachinga alikuwa anategemea kupata mkopo kutoka kwenye Halmashauri yake kama sheria inavyosema kwamba, kuna asilimia 5 ya pato la Halmashauri kwa ajili ya kuwakopesha wanawake na vijana. Sasa pato la Halmashauri lilikuwa linatokana na hizi leseni. Halmashauri kama ya Temeke, *one third* ya pato lake lote lilikuwa linatokana na leseni. Sasa kama umesema kwamba hakuna kukata leseni, *it means* kwamba, pato lao litashuka na *multiplication* yake inakwenda kwamba kama pato la Halmashauri limeshuka pia ile fedha asilimia 5 ambayo ilikuwa inatakiwa iende kwa ajili ya kuwakopesha wanawake na vijana na yenyewe itapungua. Kwa hiyo, hapa tumewatia kitanzi Halmashauri wasiweze kupata pato la kuweza kuwakopesha hawa watu. Kwa hiyo, habari ya kushangilia kwamba Mmachinga anapunguziwa adha ya kuwa na leseni hapa ni kitanzi chake huyu mtu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amezungumzia sana juu ya kilimo na kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa nchi hii na kwamba wakulima kwa kupitia bajeti hii wamepata unafuu mkubwa sana. Kwanza, wamepunguziwa mbolea haina kodi na kwamba sasa itawafikia hiyo mbolea kwa bei ndogo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 haya maneno yalikuwa kwenye bajeti, nilitegemea kabisa walipotoka hapa wanashangilia watu wa Kusini, Mtwara, Ruvuma, Iringa, *Big Four, Big Three,* kwamba kweli sasa watapata kura zote mwaka 2005 kwa sababu bei ya mbolea imeshuka. Baada ya miezi miwili, mitatu, tuliona kwenye televisheni watu wa Mbeya wakilalamika bei ya mbolea ilipanda maradufu zaidi ya mwaka uliopita. Sasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sijui hili mwaka huu utali-*control* namna gani? Wewe umetangaza kufuta kodi kwenye mbolea, umetangaza kuwaongezea ruzuku kwa ajili ya kusafirisha hiyo mbolea, lakini mbolea hiyo hiyo mpaka Desemba itakuwa mara mbili ya bei ya mwaka 2003! Sasa tunachoomba ni kwamba lazima uje na *formula* ambayo inaweza kusaidia. Kweli mbolea na pembejeo zisiwe zinapanda hata kama kodi imefutwa

Mheshimiwa Spika, niliunganishe hili tatizo namna gani watu ambao wanatakiwa kusaidia kilimo hawasaidii, hii inahitaji kwamba Wizara labda zinge-*coordinate*. Wizara ya Kilimo na Chakula ina matatizo mengi sana hata kama ungeipunguzia mbolea, lakini bado tu watu hawataongeza kilimo na hawataongeza chochote kile. Hata pale ambapo kuna madawa, kwa mfano, madawa ya pamba. KatikaWilaya yangu ya Bariadi kumekuja mtindo sasa wa kuwaambia wakulima watakopeshwa madawa ya pamba na kwamba watalipa shilingi 15/= kwa kilo kwa mkopo.

Mheshimiwa Spika, *infact* ni kuwaumiza zaidi kwa sababu *practically* tumeshaona, tumeenda Wilaya ya Kilosa juzi kama Kamati ya *LAAC,* tumekuta watu wamepelekewa madawa ya pamba ambayo hayaui wadudu wala kufanya kitu chochote. Mpaka tukaanza kuwatafuta watu wa Bodi ya Pamba watuambie kwa nini wao katika shamba lao wametumia dawa ambayo ni nzuri na inaua wadudu, lakini kwa wakulima wa kawaida ambao wamewakopesha dawa ile wadudu hawafi. Baada ya mwezi mmoja kwa kusaidiana na Mheshimiwa Mashishanga, wamepelekewa sasa wanasema mambo yanaenda vizuri. Lakini hii ni tabia hata kule Bariadi watu wanapelekewa madawa ya

pamba ambayo yamechanganywa na maji hayaui wadudu. Sasa tukienda kuwakopesha katika hiyo *style* ambayo unataka kuiweka sisi tunasema hatutaki. Tunaiomba Serikali iendelee na hiyo Bodi yao iendelee na utaratibu wa kuwawekea maduka watu kule kule vijijini wanunue madawa ambayo hayajachanganywa na maji ili waweze kufanya kazi ambayo inatakiwa na wazalishe na waue wadudu na pamba yao iwe safi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii kuna suala la nishati, nilipokuwa naangalia katika bajeti niliona hata juzi Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anazungumzia kwamba, umeme sasa utashuka kwa sababu tuna *Songo Songo Gas.* Mimi naona hapa huu ni mchezo tu wa kubadilishana maneno. Kwa sababu nakumbuka kule nyuma tulipoanzisha Kidatu tuliambiwa kwamba, *the only source of energy* ambayo ni *cheap* ni *hydro-power* tukiachana na *thermal* na njia nyingine. Lakini baada ya mwaka mmoja au baada ya miaka mitano, bado umeme ulikuwa unapanda juu. Tukasema kwamba, labda kwa sababu Kidatu, *the turbines* zimechoka na *consultation* imefanyika kwenye Bwawa la Kidatu tukakimbilia Mtera, tukatengeneza Mtera iweze ku-*supply* maji ya kutosha lakini bado tatizo la umeme likabakia pale pale.

Mheshimiwa Spika, leo tukasema sasa tunaikimbilia *IPTL* na kwenyewe ndiyo huko sasa tumezama, tumeambiwa tunalipa shilingi bilioni 3 na sasa tunaanza kufikiria pia kwamba, hiyo *IPTL,* shilingi bilioni 3 kwa mwezi hazitoshi sasa tutaongeza tena na *Songo Songo Gas* shilingi bilioni 2.5 kwa mwezi na tegemeo ni kwamba, umeme utashuka. Mimi hapo bado naona tatizo liko pale pale, kuna watu ambao wanatuchezea. Nilikuwa nafikiria kwamba, sasa labda vichwa vyetu tungelikaa chini kwanza, tukaanza kufikiria upya, wapi ambako tunakuwa *mis-directed.* Tumekimbilia *Hydro-power* tumeambiwa hiyo ni aghali sana, sasa twende *Songo Songo Gas* na kwenyewe japokuwa wanasema kwamba itashuka lakini nimesoma kwenye *the East African* inazungumzia juu ya *seven cents* na kwamba zile *seven cents* bado ni *the highest* katika *Eastern and Southern Africa,* kwa hiyo, *seven cents per unit* sasa ninachofikiria ni kwamba hapa kuna tatizo.

Baada ya kuhamisha hizi *turbine* tukatengeneza *turbine* za *IPTL,* baadaye kesho kutwa tutaambiwa na zile nazo zimeharibika tunaanza tena kutengenezewa mradi mwingine. Sasa kuna tatizo mahali, mimi nafikiria kwamba, muda sasa umefika kwa Wizara kusimama na kuweka vichwa vyetu sawa na kuanza kujipanga vizuri na kuangalia ni wapi tunapokoseshwa tuanze kupanga mpango mmoja, tuuone kama unaweza kuwa *sustained for fifteen years* bila kuanza kukimbia kimbia mara *Songo Songo Gas*, mara *Hydro-power*, mara kesho kitu kingine na kesho kutwa kitu kingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa na mimi nafasi ili niweze kuchangia hotuba zetu mbili zilizopo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia, naomba niwape pole sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, ambao wamefiwa

na baba yao mzazi. Naomba Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amen.*

Mheshimiwa Spika, naomba basi nichukue nafasi hii, kumpongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga, baada ya kupata ushindi mzuri sana kupitia Chama cha Mapinduzi, hivyo tunamkaribisha tena ili aweze kuwasimamia wananchi wake wa Bariadi Mashariki kwa kupitia sera nzuri sana ya Chama cha Mapinduzi na kuwasimamia maendeleo yao kupitia Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisahau mwishoni kabisa labda inawezekana muda ukaniishia, niunge mkono hoja hii moja kwa moja kwa asilimia mia kwa mia hotuba zote mbili zilizoko mbele yetu kwamba naridhika nazo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Waziri Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kazi nzuri sana, ambayo waliionyesha kwenye bajeti ya mwaka 2003/2004 ya kuhakikisha kwamba wamechukua maelekezo yote ya Waheshimiwa Wabunge katika kusimamia uchumi wa Taifa letu na kusimamia vizuri sana Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2000, pamoja na utekelezaji wote kwa maagizo yaliyotolewa katika bajeti ya miaka iliyopita na hatimaye Wizara ya Fedha ikahitimisha kusimamia vizuri matumizi ya fedha zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba basi nianze kwa kuchangia katika Wizara ya Mipango. Ninapenda sana nichukue fursa hii kuishukuru sana Wizara hii katika mikakati yake ambayo walikuwa wanaileta na sisi wenyewe hapa Bungeni tunaipitisha. Ninaanzia kwenye suala la Urekebishaji na Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Sera ilikuwa ni nzuri sana na kama sisi wasimamizi wa sera hiyo ninasema zoezi hilo lilienda vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini ninaomba tu katika kuzungumzia hapo, nijaribu kumwomba Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda atusaidie sana, maana yake sasa imefikia mahali kiwanda fulani tayari kilishabinafsishwa lakini hakifanyi kazi, tukianza kuuliza ni kwa sababu gani wanaanza kutupiana Wizara fulani husika na Wizara fulani husika.

Mheshimiwa Spika, labda nimwombe basi Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, hebu basi zoezi hili aendelee kulichukua yeye kwa sababu ninavyoliangalia hapo, mikataba yote waliipitia *PSRC* ambao wako chini ya Wizara yake na ni chombo ambacho tunakifahamu kisheria, kwa nini basi asiachie Wizara hizo ambazo zinahusika, kwa mfano, kuna Kiwanda cha *MOPROCO* - Morogoro kimebinafsishwa na kimefungwa, kuna kiwanda cha magunia na vingine vingi vipo pale Mkoani kwetu. Lakini imefika hatua sasa havifanyi kazi, ukienda kwenye Wizara yetu ya Mipango wanakwambia uende Wizara ya Viwanda na Biashara. Lakini sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri, hili zoezi naomba basi uendelee kulisimamia vizuri kwa sababu ilikuwa ni lengo kwamba vifanye kazi na Watanzania wapate ajira. Sasa inakuwaje sasa hivi viwanda havifanyi kazi, kwenye kumalizia ulipaji wa fedha zetu hawalipi na bado tunawaangalia tu?

Basi nikuombe Mheshimiwa Waziri, utusaidie sana ili tuendelee vizuri na zoezi letu kama lengo tulilolweka kwamba, Mashirika haya yote tuhakikishe kwamba yanabinafsishwa na tuhakikishe kwamba yanafanya kazi na yanachukua Watanzania wetu ambao ni tegemeo kubwa sana. Wananchi wa Tanzania waliona kwamba viwanda hivi vitakapofanya kazi watapunguza umaskini, watapata ajira na kusomesha watoto wao.

Mheshimiwa Spika, hili nalizungumzia sana kwa sababu utaratibu wote wa kubinafsisha mashirika unapitiwa na Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, basi ni pendekezo langu tu kwamba, Mashirika haya ambayo ameyaorodhesha Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu chake hiki *NMB, THA, TANESCO, TRC, TAZARA, NIC* na Viwanda vya Korosho, vitakapofikia zoezi hilo, basi tumwombe Mheshimiwa Waziri, makosa yote ambayo yalitendwa nyuma kwa Mashirika ambayo tulishayabinafisha, yasitendeke tena, tuweke lengo letu ambalo ni usimamizi mzuri na *PSRC* ni chombo ambacho tumekikabidhi kifanye kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie tena suala la kilimo. Mwaka 2003 katika mipango yetu tulisema kwamba, kilimo ndiyo uti wa mgongo, lakini sasa katika utekelezaji hata kwenye *speech* ya mwaka huu, sioni kwamba, kweli kilimo tumekiweka kama ndiyo uti wa mgongo.

Mheshimiwa Spika, mimi nasikitika sana nikisema kwamba, Tanzania itakuwa ni ajabu sana kusema kwamba tunatakiwa tuwe na njaa. Kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri, amesema kwamba tuna ekari milioni 2.3 ya mabonde, ni nini basi kinachokwamisha? Kwa nini haya mabonde basi tusiyaanzishe ili tuhakikishe basi tunaanzia kwenye mabonde ambayo yapo tayari kwa kufanya hii shughuli ya kilimo cha umwagiliaji. Nitamwomba basi Mheshimiwa Waziri, atueleze mabonde haya yataanzishwa vipi, pamoja na kwamba kuna Wizara ya Kilimo na Chakula lakini mipango inatoka kwenye Wizara yake? Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Waziri atusaidie sana kwa sababu mabonde haya yako kwenye Wilaya. Sasa tuwaombe Maafisa Mipango wa kwenye Mikoa na Wilaya husika basi wakuletee taarifa ya uhakika kwa sababu wao ndiyo wanaelewa mabonde hayo yalipo na yanatakiwa yafanyiwe nini?

Mheshimiwa Spika, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie sana kwa sababu sasa Maafisa Mipango walioko Mikoani, mara nyingi wanaandika tu taarifa wakiwa mezani. Hebu basi tuwaombe waende *site* ili wawe wanaandika taarifa ambazo kweli zinaonyesha maeneo haya yako hivyo na yanatakiwa yaendelezwe kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwamba, Tanzania hatutakiwi kuwa na njaa, kwa sababu tuna maziwa matatu ambayo ni makubwa, inakuwaje basi Tanzania tumezungukwa na maeneo ya aina hiyo tuna Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, yote yametuzunguka Tanzania, inakuwaje sasa tunaanza kulalamika kwamba, Tanzania tuna njaa, hebu naomba tuyatumie basi maji haya ambayo Mwenyezi Mungu, ametukabidhi tuyafanyie kazi ili yasipotee bure. Kwa kumwomba tu Mheshimiwa Waziri kwenye, suala la Maafisa Mipango ni hivyo tu wafanye kazi ili wahakikishe basi takwimu wanazompelekea kwenye Wizara yake ziwe ni sahihi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri amesema mwaka 2004/2005, Sekta ya Madini itaendelea na utekelezaji wa mabadiliko ya kiuchumi ambayo yatatoa kipaumbele, inalenga katika kufanikisha mambo yafuatayo: Sawa nakubaliana nayo kwamba kweli yataendelea. Nitazungumzia haya maeneo ya madini kupunguza umaskini. Anaposema kwamba sekta hii wataisimamia katika kutekeleza hayo mabadiliko ya kiuchumi, sasa sijui Mheshimiwa Waziri atanisaidiaje, nikiangalia wananchi wanaoishi katika maeneo hayo ni watu wenye maisha duni sana. Ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge wa Wilaya ya Geita, jana alilizungumzia. Baada ya kuyakata maeneo ya dhahabu na almasi sasa labda Mheshimiwa Waziri atayaangalia tena upya ili hata maeneo hayo basi yaangaliwe wanasaidiwaje na wenyewe ili waonekane kwamba na wenyewe Mwenyezi Mungu aliwaweka katika eneo ambalo limezungukwa na almasi na dhahabu ambazo kweli na wao wamezaliwa wamezikuta, basi nitamwomba sana Mheshimiwa Waziri atusaidie sana ili na hao watu tuwaone kwamba na wao wako katika nchi ya Tanzania na wanafaidika na maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, lakini ninaomba tu labda hilo atalipeleka kwenye Wizara ya Nishati na Madini. Nikiangalia sana uchimbaji wa *Kahama Mining* sijui atanieleza kwamba kuna usalama gani wa wananchi walioko huku juu, uchimbaji wao ni wa kwenda ndani, wanachimba kwenda ndani kuelekea kwa wananchi wanakoishi, sasa sijui watakuwa wamejiwekea ulinzi gani wa kuhakikisha kwamba wananchi wa maeneo hayo hawataathirika? Siombei tetemeko linaweza likatokea ni bahati mbaya Mwenyezi Mungu ataamua tu tetemeko lipitie katika maeneo hayo, itakuwaje wananchi wetu wa eneo hilo kwamba hawatafukiwa na hayo mashimo, maana yake kule chini kuna barabara, yaani barabara ziko chini ya nyumba za watu wanakoelekea kupasua. Sasa nitamwomba tu Mheshimiwa Waziri, anisaidie kunieleza watasaidiwa vipi?

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichukue nafasi hii tena kuipongeza sana sana Wizara ya Ujenzi, kwa sababu baada ya kuamua Waziri atumie fedha za nchi yetu za ndani katika kutengeneza barabara, hali ya sekta ya barabara inaonekana kwa kweli itakuwa ni ukombozi mkubwa sana kwa wananchi waendao eneo la Kanda ya Ziwa, kama barabara ya Dodoma hadi Mwanza itakapokamilika, kwa kweli wananchi wa maeneo hayo wataweza kufaidika na gharama za usafiri katika maeneo hayo zitapungua na watafanya biashara ya samaki kutoka Mwanza kupeleka Dar es Salaam watakwenda kwa urahisi zaidi.

Hivyo naipongeza sana Wizara hiyo kuhakikisha kwamba basi barabara hiyo inaisha kwa wakati ambao mmekubaliana na Makandarasi niwapongeze sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la elimu. Naipongeza sana Serikali baada ya kuboresha elimu ya Shule za Msingi. Sasa hivi tuko kwenye mkakati wa kuboresha shule za Elimu za Sekondari. Lakini nitamwomba sana Mheshimiwa Waziri katika Bajeti yake ya mwaka 2004/2005 ihakikishe basi inakwenda sambamba na ufundishaji wa Walimu. Kwa mfano Mkoa wa Mwanza kuna Azimio la Mkoa limesema kwamba kila Kata tuwe na Sekondari. Lakini kama tutakapokuwa na Kata 174 na Sekondari 174 tutakosa Walimu itakuwa haina maana yoyote. Nimwombe sana katika

mipango yao hii katika Bajeti ya mwaka huu iende sambamba na ufundishaji wa Walimu. Hivyo ninaomba sana zoezi litakapokuwepo na nina hakika kwamba Mkoa wa Mwanza kuanzia mwaka Januari 2005 shule zote zile zitafunguliwa. Sasa kama hatutakuwa na Walimu tutakuwa tunawavunja moyo wananchi kwa sababu wameshaambiwa kwamba wanaanza kujenga kwa nguvu zao wenyewe sasa watakapokamilisha tukose Walimu itakuwa sisi Waheshimiwa Wabunge tunavyowahamasisha wananchi wachangie elimu watakuwa wamevunjika moyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala la UKIMWI. Naipongeza sana Serikali yetu katika mipango kwenye hotuba ya Waziri wa Mipango anasema kwamba zile dawa zitatolewa bure. Nilikuwa naomba atusaidie sana hizi dawa zitagawiwaje. Je ni kwamba hata Vijijini hizi dawa zinafika kwa walengwa ili wahakikishe na wenyewe kweli zile dawa zimewafikia. Maana yake sasa hivi tunaulizwa maswali dawa ziko wapi. Basi kwa sababu hotuba imeeleza wazi nitamwomba tu na atuhakikishie kwamba lini zitaanza kufikishwa kwenye maeneo kwa wananchi wetu waweze kusaidiwa basi wapate hizo dawa hatimaye waweze kushiriki katika maendeleo wakiwa na matumaini.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sasa nizungumzie suala moja la mwisho sana suala la kuondoa umaskini kupitia *TANESCO.* Tumesema kwamba Sera ya Nishati inawahakikishia kwamba Vijiji vyote vimepata umeme. Lakini kinachosikitisha naomba nisaidiwe tu imefikia sasa gharama za *TANESCO* kwa kweli zinazidi kuwa kubwa. Mimi sikatai tunavyoelekea ndiyo zinaongezeka. Lakini tuangalie Serikali yetu tena bado inatenga ruzuku kupeleka kwenye Shirika la *TANESCO.* Ukifikiria kwamba gharama tu ya kuvuta ule umeme, gharama ya nguzo, nguzo moja ni Sh. 305,278/= kama sikosei baadaye Waziri atalifuatilia hili na *service line Shs. 198,000/=.* Kwa wananchi wa Kijijini na sisi tunasema kwamba wanahitaji umeme ili waweze kuwa wanaangalia *TV* kwenye maeneo yao uwezo wa mwananchi wa kawaida kwa kiasi hiki nitaomba basi kwa sababu Serikali imeshajiingiza katika kutoa ruzuku kwenye Shirika hili basi lenyewe lijiangalie katika kuhakikisha linakusanya gharama za watu wanavyotumia umeme ili basi wapunguze fedha nyingine ambazo Serikali inachangia kule ili ziende kwenye maendeleo mengine. Lakini sasa tunapofikia kwamba kuna wakati namkumbusha Mheshimiwa Spika ilitokea uzembe wa Shirika hili watu wakawa wanatumia umeme bila kudai madeni, halafu tukaleta *Net Group* ambayo nilikuwa nafikiri sasa katika Shirika la Kujitegemea litakusanya fedha nyingi na litapunguza gharama kwa Serikali yetu kuchangia tena ruzuku. Lakini sasa bado ninaona *Net Group* bado ipo na gharama ya umeme inapanda tutamsaidiaje huyu Mtanzania; afadhali basi hiyo ruzuku ya Serikali ambayo inatolewa kule ipelekwe kwenye maendeleo mengine wao wasimamie gharama za bili ambazo zinatumika kwa kila mtu anajua wajibu wake kwamba anatumia kila siku. Lakini inasikitisha hata nguzo zinatoka Afrika ya Kusini. Inasikitisha kwa sababu tuna miti mingi tumepanda ni nini kinachotokea mpaka hata nguzo zitoke Afrika ya Kusini. Naomba katika hili waliangalie hapa *TANESCO* kuna nini? *(Makofi)*

Kwa kumalizia naomba basi migogoro hii inayotokea kwenye Mashirika yetu tunayobinafsisha hebu Serikali yetu tuangalie. Sasa hivi *TRC* kuna mgomo mkubwa sana na sisi tunajiandaa katika kulibinafsisha hili Shirika. Naomba sana kwa kupitia Bunge

hili tuangalie kwa sababu ni vyombo vinavyobeba abiria, kama treni inabeba watu wengi sana. Mnakumbuka kwamba mwaka juzi ilivyoanguka hapa karibu na Dodoma watu walitaka kusema kwamba ni mgomo wa wafanyakazi, lakini sasa tusiingize kwamba mgomo wa wafanyakazi mlichunguze hili Shirika kuna nini. Juzi tu hapa Dar es Salaam imetokea kwamba nao wamegoma na *engine* imefichwa kwenye gereji huko. Ni nini hiki?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia hotuba zote. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hotuba hizi mbili tulizonazo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na mpendwa baba yao mzazi. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *(Amin)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pole hiyo naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Waheshimwa Mawaziri, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Manaibu wote wawili wa Wizara ya Fedha na Makatibu Wakuu wa Wizara hizi zote mbili na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hizi zote mbili Mipango na Matumizi yake ya Wizara ya Fedha hazina mjadala sina budi kuziunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Bajeti hii imegusa pande zote za wenye uwezo na maskini. Lakini kwa asilimia kubwa pamoja na kwamba inajitahidi au zinajitahidi kuondoa au kurekebisha umaskini lakini kuna tatizo kubwa sana tulilokuwa nalo hapa nchini. Serikali imejiondoa katika sehemu nyingi. Imejiondoa kwenye masuala ya biashara na imejiondoakatika usimamizi wa bidhaa au shughuli zote za uzalishaji hapa nchini. Sasa sielewi kama ni masharti ya hawa wenzetu ambao wanachangia asilimia nusu au robo ya Bajeti yetu. Lakini nina imani kwamba Bajeti yetu inajitosheleza. Kama inajitosheleza kuna mambo muhimu ambayo Serikali ichukulie kama ni kero kwa wananchi hususan upandaji holela wa bidhaa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali katika mipango yake imezungumzia kwamba italinda viwanda vya ndani, itamlinda mlaji, lakini cha kushangaza hali ya sasa hivi kwa wananchi wetu upandaji wa bei ya sukari Serikali inasemaje kwa hilo. Kwa sababu sasa hivi sukari hapa mjini, nikizungumzia mjini tu kwenye maeneo hayo sukari kwa kilo moja shilingi 800/=. Je, Vijijini umbali wa kutoka mjini wanapata kwa shilingi ngapi? Sasa hivi Vijijini sukari kilo moja ni shilingi 1,200/= mpaka 1,500/= hivi Serikali hailioni hili. Juzi tulikuwa na mijadala mingi tu ya kuhusu upandaji wa mafuta. Mafuta yamepanda sana. Watu wamekaa wametafakari Waziri wa Fedha ambaye ndiye tunamtegemea sana ndio kiungo alidiriki kukemea upandaji wa bei za nauli. Alikemea sana. Hivi Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa mapenzi yako na wananchi wako na kuilinda Sera ya Chama cha Mapinduzi hili unaliwekaje. Suala la sukari unaliwekaje kwa wananchi wako. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba hili lisiweze kufuta matatizo yaliyopo. Bajeti inasema uchumi umekuwa. Bajeti inasema inaondoa umaskini, Bajeti hiyo hiyo inasema ina matarajio lakini kwa hili mimi ningeomba Waziri upandaji wa bei turudi kule kule kuwe na *controlled price.* Kwa sababu kama tukiliacha hivi hivi tu bila Serikali kuingilia na hawa wawekezaji wapo watapandisha kila kitu, mbona dhahabu hatuwapandishii kodi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri kwa hili nimeliongelea kwa uchungu sana kwa sababu waathirika wakubwa ni watoto, wazee hata wanaume pia kwa sababu atamwuliza mama chai iko wapi. Kwa hiyo hili suala linagusa jinsia zote. Kwa hiyo nilikuwa naomba wakati wa kufikiria kama ulivyosema kwamba tutoe mawazo yetu suala la sukari nadhani litachangia kiasi kikubwa kuendelea hadhi ya kuhodhi Sera za Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nizungumzia hali halisi ya Walimu. Wenzangu wamezungumzia kwa kina kwa ndani lakini pia na mimi ingawaje si vizuri kurudia rudia lakini nitarudia kwa njia nyingine. Walimu wanahitaji kujengewa mazingira mazuri kwa sababu hawapati muda wowote wa kuwa nje ya maeneo yao ya kazi kutafuta miradi. Sasa kwa kuwa wanakuwa hawapo nje hawatakuwa na uwezo wa kujitosheleza angalau kujenga hata kibanda cha chumba na sebule. Kwa hiyo nilikuwa naomba tuangalie uwezekano wa kuwasaidia hawa Walimu ujenzi wa nyumba za bei nafuu. Lakini katika hilo tuwasaidia pia kupata mikopo midogo midogo kwa mfano kama tutaweza kupitia upande wa Viwanda na Biashara *SIDO* mimi bado kila ninapochangia kila mwaka lazima niilee *SIDO*. Kwa sababu *SIDO* sasa hivi ina mikakati mizuri sana ambayo uwezo wao ni mdogo kifedha, hauridhishi. Kwa hiyo nitamwomba Waziri kama hatutaweza kuwasaidia hawa Walimu kwani *SIDO* huwa wana utaratibu hata wa kukopesha cherehani, *TV* na kadhalika. Kwa hiyo hivyo navyo vitawasaidia Walimu ambao hawana uwezo wa kuweza kujitosheleza kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, pia nizungumzie kwamba hawa wenzetu Walimu kama wanaweza kupata mkopo Wakuu wa Shule za Sekondari au za Msingi kwa ajili ya pikipiki itakuwa pia ni faraja kubwa kwao angalau wakaweza kuona nini cha kufanya kwa sababu uwezo wa kupata magari hawana. Wanaishi katika mazingira magumu na wanaishi Vijijini. Kwa hiyo nilikuwa naomba haya yote katika mtiririko huo Mheshimiwa Waziri atusaidie kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia kilimo kwa sababu kila anayesimama hapa anazungumzia kilimo. Kilimo tulishakubaliana kwamba ni uti wa mgongo na kelele au maelezo wanayotoa Wabunge ni vyema Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu amekiri atakubali mawazo ya wananchi au ya Wabunge kwa suala zima la kilimo ni vyema Waziri akaliangalia suala la kilimo kwa wakulima wadogo wadogo. Mimi Tanzania sijamwona mkulima mkubwa. Kama ni mkulima mkubwa basi ujue amekopa mikopo mikubwa nje kwa kupitia Tanzania hii hii. Lakini kwa mkulima mdogo yoyote hata kama akilima eka moja kwa Mtanzania bado ni mkulima mdogo.

Waziri wa Fedha mwaka jana alisema kwamba ataanzisha Benki. Lakini katika taarifa yake pia amesisitiza kwamba kuna uwezekano wa kuanzisha hizi Benki ambazo itawakopesha wakulima wadogo wadogo. Sasa kama ndivyo hivyo ukiangalia bajeti

nzima Mheshimiwa Waziri wa fedha hajazungumzia kabisa suala la kumkomboa mwanamke. Nimejaribu kusoma usiku na mchana, naamka usiku nasoma lakini sijaiona hiyo. Sehemu sasa kama sijaiona ina maana kusema bado Mheshimiwa Waziri wa Fedha suala zima la mkopo wa Wanawake bado wewe ni kiungo cha kutusaidia kukamilika. Sasa hivi masharti hayo mnayotueleza kwamba akinamama waende wakakope kwenye Benki hizo kuna masharti yao. Kuna masharti yao ambayo Wanawake hawawezi. Vikundi vinavyanzishwa na akinamama lakini mitaji ni midogo kiasi ambacho shilingi 50,000 hazitoshi kuanzisha biashara.

Kuna *PRIDE*. *PRIDE* kweli inasifika imefanya kazi nzuri lakini masharti yake ni kwamba lazima muwe watu watano. Watu watano ambao hamuelewani ila muwe watano. Inapotokea mmoja hayupo hajalipa Mheshimiwa Waziri ina maana wale wanne wanamlipia yule mmoja. Wote waliokopa mimi sijaona kama wamebadilika, hali yao ni duni tu. Bado hawa watu wanaifanyia *PRIDE.* Sasa kama tutakuwa na chombo chetu cha Serikali kwa uchungu wake nina imani kwamba Wanawake na Vijana watajikomboa. Ukimuelimisha mwanamke unamwelimisha mwanaume na jamii nzima. Nilikuwa naomba Waziri aliwekee msisitizo na umuhimu kwa kuipa kipaumbele Benki hii ili iweze kushirikisha watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la ushirika, Vyama vya Ushirika. Hivi juzi tu nimesikia kwenye redio kwamba Mkuu wa Mkoa wa Tabora amekemea Viongozi wote Igembensau ambao wamekula fedha za Ushirika. Wakati huo mnatushauri kwamba tuanzishe Benki za Ushirika, tujiunge na ushirika usalama wake na imani kwa wananchi tunaiwekaje ili hawa wananchi wawe na imani kubwa na Ushirika huu kama ni juzi tu tumeanza kupiga kelele sana kuanzisha ushirika na sasa tena wameanza wizi huo, Serikali inasemaje kwa hili. Ina mikakati gani kwa hili ili wananchi waelewe kwamba hawawezi kuibiwa fedha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo yote pamoja na kwamba nimemaliza lakini niombe pia Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji iendelee kuangalia kwa kina kwa Mtanzania kumlinda kuhusu suala zima la ulaji. Wamezungumzia upandaji wa bei ya soda. Mheshimiwa Waziri ebu iondoe hiyo soda. Soda watoto tunawapa na wao wanajua uchumi unakwendaje, wanafaidi kwenye matunda kwa soda. Soda shilingi 250/= ukishaweka 400/= wananchi kipato chao na mshahara wao wa mwisho wa mwezi kama Mtanzania atafanya nini, hawezi kunywa soda mtoto wa mkulima. Sasa hivi watu wote walianza kuonekana kwenye masuala ya ulevi wanakwenda kushiriki na watoto wao katika familia zao ili waweze kunywa angalau soda. Sasa kama Serikali imepandisha hata juisi tunafanyaje kwa hiyo nyumba zitaanza kuyumba tena baadhi wataanza kwenda kunywea huko huko. Kwa hiyo, nilikuwa naomba niunge mkono asilimia mia kwa mia hoja zote mbili na niwapongeze. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kama ilivyo kwa wenzangu na mimi naomba nitoe pole sana kwa hawa Waheshimiwa wenzetu wawili waliopotewa na baba yao mzazi. Ninawapa pole. Lakini pia tumpe pole pia Mheshimiwa Rais na tumwombee Mungu amjalie afya njema arudi tena nchini tushirikiane naye katika haya masuala ya maendeleo. Vile vile niwape

pole Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamepata matatizo mbalimbali. Wengi wetu wamepata ajali na wengine pia bado wako mahospitalini wakijiuguza, lakini kuna wengine ambao Mungu amewasaidia tuko nao hapa Bungeni. Kwa hiyo, tunawapa pole wote. Tunawapa pole Watanzania wengine wote waliofikwa na maafa mbalimbali yaliyowakuta hivi karibuni.

Mheshimiwa Slpika, kwa hali ya pekee naomba nimpongeze sana Ndugu yetu Danhi Makanga, Mbunge aliyeingia hivi karibuni hapa Bungeni. Tumeshangaa kidogo Ndugu yetu Cheyo wa *UDP* aliposimama kuchangia hoja hii alijisikia taabu sana kumsifia Makanga, lakini kwa niaba yake na mimi binafsi na Watanzania wote tunampongeza sana ndugu yetu Makanga kwa kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niipongeze Serikali ya Tanzania na niwapongeze watendaji wote wa Serikali ya Tanzania. Hasa naomba nimpongeze Waziri wa Fedha na Mipango na Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa kutuletea Bajeti hii ambayo imekuwa na mwelekeo mwingine mpya na mwelekeo tofauti sana wa kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, bajeti yetu ya mwaka huu inaleta picha halisi ya nini maana ya Chama cha Mapinduzi kuendelea kushika hatamu ya uongozi katika nchi ya Tanzania. Ule mfano alioutoa Mheshimiwa Rais wakati akilihutubia Bunge na kuwafananisha wale wote wanaona haya yanayofanywa na Serikali ya Tanzania kama si kitu ni sawa na wale walevi watatu waliotembea usiku halafu hawaelewi kwamba ni usiku kama ni mwezi ama ni jua. Kwa hiyo naomba niseme kwamba yule ambaye anaona bajeti hii si kitu mwaka huu kwa kweli bado nadhani anaendelea kusumbuliwa na tatizo la ulevi kama wale walevi watatu aliowatolea mfano na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii kwa kweli ni ya namna yake kabisa. Mimi naanza kwa kuiunga mkono asilimia mia kwa mia na ninaamini itafanyiwa utekelezaji wa hali ya juu. Kwa kipindi kirefu sana mambo mengi yamejitokeza wazi yametuonyesha mafanikio makubwa ya utekelezaji wa mipango ya Serikali hii. Barabara nyingi zinaonekana, mashule yamejengwa. Tumesema hapa maji safi na salama yamefikishwa mpaka maeneo ya Vijijini, tumeona kabisa jinsi gani Serikali yetu inavyoboresha suala zima la afya. Kwa kweli tulikotoka na tulipo ni tofauti na ninaamini tunakokwenda tutakuwa bora zaidi kama tutaendelea kushirikiana kama tulivyoshirikiana toka mwanzo. Ninaomba hili kuyafanya mambo yote yaweze kwenda vizuri nichukue nafasi ya pekee kushauri mambo mawili matatu yatakayotusaidia kuifanya bajeti hii iwe bora zaidi na iweze kutekeleza kiyakinifu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii inasisitiza uwezeshaji raslimali watu. Katika kila Wizara na Mheshimiwa Waziri wa Mipango mimi nilikuwa napitia sana huu mpango wake wa maendeleo wa mwaka 2004/2005. Kila Wizara imeweka kipaumbele katika suala zima la uwezeshaji la raslimali watu. Mimi naunga mkono kabisa wazo hili ambalo ni la kimsingi. Tunapozungumza suala zima la maendeleo tunazungumza kwamba ni lazima mtaji mkubwa utokane na watu wenyewe kwanza halafu uingize mtaji wa kuwawezesha tukijumlisha na ardhi, siasa safi na uongozi bora basi tunaweza tukafanikiwa. Sina shaka suala zima la uongozi bora na siasa safi katika nchi yetu ya

Tanzania lipo, hatuna tatizo nalo. Lakini raslimali watu ni suala zima la msingi la kuangaliwa na namna gani tunalishughulikia.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri tuhame katika suala la ubinafsishaji kama tulivyolianza limeweza kutusaidia kufika mahali ambapo panaleta mwelekeo. Suala la uwekezaji limeweza kuleta nguvu ya ziada katika masuala ya maendeleo.

Lakini tuingie sasa kwenye suala zima la uwezeshaji jamii na hasa jamii ya watu maskini. Suala la uwezeshaji ndilo litakaloipa picha bajeti hii kwamba ni bajeti ya watu na hasa ni bajeti ya maskini.

Tunapoingia kwenye uwezeshaji ndio hapo tunaweza kujipanga vizuri tuwawezeshe wananchi wa Tanzania katika nini na hasa wale ambao ni maskini waishio Vijijini waweze kumudu hali ya maisha katika Vijiji vyao na kule katika maeneo ya Vijiji tunaamini kabisa ndipo kwenye uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa la Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilimo kiongoze katika suala la uwezeshaji na sekta nyingine zifuatie. Lakini mimi nilikuwa nasoma historia ya Wamerikani. Wamerikani wenzetu wanasema kwamba miaka 3000 kabla ya kuzaliwa Kristo suala la umwagiliaji maji mashambani lilikuwa limeshaanza kujitokeza ingawa katika hatua za kienyeji.

Kwa hiyo, hiyo inaonyesha ni namna gani kabisa suala zima la umwagiliaji maji lina umaana na wa kiasi kikubwa katika maendeleo ya mahali popote pale. Lakini tunasema kwamba ili kilimo kiweze kuwa bora tukiwa na kilimo cha umwagiliaji tutawasaidia wananchi kuwa wazalishaji kwa mwaka mzima na hivyo kupambana na umaskini.

Lakini umwagiliaji peke yake hautoshi na lazima tuongeze suala zima la upatikanaji wa pembejeo na mbegu na vitu vingine ambavyo ni muhimu. Lakini teknolojia ipi ambayo ni muafaka katika kusaidia haya yanawezekanika ili kukikomboa kilimo cha mkulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nafuatilia Bajeti zetu. Kama kweli Wizara inataka kusema kwamba kilimo ni sekta kiongozi, kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa. Katika mpango wa maendeleo wa nchi yetu ya Tanzania wa mwaka 2002/2003 suala la umwagiliaji lilipewa na wafadhili na serikali jumla ya shilingi 11,526,075,400. Lakini nilipokuwa napitia mpango wa maendeleo wa mwaka 2004/2005 ukurasa wa 59 uendelezaji wa suala zima la umwagiliaji na huduma za kiufundi umepewa jumla ya shilingi 4,121,733,200.

Lakini hapo hapo katika mpango wa maendeleo wa mwaka huu suala la sera na mipango imepewa jumla ya shilingi 10,262,998.8. Ni kwa kiasi gani tuko makini kwenye suala hili la kujikomboa katika suala zima la kilimo na ongezeko la chakula katika nchi yetu. Kama mwaka 2003 wakati huo hatukuwa tumejipanga vizuri bilioni 11

zilitengwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji hiki kitabu cha maendeleo ninacho. Lakini leo mwaka 2004/2005 tunaweka bilioni 4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba kabisa ebu kabla hatujahitimisha bajeti hii tuangalie upya kama kweli tumeamua kuondokana na tatizo la njaa kuwasaidia wakulima wetu na kuhakikisha kwamba maendeleo ya uchumi wa Tanzania yatapiga kasi. Wakati tunachangia katika semina ya umaskini juzi nimesema tunazungumzia masuala ya trekta iko mikoa ukihesabu jumla ya matrekta katika mikoa ile inawezekana isizidi matrekta 10 ama hata 10 yanaweza kuwa hayafiki.

Bado wananchi wanaendelea kulima kwa jembe la mkono. Kama kweli tuna hakika kwamba uchumi wa Taifa unaongozwa na kilimo mimi naomba Wizara ya Kilimo safari hii ituambie ni matrekta mangapi yatasambazwa mikoani ni majembe mangapi ya kukokotwa na ng'ombe yatapelekwa kwa wakulima na ni mkakati gani umewekwa wa kuhakikisha kwamba jembe la mkono linaacha kutumika katika nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninashauri utaratibu uliotumika katika Wizara ya Elimu ya kuboresha Shule za Msingi katika Vijiji vyote utumike katika kukomesha jembe la mkono na kuingiza kilimo bora na cha kisasa. Tukiboresha hayo masuala ya masoko yatajileta yenyewe. Yatajileta kwa sababu uzalishaji wetu utakuwa ni bora kwa kuwa tumefuata kanuni bora za kilimo cha kisasa bidhaa zetu zitakuwa bora na masuala yote yatakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunazungumzia suala la viwanda. Kila siku tunasema suala la viwanda. Maendeleo ya nchi za Ulaya yalitokana na uboreshaji wa viwanda.

Ni kweli kwamba tumeweza kubinafsisha, tumewekeza katika viwanda huko mijini, lakini tunawasaidiaje wakulima wadogo wadogo kusindika mazao yao kwa kuwatengenezea viwanda vidogo vidogo huko vijijini?

Mheshimiwa Spika, ninaomba kabisa Wizara ya Viwanda na Biashara itupatie mkakati maalum wa kuhakikisha uanzishaji wa viwanda vidogo vidogo katika maeneo ya vijijini ili kuboresha hali za Watanzania. Lipo suala la kuendelea kupanda bei na kushuka kwa bidhaa maalum ambazo zingeweza kuchangia katika Sekta ya Kupambana na Umaskini kama ilivyo katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ardhi inasema inajenga nyumba za bei nafuu, nyumba zote hizo zinaishia mijini, vijijini ndiko kwenye nyumba mbovu kuliko nyumba zote katika nchi ya Tanzania. Tunafanya nini kuboresha maisha ya wanavijiji wa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, bei ya cement na bei ya bati katika maeneo ya vijijini ni kubwa kuliko kule mjini kunakojengwa nyumba za bei nafuu. Hebu tuone sasa tunafanya nini, hebu tujipeleke huko vijijini tuboreshe maisha ya Watanzania na waweze kuona kabisa mipango hii ya maendeleo inawagusa wao moja kwa moja. Kwa nini Mheshimiwa Waziri wa Fedha hazungumzi suala la kushuka kwa bei ya cement na bei ya

bati ili wakulima wetu na Wananchi wa vijijini wakaweza kuboresha maisha yao? Wataendelea kuishi katika makazi duni ya kimaskini mpaka lini? Bajeti hii ni ya Wananchi, kweli iwekewe mkakati wa kuwagusa Wananchi na kuwasaidia kujikomboa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Ushirika na Masoko inafanya kazi nzuri sana, lakini yale ambayo yanatakiwa yashughulikiwe kuwasaidia Wananchi kuboresha ushirika na kuutumia ushirika kama nguzo pekee ya kuwaletea wanyonge maendeleo yazingatiwe. Tungeboresha ushirika hata suala la mbolea kuwafikia wakulima lingeweza kupitia kwenye ushirika na Wananchi wetu wangenufaika vizuri sana, lakini yapo mapungufu ya namna moja ama nyingine. Ushirika unapoanzishwa waangalie hao wanaushirika kupewa mitaji na kuongezewe nguvu za kuwa na ushirika ulio imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naungana na wenzangu kutetea hoja ya walimu kupewa malimbikizo ya mishahara na posho zao. Ninaipongeza Serikali kwa kuwarejesha wastaafu katika malipo yao ya pensheni tena, lakini naomba iangalie suala zima la kupanda kwa bei ya mafuta ambako kutasababisha matatizo makubwa sana kwa Wananchi katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana niendelee kusisitiza uwajibikaji na umaskini wa Watanzania katika kubeba majukumu ya kuwatumikia Watanzania wenzao. Kama kweli Wananchi wote wa Tanzania na hasa wenye madaraka na wale wanaobeba majukumu ya kuwasaidia Watanzania kwenda katika harakati za maendeleo wangekuwa makini, wangekuwa na uzalendo nadhani tungeweza kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, Kamati mbalimbali za Bunge zimegundua mapungufu makubwa katika utendaji kazi kwenye Serikali yetu. Ili bajeti hii iwafikie Wananchi ni wakati wetu muafaka wa kupambana na watendaji wabovu wote na kuhakikisha kwamba tunawadhibiti na kuwaadhibu kulingana na vile ambavyo wamelisababishia Taifa hili upungufu katika Sekta zao za maendeleo kwa kipindi kirefu. Suala la kuhamisha watendaji wabovu kutoka eneo moja kwenda lingine likome. Suala la kuhamisha watendaji wabovu liishe, liwe ni suala la kuangalia nani anafaa na nani aendelee kulitumikia Taifa la Tanzania. Wananchi wa Tanzania wako tayari kupigania maendeleo, wanasubiri kuongozwa na wala hawana matatizo katika hili, lakini wamekosa watendaji ambao wanaweza wakawa ni kioo safi na kioo bora katika kuwapeleka kwenye maendeleo yakinifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa niipongeze Wizara ya Afya kwa harakati zake za kupambana na tatizo la UKIMWI. Lakini ninaomba sana Tume ya Kudhibiti UKIMWI iendelee kuhakikisha mipango hiyo inafanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN A. SADIQ:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Nami naomba niungane na wenzangu kwa kumpa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na ndugu yake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa msiba wa baba yao. Pia, niwape pole Waheshimiwa wengine wote waliopata matatizo katika kipindi hiki cha Bunge la Bajeti pamoja na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri Mramba na Waziri Dr. Kigoda kwa Bajeti zao nzuri na mipango mizuri ya uchumi waliyotuletea katika Bunge letu hili Tukufu. Pia, nampongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga kwa ushindi wake mkubwa aliopata na kurudi tena Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania kama Taifa tumepata heshima kubwa ndani na nje ya nchi kutokana na umahiri wa viongozi wetu waliotuongoza. Tulianza na Mheshimiwa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere, leo tunaye Rais wetu Benjamin William Mkapa, Rais ambaye anakubalika ndani na nje ya Taifa letu kwa kazi nzuri anayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais Mkapa ni kiongozi shujaa, sasa hivi anafanya kazi pamoja na kuumwa kwake, lakini sisi kama Taifa hivi ni kweli tunajua uwezo wa Rais wetu? Mataifa ya nje na kimataifa wameshatambua uwezo wa Rais Mkapa na sasa wanaanza kumtumia. Sisi kama Watanzania, Rais Mkapa ni Mtanzania, Rais Mkapa ni kiongozi wetu, hivi tunajua nini uwezo wa Rais wetu? Ni lazima Watanzania tujiulize na tumsaidie Mheshimiwa Mkapa kwa faida ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo letu kubwa ni katika masuala ya utekelezaji na usimamizi. Tunapanga mipango mizuri, tunapanga mambo mengi, lakini tukifika kwenye utekelezaji tunapata kigugumizi. Ukiangalia Bajeti iliyosomwa na Mheshimiwa Waziri Mramba mwaka jana na Bajeti iliyosomwa mwaka huu kuna mambo yamechukua mwaka mzima katika utekelezaji. Leo kila Mbunge anasimama anazungumzia mafuta. Mwaka jana tulipitisha kwenye Bajeti tuweke *flow meter* katika bandari ya Dar es Salaam, leo zimechukua mwaka mzima tunaambiwa zitafungwa mwezi wa saba. Utekelezaji tu unachukua mwaka mmoja! Wakati umefika sasa tubadilike.

Mheshimiwa Spika, leo tujiulize suala la mafuta linazungumzwa kwa uchungu, lakini limeanzia wapi? Tatizo hili limesababishwa na nani na chanzo chake ni nini? Mheshimiwa Mramba atakumbuka miaka ya 1997, 1994 na kurudi huko nyuma tulikuwa na *TIPPER,* katika kipindi cha *TIPPER* tulikuwa tunafanya vizuri mno, leo hatuna *TIPPER,* lakini baraka hizi za kutokuwa na *TIPPER* zimetolewa na nani? Zimetolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali ndiyo imetufikisha hapa tulipo. Kila anayesimama anazungumzia mafuta. Nani katufikisha hapa tulipo na ni utaratibu gani uliotumika kutufikisha hapa tulipo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumuombe Mwenyezi Mungu atuepushe na balaa au janga la vita. Leo nchi hii ikikumbwa na vita mafuta tutakayotumia kwenye vifaru, kwenye

majeshi tutaenda kuomba kwa watu binafsi, huu ndiyo ukweli. Serikali imejiandaa vipi? Serikali inahifadhi vipi mafuta yake kwa faida ya Taifa hili? Ni chombo gani kinasimamia mafuta ndani ya Taifa hili? Leo tunawashukuru wana watu wa *TRA*. Nimshukuru sana ndugu Kitilya na Makamishna wake wote. Tunapewa taarifa kwamba mapato ya Taifa yameongezeka kwa asilimia 25 kutokana na mafuta. Inaonekana *TRA* wanafanya kazi kweli kweli na wanastahili kupongezwa, lakini sisi wenyewe kama Serikali tumefanya nini katika hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe ushauri kwa Wizara ya Fedha na *TRA* kwa ujumla kwa sababu tayari kuna tamko kwamba *flow meters* zitafungwa kwenye bandari ya Dar es Salaam mwezi wa saba. Mheshimiwa Mramba ameeleza kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge kwamba Julai 25 *flow meters* zitafanya kazi. Nashauri bandari ya Dar es Salaam itumike kama bandari pekee ya kuingiza mafuta hapa nchini ili kudhibiti hali halisi ya matatizo yanayojitokeza.

Baadaye tukiwa na uwezo wa kufunga *flow meters* Mwanza, Tanga, Mtwara na kwenye *borders* tutaruhusu, lakini kwa sasa hivi tu-*centralize* bandari ya Dar es Salaam iwe ndiyo *entry* moja tu yenye uwezo wa kuingiza mafuta na yadhibitiwe pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilimwambia Waziri Kigoda kwenye Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi tarehe 31 Mei, 2004 kwamba, kwa taarifa nilizonazo kesho mafuta yanapanda bei. Nilikuwa ninamaanisha mwezi Juni. Bajeti inasomwa hapa ndani bei ya dizeli ukinunua Dar es Salaam kwenye *depot, TOTAL, ORYX* na *GAPCO* ilikuwa Sh.736/=, leo imepanda kwa Sh.50/= tokea siku iliyosomwa Bajeti na leo, tofauti ya siku 5 tu! Kumetokea nini? Alaumiwe nani? Tumuulize nani? Hakuna chombo madhubuti cha kusimamia suala la mafuta katika Taifa letu. Leo tunazungumza kilimo ni uti wa mgongo, tunakubali, lakini mafuta ni sehemu ya uchumi katika Taifa lolote duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Fedha iliangalie suala la mafuta kwa makini sana, athari zake ni kubwa kwa usalama wa Taifa hili na kwa uchumi wa Taifa hili. Lolote litakalotokea katika Taifa letu bado tutasema majuto ni mjukuu. Zambia pamoja na umaskini wao wameing'ang'ania *TIPPER* yao hadi leo . Kenya wameng'ang'ania *TIPPER* yao, Tanzania kulikoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wako viongozi wazuri sana wenye uchungu na nchi hii waliishauri Serikali kwamba *TIPPER* ibaki kama mali ya Serikali. Viongozi hawa wamepuuzwa, hakuna aliyewasikiliza, leo tunazungumzia mafuta, mafuta, mafuta. Kesho kutatokea kilio kikubwa katika Sekta ya mafuta. Suala la mafuta ni nyeti na linahitaji mazungumzo marefu na linahitaji ushirikiano wa pamoja ili Taifa liende pamoja kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niingie kwenye eneo la umaskini. Leo tumezungumzia kilimo. Tunazungumzia kilimo kwa uchungu, wakulima wetu vijijini wana mashamba, wana majumba, lakini hawana hati za kumiliki mashamba wala majumba yao, nani atawapa dhamana? Mkopo watapata wapi? Namshauri Mheshimiwa

Waziri wa Fedha atenge Bajeti maalum kwa ajili ya kupima mashamba ya wakulima vijijini. Wakulima vijijini wana mashamba, mwingine ana eka tano, mwingine kumi, mwingine ishirini, hawana hati za kumiliki mashamba yale. Wakulima vijijini wakivuna wanajijengea majumba yao, lakini hawana hati za kumiliki nyumba hizo. Leo mkulima anahangaika kutafuta mkopo, mtaji wa kuendesha biashara hana, lakini ana nyumba ana shamba ambavyo havitambuliki kisheria. Serikali itenge Bajeti kupitia Halmashauri za Wilaya kupima mashamba na nyumba za wakulima vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwa upande wa *TRA*. *TRA* wenzetu wanajitahidi sana, kuanzia Kitilya hadi Makamishna wanafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa. Tatizo la *TRA* ni ngazi za chini. Ukimuangalia Kamishna Kasera, *Income Tax* ameimudu sana. Ukimwangalia Kamishna Lauwo, amemudu sana Kitengo cha Forodha. Ukimwangalia Luoga pale amemudu. Ukienda *VAT,* Malya anajitahidi, lakini tatizo linakuja huku chini. Sasa hivi katika kitengo cha *VAT* kuna matatizo. Matatizo ambayo yamesababisha Serikali leo imeondoa *stamp duty,* iliondoa *sale tax* yatakuja kusababisha hata *VAT* iingie dosari. Leo hata dereva wa *TRA* anakagua *VAT* kwenye maduka ya wafanyabiashara, ni aibu! Ni aibu na ushahidi upo. Ukienda mikoani wataalam wa idara ya *VAT* ndiyo wamekuwa kero kubwa, ukaguzi hauishi kila kukicha. Kuwe na utaratibu maalum wa kukagua *VAT.* Idara ya *Income Tax* imefanikiwa sana katika *TRA,* lakini Idara ya *VAT* bado kuna tatizo. Ningemshauri Kitilya awatumie wataalam wa Idara ya *Income Tax* wafanye kazi nzuri kuimarisha Idara ya *VAT.* Kwa kweli watupeleke mahali ambapo kesho na keshokutwa tutakuja kusema uchumi wa Taifa hili ulisimamiwa vizuri. Katika suala la utekelezaji na usimamizi, mimi *TRA* nawapongeza sana, wanasimamia, wanatekeleza. Kwenye mapungufu ni wajibu wetu kuwaeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye tatizo la chakula. Tanzania Taifa lenye watu wasiopungua milioni 35 tunapewa msaada wa chakula kutoka India. Bandari ya Dar es Salaam kuna tani 5,000 za mchele tumepewa msaada na Serikali ya India, leo wiki mbili zimepita Wizara inapata kigugumizi ni jinsi gani mchele ule utolewe na ugawiwe kwa nani. Tunarudi kule kule kwenye matatizo, kesho tutakuja kuambiwa: “Chele naoza baba.” Mchele umekuja mzuri, mchele uko bandarini, urasimu wa kugawa mchele ule unachukua miezi. Miezi sita iliyopita tani zaidi ya 700 za mchele zilioza, wanasema meli ilitoboka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa namtania *AG* siku moja namwambia: “Chele yote naoza bandarini baba.” Ulikuwa mchele wa *Grants* ya Japan. Sasa leo umekuja mchele kutoka India tani 5,000 ziko pale bandarini, lakini tunaambiwa kuna njaa huku siku zinzenda. Serikali ya India imetoa mchele, kwa Serikali ya Tanzania kugawa mchele ule imekuwa kigugumizi. Hivi jamani tunakwenda wapi? Watu wa India ni zaidi ya bilioni 1 wanalima, wanavuna, wanaendesha nchi yao kwa utaratibu ambao sisi tunatakiwa tuige kwao. Taifa kama lile linatusaidia tani 5,000 kwa kweli kwanza tutoe shukrani, lakini tuige. Tufike mahali tuwe watu ambao tunaona wivu wa maendeleo katika mwamko wa kiuchumi katika mataifa mbalimbali duniani, hususan katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika uwanja wowote wa ndege kuna sehemu inaitwa *runaway,* ndege inasimama pale ina-*takeoff.* Tanzania kama nchi sasa hivi tupo katika

*runaway*, tuna-*takeoff* wakati wowote katika uchumi. Katika uchumi tumejipanga na Rais Mkapa katufikisha tayari ku-*takeoff.* Hivi tunamsaidiaje kufunga mikanda ndani ya ndege yetu ku-*takeoff* kiuchumi? Hatujaweza kumsaidia Rais wetu ku-*takeoff* katika suala la uchumi. Wabunge, Mawaziri na viongozi wengine tuna wajibu mkubwa wa kumsaidia Rais wetu tuweze ku-*takeoff* katika suala la mabadiliko ya uchumi duniani. Misingi imara imeshawekwa, uchumi umeimarika, tunakubalika ndani na nje, tatizo linakuja usimamizi na utekelezaji. Nashauri tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo vijijini ni benki kwa ajili ya wakulima, lakini vijijini tuna *SACCOS.* Turiani sehemu ambayo tunalima sana miwa na tunazalisha sukari tuna *SACCOS* moja sasa hivi ina mtaji wa Shilingi milioni 300. *SACCOS* ile ndiyo benki ya wakulima vijijini. *SACCOS* za namna ile zinapata msaada na utaalam kutoka *CRDB* na *SACCOS* yetu sisi ya Mtibwa pale Turiani inayoitwa *MOA SACCOS. MOA* ni *Mtibwa Outgrowers Association.* Tumepewa Shilingi milioni 300 kutoka *CRDB,* ningeshauri utaratibu ule uliotumika Turiani kupitia *CRDB* utumike katika *SACCOS* nyingine hapa nchini kuwasaidia wakulima. Kipindi hiki *CRDB* wana uwezo wa kufundisha na wanao wataalam wanakwenda vijijini na wanasimamia *SACCOS.* Ningeomba wakati tunajiandaa kuanzisha benki ya mkulima, *SACCOS* ambazo zipo kuwasaidia wakulima waliojiunga kwenye ushirika zipate mitaji na ushauri kupitia *CRDB.* Katika Jimbo langu nina *SACCOS* zaidi ya 30 ambazo zinapata utaalam kutoka *CRDB,* Tawi la Morogoro. *SACCOS* kubwa kabisa ni hii ya Mtibwa iliyopata mtaji wa milioni 300 na mwaka huu tumeomba milioni 700 na inawezekana kwa msimu huu wa mwaka 2004/2005 tukapata milioni 700 kutoka *CRDB.* Sisi vijijini, *SACCOS* ile tunaita benki. Ningeomba Wizara ya Fedha iliangalie hili kwa makini ili na maeneo mengine yaweze kufaidika kupitia utaratibu huu wa *CRDB. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, niipongeze sana Serikali kwa uamuzi wake wa kujenga Uwanja wa Taifa na wa kisasa. Nimpongeze Mheshimiwa Rais katika kipindi chake ameweza kufanya mambo makubwa pamoja na hili katika michezo. Tatizo ambalo litajitokeza siku za usoni ni miundombinu kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam kufika kwenye uwanja wa kisasa na kurudi katikati ya Jiji la Dar es Salaam, Serikali kama Serikali tunalionaje hilo? Sasa hivi shughuli zote za kitaifa, shughuli zote za ndani ya Taifa letu tutakuwa tunazifanyia kwenye uwanja wa kisasa. Je, kutoka kwenye uwanja ule na kurudi katikati ya Jiji na kwenda kwenye maeneo yenye mahoteli makuba miundombinu gani iliyoandaliwa na Serikali kwa ajili ya faida ya kesho ya Taifa letu? Ni jambo la kujiuliza, ni jambo la kujipanga, ni jambo la kulitolea maamuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Dr. Aisha Kigoda kwa kupotelewa na mzazi wao (baba yao) na tunamwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Bariadi Mashariki. Mheshimiwa Makanga amezaliwa nyumba ya CCM. Ulizaliwa ukakulia huko, ukachomoka ukaingia sehemu mbaya, sasa umerudi. Mtoto mpotevu anapokelewa kwa shangwe. Kwa hiyo, tunakupongeza sana. Nilimuona amevaa shati la green alikuwa kweli anapendeza. Sasa Mheshimiwa umefika kwako. Karibu nyumbani. Napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Mramba na Mheshimiwa Dr. Kigoda kwa hotuba zao nzuri. Nchi hii tukikumbuka tulikotoka miaka ya 80 na mahali ambapo Mheshimiwa Mramba anatupeleka kwa kweli anastahili pongezi. Sasa hivi ukienda Dar es Salaam, na sehemu zote hata huko Serengeti barabara zimetengenezwa wanasema: “Hivi hizi pesa zilikuwa wapi?” Hii ni namna alivyoweza kusimamia hela zinapotoka. siku hizi hela zikitoka huko zinatumika vizuri. Kwa hiyo, ninakupongeza sana Mheshimiwa Mramba.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais alipotembelea mwaka 2000 akikampeni, alitoa ahadi kwamba Serengeti itapata umeme na itapata bwawa la maji. Ninayo furaha na ninampongeza Mheshimiwa Rais kwamba ahadi zake zimetimia. Sasa hivi bwawa la maji la Manchira makarandinga yako huko yanalia, baruti zinapigwa na kazi inaendelea. Kwa hiyo, napenda kuishukuru sana Serikali. Nilitembelea pale nikakuta kwamba *60 percent ya spillway* ilikuwa imekwisha na sasa makarandinga mengine yakaingia siku hiyo niliyokwenda na wanaendelea na kazi. Sasa walichoniambia ni kwamba: “Kamwombe Mheshimiwa Mramba tutakapoingia kutengenza tuta atuletee hela kwa sababu kama tukisimama mvua ikaja bila ya kazi yoyote tutakayokuwa tumefanya kwa kweli itakuwa haina maana.” *(Makofi)*

Namwomba Mheshimiwa Mramba atukumbuke kutoa hizo pesa mapema kwa sababu sisi tuna mvua mara mbili. Kipindi cha kiangazi ni kati ya mwezi wa saba na wa tisa, baada ya hapo mwezi wa kumi mvua inanyesha tunalima, tunavuna. Tena inaanza kunyesha mwezi wa pili tunalima, tunavuna. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mramba naomba sana utukumbuke hapo mwezi wa saba hadi wa tisa ile kazi ikamilike ama sivyo tukikosea hapo kazi haitafanyika tena.Wakati Mheshimiwa Rais alipokuja aliahidi kwamba Serengeti itapata umeme na kwa kweli tunapoongea hapa Wizara ya Nishati na Madini imefuatilia hili jambo, pesa zimepatikana, *contractor* amepatikana na kazi inaanza. Sasa naomba Serikali ifuatilie ili kazi hiyo iendelee bila kusimama kwa sababu mwaka 2005 ndiyo tuliahidiwa kwamba umeme utapatikana. Upatikane *on time. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipokwenda jimboni nilitembelea Hospitali ya Nyerere *DDH.* Nilipofika nikaambiwa kwamba kuna mgomo hapa. Nikauliza: “Huo mgomo wa nini?” Je, mganga ana matatizo?” Wakasema: “Hana.” Nikauliza tena: “Tatizo ni nini?” Wakasema: “Hatujaongezwa nyongeza ya mshahara uliotangazwaJulai, 2003.” Nikashangaa, mbona mimi nimeishakula nyongeza zangu nimemaliza kwa nini nyie mpaka leo bado? Kukawa na barua imetoka Wizara ya Afya ikisema tatizo ni kwamba, hospitali zote za *mission,* wale wafanyakazi ambao wako Serikali Kuu hawajapewa nyongeza mpaka *May 14th*. Sasa jamani, kweli hiyo ni sawa? Yaani hata huko maporini hawapewi nyongeza ya mishahara on time! Nafikiri hicho ni kitendo cha aibu, ninaiomba Wizara ya Afya ambayo ilichelewesha kupeleka majina yao kwa Wizara ya

Utumishi ihakikishe inafuatilia na hao watu wanalipwa mishahara kwa sababu wakikwama watu watakufa na itakuwa ni kwa ajili ya uzembe na Wizara hiyo italaumiwa. Naomba sana suala hilo lifuatiliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, nilikutana na walimu. Walimu wanalalamika kuhusu malimbikizo yao ya miaka na miaka. Ninashukuru Mheshimiwa Mramba amesema kwamba mwaka huu yatashughulikwa. Naomba hilo suala nalo lishughulikiwe kwa sababu walimu wenye njaa hawawezi kufundisha. *A hungry man is a hungry man,* hawezi kufanya kitu cha maana. Kwa hiyo, wenyewe tuwakumbuke, watoto wetu wataanguka mitihani kwa sababu walimu wana njaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchumi wetu, nashukuru kwamba unakua kwa asilimia 6. Zamani tulikuwa na *negative,* sasa tumeingia asilimia 6. Ninawapongeza sana Wizara ya Fedha, ukusanyaji wa kodi umekuwa ni mzuri, wamejitahidi sana hawa watu wa *TRA*. Ndugu yangu Kitilya ni jirani yangu tunaishi naye, kila siku nikimwona najisikia vizuri, huyu mtu anafanya kazi vizuri na Mheshimiwa Mramba nikimwona nafurahi. Siku hizi tunalimiwa vibarabara ambavyo tulikuwa hatulimiwi, eeh! Tunawapongeza, lakini uchumi wetu siyo endelevu. Kitu tunachotaka ni kuwa na uchumi ambao ni *sustainable.* Sasa nitasema ni kwa nini siyo endelevu. *Budged Deficit 41 percent,* hiyo ni *indicator* ya kutosha kabisa kwamba uchumi huo siyo endelevu. 40 *percent* unategemea hela toka nje zije kukufanyia maendeleo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pesa zikikusanywa zinapelekwa katika matumizi ya kawaida, halafu tunaenda kutafuta nje ndiyo tufanye maendeleo. Hivi wewe unaweza kuendeleza mji wako kwa namna hiyo? Pesa zinanunua ma-VX, kila mtu tukitoka hapa Makatibu Wakuu, wana VX. Nchi maskini kama hii, hela zinatumika kununua VX na *seminars!* Hatuwezi ku-*afford* hiyo *luxury.* Leo nikiwa Rais VX nitazikusanya na kuchoma tu, ingia kwenye *Mark II.* Nitawaambia ingieni kwenye *Mark II* mje ofisini. *I will burn those VXs.* Hivi Dar es Salaam unahitaji VX? Kila mtu anakuja sasa na VX na viyoyozi wanashuka. Nimekwenda Japan hamna VX, nimekaa *South Africa* hamna VX , nimekaa Botswana hamna VX. VX ziko Tanzania, kwa nchi maskini kama hii. *We can't afford.* Ni lazima hela zielekezwe kwenye maendeleo. Tukusanye tupeleke kwenye maendeleo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye kilimo hamna hela. Tukija kwenye deni la Taifa sasa hivi ni Shilingi bilioni 8. Tunaambiwa tunasamehewa madeni lakini ukija kuchungulia deni liko pale pale bilioni 8. Ina maana mtoto anayezaliwa sasa hivi Muhimbili anashuka na deni la Shilingi laki 3 linamngoja pale na linaendelea kukua. *Interest Rate* katika lile deni ni 9 *percent,* ina maana kwamba 700 million *dollars* zinahitajika ku-*cover* hiyo na deni liko pale pale. Tutafute njia ya kulipunguza hilo deni litatufikisha pabaya, tujifunge mkanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa Washington nahudhuria mkutano na watu toka Morocco na nchi zingine wanasema wenyewe wanashughulikia kupunguza deni lao, lakini sisi linaendelea kukua na halizungumziwi. Huwezi kuwa mtu wa maana kama una

madeni. Kama unatembea na madeni watu wanakudharau! Mimi naogopa madeni, hakuna mtu ananidai hapa. Familia yangu ilinikataza Wanyancha usifanye madeni *and I don't.* Sina deni na mtu hapa ndani. Sasa sisi nchi hii Tanzania inanuka madeni *and nobody is talking about it.*

Mheshimiwa Spika, shilingi yetu inavyoshuka ndivyo hivyo deni linaongezeka. Nime-*calculate* mtoto anayezaliwa leo laki tatu zinamgoja, anapozaliwa pale tu, laki tatu zinamngoja ulipe toka wapi? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kama unataka kuua uchumi wako cheza na *transport costs.* Ninyi mnasema mnataka kuinua kilimo mnasaidia kule Kusini yale mahindi hawawezi kuyaleta kuyauza Dar es Salaam hata Shinyanga. Sasa kitu kinachotufanya tushindwe ni madeni, sisi tumeshindwa kupanua *tax collection base* badala yake tunakimbilia kwenda kuweka *VAT* pale pale, sijui kodi gani. Sasa mafuta ni ghali, nchi zingine za jirani mafuta yao ni rahisi kwa sababu deni lao ni ndogo. Sasa ninachoomba Serikali iangalie zile kodi ilizoweka pale izipunguze kusudi watu waweze kulima walete mazao ya-*compete. (Makofi)*

Kwa nini sasa *TRA* imeshindwa, Wizara ya Mheshimiwa Mramba, imeshindwa kuwa na *tax return form* kama unataka kumkamata mtu unamkamata na *tax return form*. Sasa utanikamataje nisipolipa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, riba ya mikopo. Mimi nimekopa juzi Benki ya Posta. Nilisema sina deni na mtu. Sasa nitalipa *19%, inflation 4%* nikiweka hela mle mle nalipa *1%,* haya ni mabenki gani yanatengeneza mabilioni ya hela tunaibiwa hela tuangalie. *(Makofi/Kicheko)*

Haya bei ya umeme, mimi nataka waandishi wa habari mimi na-*declare* kwamba umeme utaendelea kupanda bei, mliosema kwamba utashushwa *is not true.* Sasa hivi tunaingia Songa tutalipa Tshs. 4.5 bilioni. *IPTL* 3.5 bilioni ina maana kila Mtanzania analipa 3,000 *shillings a month* bila kutumia umeme. Sasa una haja gani ya kutoa kodi ya maendeleo halafu wanalipia *fuel? We are not serious.* Kama una umeme wa bei ya juu usitegemee kabisa uchumi wako kukua. Tuangalie mambo haya ni madogo *you do not need to go to school* kujua uchumi una hali mbaya. Uchumi uko kwenye *intensive care unit. (Makofi)*

Haya mishahara ya wafanyakazi unamlipaje mfanyakazi 60,000/= ambapo Kigogo kikikaa kwenye kiyoyozi kinapewa *sitting allowance* ya 60,000 mwalimu amefundisha *300 hours per month,* halipwi hivyo na huyu anakwenda *one hour* analipwa hiyo, *we can't afford,* kutesa watu namna hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haya wawekezaji, tumeleta wawekezaji ninyi mnafikiri kwamba tunawabembeleza hapa wale watu hawana maslahi na taifa hili. Nionyesha walipojenga nyumba, wanachukua hela wanapeleka nje. Nilikuwa *South Africa* hawa wanapeleka hela kule kwao inajengwa, Tanzania inalala, sisi tunalipwa *tax.*

Madini tunalipwa *tax* sasa hivi mauzo yetu 48% ya nje ni mauzo ya madini, lakini zile hela hazirudi. Kwa hiyo, siyo *indicator* ya uchumi. Tunataka tuangalie vitu vya namna hiyo, *you must look our nation interest first.* Kwa kweli sisi tunajidanganya sijui uchumi unakua, *Cigarette Company,* hela zinaenda Japan, *Tanzania Breweries* hela zinaenda *South Africa,* madini sijui Canada, Australia, hivi tunasema nini? Tumeshindwa sisi kukopa hela? Haya shauri yenu! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, haya tuje sekta ya kilimo. Kilimo mnasema kwamba kitafanikiwa nenda *South Africa,* utaona walivyofanikiwa. Mimi nashukuru Mheshimiwa Keenja, nimepata *offer* yake nikaenda kutembelea *South Afrika* kila mahali ni mabwawa, mabwawa ya kumwagilia sisi kiangazi unasema utaendeleza kilimo, mbolea ya kushusha bei unasaidia tu *middle men* hata mimi nataka kuanzisha hiyo biashara mkulima hapati ile anadanganyika tu. Tusidanganye wakulima, *they are finished* na kilimo tukishaua Mtanzania amekwisha, kilimo mlichosema mmefanya *there is nothing,* huhitaji kwenda shuleni kujua kwamba hii ni danganya toto. Haya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kuhusu rushwa. Rushwa ni *clear* kabisa mwaka 1995 tupoanza awamu ya tatu Jaji Warioba akapewa kazi, wamemaliza wakazika kwenye mafaili yanaota ukungu. Rushwa inatembea kama kawaida. Tunasema ipo siku. Angalia hapa Kenya *NARC* imeingia madarakani kwa sababu ya rushwa ilikuwa imekwisha wana-*clear now their house,* sisi tunakaa tunasema nini, *the time will come* wala rushwa watafikishwa panapostahili. Watu wanaopokea rushwa, sisi ni vijana tupo, watakuja kujibu na *election* ya mwaka 2005 *we shall fight it around corruption,* wanaotaka kupigania wajue kwamba na sisi vijana tupo, *we shall fight it against corruption. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sina mengi. Namalizia kwa kusema Mwenyezi Mungu amsaidie Rais wetu arudi salama anaumwa ametufanyia makubwa, *this is a best President I have ever seen* ambaye ameonyesha *economic serious,* yeye hapokei vikaratasi vya kijinga jinga hivyo ni mtu ambaye yuko *serious* tuna m-*miss* sana Mwenyezi Mungu amsaidie arudi.

Namshukuru sana Mheshimiwa Basil Mramba na wewe utakumbukwa siku ukimaliza Uwaziri wako, mambo yako ni mazuri. Baada ya hapo sina mengi, ila naunga mkono Bajeti hii kwa 100% *(MakofiKicheko)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii na mimi niweze kutoa mchango kuhusu Bajeti hii ya Mawaziri wote wawili, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha. Mimi sina kigugumizi chochote naziunga mkono kabisa hoja hizo mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza yale ambayo nimekusudia kwanza nitoe mkono wa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa msiba wa baba yao. Mungu awape moyo wa subira na pia Mungu aiweke roho ya marehemu baba yao mahali pema peponi. Amen.

Pia nampongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kushinda vizuri sana katika uchaguzi wa Bariadi. Ameonyesha vizuri sana dira ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2005. Hizo ni dalili nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo mimi nataka nitoe machango wangu kwa maeneo makubwa matatu; eneo la kwanza nataka nitoe sababu zingine, maana hizo zingine zimeshatolewa na Serikali sababu zingine zinazofanya uchumi wetu kukua polepole na wakati mwingine kushuka. Pia sababu ya pili, nataka niikumbushe Serikali kwa nini umaskini vile vile unakosa kasi kubwa ya kuondoka katika nchi yetu. Tatu, niieleze Serikali kwa nini vijana wanakimbia kilimo kwenda mijini. Maeneo hayo ni muhimu kama tunataka kujenga uchumi ambao ni endelevu, uchumi ambao utajenga uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na kwa nini uchumi wetu hauna kasi nzuri ya kukua. Ziko sababu nyingi, lakini sababu ambazo ninatoa mimi ni zile ambazo nimezifanyia utafiti mimi mwenyewe. Sababu ya kwanza ni kwamba watu wote wanaostahili kushiriki shughuli za kilimo, bado hawajaingia katika sekta hii ya kilimo vizuri, yako makundi mengi tu. Sasa kundi la kwanza ni nguvu kazi ya vijana ambao ni zaidi ya asilimia 30 lakini wapo zaidi ya milioni 10, hawa hatujawaingiza katika sekta ya kilimo. Nitakuja kueleza kwa nini hawa vijana wanakataa kuingia katika kazi hii ya kilimo. Kwa hiyo, hilo ndiyo kundi la kwanza. Lakini kundi la pili ni kundi la taasisi mbalimbali. Ziko taasisi ambazo zingeweza kuchangia katika kilimo, lakini hazijafanya hivyo.

Kwa hiyo, lazima shughuli zetu za kilimo zitaendelea kudorora, zitaendelea kuwa dhaifu. Lakini kundi lingine vile vile la Mashirika ya Umma. Zamani mashirika yetu ya umma yalikuwa yanafanya kazi za kuchangia kilimo, lakini sasa haya masharika ya umma yameacha kabisa shughuli za kilimo, tumewaachia wananchi tu huko vijijini wanagonga gonga kilimo kile cha ujima hakuna kilimo cha kisasa katika maeneo mbalimbali. Lakini vile vile hata vyama vya ushirika ambavyo sasa hivi ndiyo vinanunua, vinauza mazao, vimesahau kwamba kazi yao kubwa kwanza ni kuzalisha, wazalishe halafu ndiyo wafanye biashara hiyo baada ya kuzalisha mazao kupitia kilimo.

Lakini vile vile hata makampuni makubwa, kuna makampuni mengi tu makubwa ambayo yenyewe yanafizia tu baada ya uzalishaji wa wananchi ndiyo wanaingia katika biashara lakini yangeweza vile vile kuzalisha katika kilimo. *(Makofi)*

Eneo jingine katika hilo ni matajiri, tuna matajiri wengi sana, lakini matajiri hawa wote wanavizia tu vitu ambavyo vimelimwa na wakulima hawa wadogo wadogo ndiyo wanafanya biashara. Wangeweza kufanya biashara katika mashamba kwa kulima ili tuweze kuzalisha na kujenga uchumi wetu. Kwa hiyo, kundi hilo lote likiingia kisayansi na kiteknolojia katika kilimo, kinaweza kikakua kwa asilimia 8 mpaka 10, kuliko sasa hivi kilimo chetu kinakua kwa asilimia 4 mpaka 5 kwa vigezo vya mwaka 2002 na 2003. Hili ndiyo eneo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili umaskini haujawezeshwa kupata kasi inayostahili kuondoshwa miongoni mwa wananchi. Bado tunazungumza tu. Sasa kwa nini? Ziko

sababu hasa ambazo naziona vile vile ni muhimu Serikali kujua, inawezekana sisi tunafanya kazi kwenye makaratasi, lakini sisi tunaofanya kazi kule na wananchi, tunaona hali halisi. *(Makofi)*

Sababu ya kwanza, ni kwamba kilimo chetu kwa zaidi asilimia 60 bado ni kile chenye misingi ya ujima bado mabadiliko katika kilimo hakuna, bado tunatumia jembe la mkono, tunataka jembe la mkono libaki kwenye kupalilia, si katika kulima, kulima lazima tulime kwa matrekta, tulime kwa jembe la kukokotwa na ng'ombe na zana mbalimbali, ndiyo tutapiga hatua zaidi. Kwa hiyo, kilimo chetu hakina sayansi, hakina teknolojia ya kileo na vile vile kilimo chetu bado ni cha mtulinga, cha maguvu ndiyo maana hata vijana wanakimbia vijijini, atalimaje kwa kutokwa majasho na kadhalika wakati nchi zingine hazitokwi na jasho? Kwa hiyo, hilo ndiyo jambo la msingi. *(Makofi)*

Vile vile katika hali hiyo basi kilimo kitaendelea kukwepwa na vijana na vile vile kukwepwa hata na wasomi, watashindwa kushiriki kwa sababu bado ni kilimo cha hali ya zamani. Vile vile zana za kilimo na pembejeo huko vijijini, sisi kwa sababu tunaishi kule zinachelewa sana kutufikia. Hata Baba wa Taifa aliwahi kutuambia kwamba mvua zote ni za kupandia siyo za kulimia.

Kwa hiyo, pembejeo zikichelewa ndiyo zile zinafanya mpaka wakulima sasa walime wakati wa mvua ndiyo wapande watachelewa. Kwa hiyo, njaa haiwezi kuondoka. Lakini pia kuna jambo jingine ambapo hatujawa na programu mahususi ya kuondoa umaskini wa kipato. Tumejitahidi sana kupunguza umaskini katika huduma, katika afya, katika elimu, katika maji na kadhalika. Lakini umaskini wa kipato ni kisumbufu kikubwa kwa wananchi. Hiyo, ndiyo hasa tungetilia maanani tuondoe umaskini wa kipato sasa kwa maana kwenye kaya, kwenye nyumba na kadhalika. Namna ya kufanya lazima tukubali tuamue sisi kama nchi tukope katika mabenki ya nje, lakini pia tukope katika mabenki ya ndani ili kuwezesha kuondoa umaskini ndani ya nchi. Tukifanya hivyo uchumi wetu utakua, tutaondoa umaskini na tutaondoa matatizo mbalimbali kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ni lile ambalo nilisema kwa nini vijana wetu ambao ni nguvu kazi kubwa wanakikimbia kilimo vijijini na nguvu kazi hiyo nilishaibainisha inakisiwa kuwa ni asilimia 30 ya wananchi wote, lakini takribani vijana zaidi ya milioni 10 hawajaingia katika sekta hii ya kilimo kwa sababu hakuna zana za kisasa za kulimia. Sasa ni kwa nini basi, kwanza umeme ambao ni nyezo ya kisasa katika kazi haupo vijijini, kwa hiyo hakuna motisha ya kuweza kushiriki katika kilimo vizuri.

Lakini vile vile kilimo hicho chenye zana duni hakihamasishi maendeleo ya haraka ya vijana na uchumi kwa ujumla. Lazima Serikali ijitahidi kuhamasisha kwa sababu tunategemea nguvu hii ya vijana ndiyo itazalisha zaidi tuweze kukuza uchumi, tusipowaangalia hawa vijana wataendelea kuzamia mijini, kitu ambacho hawawezi kuchangia maendeleo vizuri. Maendeleo yatachangiwa katika kilimo hasa vijijini.

Kwa hiyo, uduni wa kilimo hicho kimekuwa kikishindwa kuondoa matatizo mbalimbali na matatizo hayo nimebainisha kwamba ni tatizo la njaa miongoni mwa

wananchi inatokana na hali duni, liko tatizo vile vile la makazi bora, nyumba za wananchi ni duni kama walivyoeleza wenzangu. Lakini vile vile liko tatizo la mavazi, lakini vile vile liko tatizo la elimu kwa wote, afya, matibabu, maji na kadhalika. Kwa hiyo, tunaomba Serikali izingatie katika eneo hilo tupeleke fedha nyingi kunyanyua kilimo ili tuweze kujenga uchumi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kilimo cha kisasa kinachozaa tija kinahitaji mitaji, bila mitaji tutakuwa tunajidanganya. Vijana hawana mitaji, lakini sasa tufanye nini, lazima vijana hao tukubali kabisa kwa kila namna wakopeshwe zana zinazorahisisha kazi za uzalishaji mali, tusipofanya hivyo tutashindwa. Wakopeshwe matrekta makubwa, madogo, pembejeo za kilimo kwa maana mbegu bora, madawa bora, mbolea, hata madawa ya kupalilia, watu wanaweza wakalima maeneo makubwa lakini wakashindwa kupalilia. Lakini vile vile wakopeshwe fedha ili kuboresha maisha yao, maduka wanayoanzisha, wajenge nyumba bora, wasomeshe watoto, wanunue mikokoteni lakini pia waishi maisha ya kileo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la mwisho ni kilimo cha umwagiliaji maji mashamba ni muhimu sana, ni mkakati mzuri wa kuweza kuwaweka vijana pamoja. Kwa hiyo, tutengeneze miundombinu ya umwagiliaji maji mashamba haraka sana. Hiyo, itatusaidia, kuwavutia vijana kushirika katika kilimo, itaongeza pato la walengwa kwa maana wananchi, lakini pia kilimo kitaondoa njaa katika maeneo mbalimbali, kitaongeza ajira nchini, kitapunguza umaskini wa kipato, pato la taifa litaongezeka na uchumi utapanda na wakati huo huo viwanda vitaibuka hakutakuwa na viwanda kama hakuna mali ghafi. Kwa hiyo, tukithubutu na tukawekeza katika maeneo hayo, uchumi utajengeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba niiambie Serikali wananchi wengi wanashindwa kuwasomesha watoto wao elimu ya sekondari, hasa wananchi maskini kule vijijini wanashindwa kabisa kulipia ada. Naomba Sekondari zote tunazojenga tuzifutie ada. Kama hatuwezi kufuta kabisa basi tuwapunguzie wananchi angalau kwa asilimia 60 ili watoto wasome. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru naomba Serikali isikie hayo kwa niaba ya wananchi. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu katika hoja ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji. Lakini awali ya yote nichukue nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu, kutoa rambirambi kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na ndugu yetu Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa msiba uliowapata wa kufiwa na baba yao mzazi. Vile vile, nitoe salaam za pole kwa Mheshimiwa Anne Kilango pamoja na Mheshimiwa Makongoro Nyerere, kwa kupata ajali na matatizo mbalimbali yaliyowasibu wakiwa safarini kuja Bungeni. Nawapeni pole sana na hasa kwa Ndugu yetu Makongoro Nyerere ambaye bado yuko hospitalini. Tunamwombea Mwenyezi Mungu aweze kumpa uponyaji, ili aweze kurejea katika majukumu yake ya Ubunge wake.

Baada ya kutoa salaam hizo za pole, nimpongeze Ndugu yangu Mheshimiwa Danhi Makanga Mbunge wa Bariadi kwa kuchaguliwa na kupewa nafasi ya uwakilishi wa Jimbo la Bariadi. Nampongeza sana yeye mwenyewe na wananchi wa Jimbo la Bariadi kwa kutoa ridhaa yao kwa Chama cha Mapinduzi na Mbunge wao aliyekuwa akiwakilisha kwa tiketi ya *UDP*. Lakini vile vile nichukue nafasi hii kuwapa pole ndugu zetu wa *UDP* kwa kupoteza lile jimbo na kuwatakia faraja kwa hayo waliyoyapata na kuwaombea waweze kuwa na subira na uvumilivu. *(Makofi)*

Sasa baada ya pongezi hizo nichukue nafasi hii sasa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha ndugu Basil Mramba, pamoja na Manaibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Makamishna, Mhasibu Mkuu pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa hoja ambazo wametuletea. Mimi nawapongeza kwamba wametuletea hotuba nzuri, Bajeti nzuri, mipango mizuri na ambayo inatupatia heshima kwa kazi ya kujenga uchumi wa nchi yetu. Nawapongeza kwa sababu kuendesha Bajeti katika nchi maskini ni kazi ngumu sana. Nilikuwa nikipiga hesabu ndogo ndogo hapa za mapato yetu ya ndani ya trilioni moja na upuuzi kwa Watanzania milioni 35 na kupata kwamba kila Mtanzania ange-*contribute* Sh.46,900/= karibu Sh.47,000/=. Sasa Watanzania wote kila mtu akichangia kwa mwaka 47,000 halafu ndizo unampa mchumi ama mhasibu akazipangie maendeleo na shida zote za Watanzania, hili ni gumu sana. Kwa hiyo, wanapotusikia tukipa kelele hapa wasije wakafikiri sisi hatuoni uzito wa kazi yao. Lakini hii kwa sababu umaskini ni mpana hilo la kwanza na la pili kizuri hakikosi hila hata mwanamke mzuri hakosi kasoro na bado hakati tamaa ya kuolewa. Kwa hiyo, nawaomba wasikate tamaa kazi yao wanayofanya ni nzuri na inaonekana. *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya kutoa shukrani zangu hizo na kuwapongeza kwa kazi yao nzuri mimi mchango wangu nitaelekeza katika sehemu tatu, ya kwanza ni Bajeti yetu tegemezi ya pili ningependa niongee kuhusu Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2003 na mwisho mkakati wa kupunguza umaskini. Sasa nikianzia na ile Bajeti tegemezi imepungua kutoka asilimia 47 mwaka 2001 ikaja asilimia 45 na sasa tumeambiwa imefikia asilimia 41. Kwa kweli kasi yake ya kupungua si kubwa lakini wanastahili kupongezwa kwa hayo wanayoyafanya. Mimi nadhani ningechukua nafasi hii vile vile kuwapongeza *TRA* kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kutusaidia sisi kuondokana na dhana ya kuwa tegemezi. Nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa *TRA* Ndugu yetu Kitilya kwa kazi nzuri anayoifanya na wenzake. *(Makofi)*

Tunamwomba aendelee kuweka jitihada hizo. Lakini pamoja na kumtaka aendeleze jitihada za kukusanya kodi itafikia mwisho kwamba kodi haifai kuchukulika zaidi sawa sawa na kumkamua ng'ombe utafika hatua unakamua ng'ombe maziwa yameisha sasa utakamua damu. Nadhani kitu kizuri kwetu ni kumwandalia mazingira ya kuweza kumwongozea uwezo na mazingira mazuri ya kupata kodi kubwa. *Tax base* kubwa. Mimi nafikiri ili kuweza kulifanya hilo tunahitaji kwa nguvu zote kabisa ku-*promote* kilimo, kilimo lazima uwe ndiyo msingi wetu wa maendeleo. Watanzania wote wakiwa na uwezo wa fedha kwa kilimo na ambapo ndiyo ajira kubwa ilipo wataweza kulipa kodi. *(Makofi)*

Kule kwetu kilimanjaro katika wilaya zote, Wilaya ya Hai inaongoza kwa mapato ya kodi. Lakini si kwa sababu ya wafanyabiashara bali kwa sababu ya wakulima wakubwa walioko pale. Kwa hiyo, nina imani Serikali ikikubali kwa makusudi kabisa kuwekeza katika kilimo tutaweza kuondokana na hili tatizo la utegemezi. Utegemezi huu unatokana na uwezo mdogo wa watu wetu kulipa kodi, inakuwa kama mtu amekwenda kuwinda mnyama mdogo kama sungura halafu wako watu 20 wote wanataka kumla na ndicho kinachotokea hapa, kila Mbunge anaposimama anataka *share* yake, kila Mbunge anayesimama anataka apate *share* yake, lakini kapo kasungura kadogo tu. Wabunge karibu 250 wote wanataka kumla sungura wa kilo tatu. Huu ni mtihani mkubwa sana.

Sasa kama tungeweza kukijenga kilimo vizuri mimi nina imani tungeweza kuwajengea wananchi wetu uwezo wa kuongeza kodi. Vinginevyo walipa kodi wakubwa watakuwa watu wa viwandani na watumishi wa Serikali na mashirika ya umma nao watafika ukomo wa kuweza kulipa kodi.

Lakini nashangaa kwamba kilimo hakijapata kipaumbele. Katika kitabu cha Bajati cha Waziri wa Fedha ukurasa wa 64 na 65 ibara ya 53, Waziri anasema waziwazi kwamba sisi Wabunge sasa tuweze kutoa kipaumbele kwa kilimo, sekta ya kilimo iwe sekta ianyoongoza. Waziri wa Fedha ametuambia, lakini katika kitabu cha Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ukurasa wa 54 na 55 ibara ya 91 Waziri naye anasema vipaumbele amevitaja pale katika mipango ya nchi, lakini kilimo hakipo, ametaja habari ya chakula ni sawa sawa na ukisema unamtaja mtoto bila kumtaja mama yake, haiwezekani. Mimi ningefikiri bado Serikali pale katika mipango yake inasuasua, inajiuma uma, lazima iweke kabisa sekta ya kilimo iwe sekta ambayo inaongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa kuondoa punguzo la kodi za sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi. Nawapongeza sana na hii nasema itakuwa changamoto kwa wakulima wetu na wafugaji wetu katika kuweza na kujiendeleza. Lakini bado Serikali inatakiwa ku-*address* tatizo la kilimo *specifically* kwa kuweka *physical development* ifahamike ni kitu gani wanafanya. Kwa maneno mengine tungeiomba Serikali ituletee hapa mpango mzima wa maendeleo ya sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Lingine ni kuhusu Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2003 imetajwa katika ukurasa wa 57 ibara ya 48 ya kitabu cha Waziri wa Fedha kwamba Serikali Kuu ilifuta ushuru wa jasi, chokaa na vitu vya namna hiyo. Sasa mimi sielewi mwaka mmoja tu umekwisha Serikali inakuja na hoja ya mrahaba na hao wanaolipa hii kodi siyo wawekezaji wakubwa wa jasi, siyo wachimbaji wakubwa wa jasi hawa ni wadogo wadogo kule kwetu wanakuja na hoja sasa wanatumia neno mrahaba wakati neno mrahaba lilikataliwa, lakini ni ushuru huo huo. Mimi ningeomba Serikali isiende mbele na nyuma. Hakuna gari linalokwenda *forward* na *reverse.* Hakuna! Mwaka jana tu leo wanageuka. Sasa kule kwetu wachimba jasi wanajua walifutiwa kodi mwaka mmoja leo inarudishwa tunaelekea kwenye uchaguzi, mimi nakwenda kuwaambia nini? Nakuomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuwe na sheria ile isibadilike badilike kama tunaamua kurejesha hiyo basi na kodi ya maendeleo ungesema kwamba ni kianzio cha mapato ya Serikali za Mitaa cha kutosha.

Lakini hili linakuja kwa sababu Serikali imeshindwa kufidia sehemu ya fedha ambazo imefuta vianzio vya Halmashauri, Serikali Kuu, ilishindwa kule katika Halmashauri wamekuwa wakilalamika sana. Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, ujitahidi kuhakikisha vianzio vile vinafidiwa inavyostahili ili kuondoa mgogoro wa kisiasa uliko kule. Serikali imeondoa lakini haitimizi kile ilichoondoa na hatimaye yanaletwa maombi madogo madogo. Mimi ningeomba hii ya ushuru wa jasi ifutwe kama ilivyokuwa katika sheria ya mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni mkakati wa kupunguza umaskini. Mkakati wa kupunguza umaskini msingi wake wa kwanza ni kilimo, kama nilivyosema. Lakini tuna mambo matatu lazima tuyazingatie. Kwanza ni kufanya kazi kwa bidii. Watu wetu bado hawajafanya kazi kwa bidii. Kule vijijini wanaofanya kazi wengi ni wanawake. Kwa sababu hiyo napenda leo nimnukuu hayati Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, katika kitabu chake cha Ujamaa *Essays on Socialism.* Hakina ubaya kukisoma leo. *(Makofi)*

Ukurasa wa 30 anasema: *"It will be appropriate to ask our farmers especially the men, how many hours a week and how many weeks a year they work. Many do not even work for half as many hours as the wage earner does. The truth is that in the villages the women work very hard. At time they work for twelve hour and fourteen hours a day. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hiyo, inatufikisha kwenye muda wetu wa kupumuzisha kikao kwa ajili ya mapumziko ya mchana. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika naomba nichukue nafasi hii ya awali kuwapa mkono wa rambirambi Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kuondokewa na mpenzi baba yao. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahala pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nitoe pole kwa wenzetu waliopata matatizo katika barabara hii yetu ya Dodoma-Dar es Salaam. Nikianza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Makongoro Nyerere na jana tena mwenzetu naye alipata matatizo Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii kwa ujumla na mwelekeo mzuri, Uchumi mzuri Tanzania ni mzuri, unatia moyo. Mwaka ujao iwapo kila kitu kitaenda ilivyopangwa, uchumi wetu utakuwa kwa asilimia 6 na ukuaji huo na ule wa mwaka jana Tanzania sasa inaongoza katika Afrika Mashariki katika ukuaji wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna aibu ya kutaja hili wala haya kwa sababu ni mafanikio yetu na hasa sisi wa Chama Cha Mapinduzi. Hata hivyo, mimi sikusimama hapa kusifu tu. Kwa sababu sifa zimetolewa sana. Naomba niende haraka haraka kwenye maeneo machache ambayo nafikiri yaleta tija zaidi katika hoja hii. Sipendi kurejea yaliyosemwa na wenzangu. Lakini kwa ajili ya umuhimu naomba nisemee kidogo tu eneo la mishahara ya Walimu.

Walimu wetu wanahangaika sana, walimu hawa sasa hivi ni vijana. Ndiyo wamepelekwa vijijini kutoka katika maeneo ya mbali. Kutoka Mtwara kwenda Ngorongoro. Kutoka Tabora kwenda Tanga. Hawana ndugu, hawawezi kupiga simu, wanaishi maisha magumu. Kwa kweli wenzangu walisemea jambo hili kwa uchungu na mimi nalisisitiza. Agizo litolewe kwa wahusika kule Wilayani, Wakurugenzi kuwakopesha walimu ili waachane na haya maisha magumu. Suala la madeni linanipelekea pia kwenye Idara mbalimbali, Idara ya Magereza na pamoja na *Cash Budget* lakini bado Serikali imewakopa wananchi kwa mabilioni na Idara sugu ni Magereza. Naomba Waziri atuelezee atafanya nini madeni yaliyolimbikizwa kwa mabilioni kwa Idara hii ya Magereza na hii pia kwenye Idara ya Polisi. Kwa sababu inawatia pengo kubwa sana wafanya biashara wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la rushwa limesemwa humu Bungeni kuhusiana na Bajeti hii. Mimi nisingependa nirudie yale yaliyosemwa. Kwa ajili ya uzito wa jambo hili ambalo haliongelewi kwa wanasiasa. Juzi kwenye *breakfast* ya *Budge*t hii kule Dar es Salaam. Mwenyekiti wa wadau wa Sekta binafsi ambaye nadhani ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya *Cement* ya Tanga.

Amesema tatizo katika utekelezaji wa Bajeti hii baadaye itakuwa ni tatizo la rushwa katika jamii yetu. Mapambano dhidi ya rushwa katika nchi yetu ukilinganisha na nchi jirani Kenya, yanaonekana kama sisi tunategemeana. Lakini kwa miaka ya karibuni tulikuwa tunachukulia mzaha tunapoambiwa kwamba pengine tutaje majina hapa Bungeni. Na jana Mbunge mmoja, ameenda mbali amesema tuwadhibiti humu humu ndani ya Bunge. *(Kicheko)*

Mimi nataka kusema kwamba hii siyo kazi ya Bunge na siyo namna ya kupambana na rushwa. Wenzetu, nchi jirani, hawakuwaondoa kazini nusu ya Majaji wa Mahakama Kuu kwa kutajwa Bungeni. Karibu sehemu kubwa ya Majaji wa Mahakama ya Rufaa, Mahakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi kule Kenya zaidi ya robo hawakutajwa Bungeni. Ni dola ilifanya kazi yake. *(Makofi)*

Watumishi wa Idara mzima ya Misitu ilistaafishwa, haikutajwa Bungeni. Bunge hii siyo kazi yake. Kazi ya Bunge ni kutunga Sheria. Kupitisha makisio ya matumizi ya

mapato ya Serikali. Hili kazi nyingine ni kazi ya Serikali, nawasihi kweli na hili nalisemea kutokana na Bajeti hii hasa katika eneo moja tunaambiwa kwamba asilimia 70 ya Bajeti hii shilingi trillion 3.3 itakuwa ni kwa ajili ya manunuzi, kwa maana kwamba tunatumia ile Sheria yetu ya Manunuzi ya Serikali, Sheria Na. 3 ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili, ndilo eneo linalofikiriwa kwamba ni chanzo kikubwa cha matatizo ya rushwa na uongozi mbovu. Ukiangalia *hansard* mimi sikuchangamkia sana Sheria hii mwaka 2001 wakati ilipoletwa kama Mswada hii yaani *the Public Procurement Act).* Kwa sababu nilikuwa na wasi wasi mno jinsi ambavyo ilikuwa inaweka ukiritimba katika maeneo fulani ya tenda, kutoka ngazi ya juu mpaka ngazi ya chini na hasa ngazi ya juu, *Central Tender Board (CTB).* Wajumbe wa *CTB* sidhani kama Waheshimiwa Wabunge wanafahamu. Ni ma-Katibu Wakuu ambao ni maskini sidhani kama hata wanao muda wa kushughulikia kwa kina tenda hizi au wanaoshughulikia ni Maafisa Wadogo katika Wizara mbalimbali. Lakini hili siyo tatizo tu, matatizo ya Sheria hii ni mengi kiasi cha kwamba wiki iliyopita Ofisa mmoja katika Wizara ya Fedha, nisingependa kumtaja asije akachukuliwa hatua. Katika Semina ya manunuzi amesema ifuatavyo, naomba nimnukuu kwa Kiingereza.

*The procurement assessment report for the year 2003 has estimated that Tanzania looses US dollar three hundred million annually through kickbacks and bogus procurement procedures.*

Dola milioni 300 maana yake ni zaidi ya shilingi bilioni 300 na haya yamesemwa na Afisa wa ngazi ya juu sana katika Wizara ya Fedha wiki iliyopita akiongelea kwenye Semina ya Ununuzi. *(Makofi)*

Afisa huyo ameendelea kusema kwamba naomba nimnukuu tena kwa lugha ya Kiingereza, anasema: *The Procurement Act needs review, because there are short falls that have created problems to some tenderers and Tender Board. He said that, the Government of Tanzania and Parastatal Organizations spend about seventy percent of the recurrent Budget and almost of the Development Budget on Procurement of goods, services and construction works."* Mwisho wa kunukuu.

Huyu ni Afisa wa ngazi ya juu katika Wizara ya Fedha, labda yuko hapa, akitoa Semina wiki iliyopita juu ya Sheria hii. Hii maana yake ni kwamba zaidi ya asilimia 70 ya shilingi trilioni 3.3 matumizi yake hatutakuwa na uhakika nayo kwa matamshi ya Wizara ya Fedha. Anataja upotevu kwa ajili ya rushwa, ndiyo tafsiri ya *kickbacks* na ubadhirifu kwa tafsiri ya *bogus procurement procedures,* inatugharimu shilingi bilioni 300.

Sasa hii maana yake ni nini, Mheshimiwa Naibu Spika. Hii maana yake ni kwamba mazuri yanayoongelewa katika Bajeti hii kwa hakika katika utekelezaji ni kinyume na ndiyo maana mimi naungana na Afisa huyu wa Hazina kwamba wakati umefika kuangalia upya kabisa Sheria hii ya Manunuzi ya Serikali. *(Makofi)*

Itakumbukwa mwaka wa fedha wa 2002/2003 manunuzi makubwa hayakufanyika karibu nchi nzima. Kwanza kwa sababu wengi katika Wilaya, katika taasisi za Serikali Wakala, Mashirika ya Umma hawakuwa wameifahamu vizuri sheria hiyo.

Lakini pia zaidi urasimu. Kwa sababu tenda hizi hasa zikiwa kubwa, ya mabilioni itaanza kwenye Shirika fulani, itaanza kwenye Wilaya fulani, itaanza kwenye Mkoa fulani. Hatimaye hadi ifikie kwenye ama Wizara ndiyo inafika kwenye ile Kamati ya Tenda ya Wizara au kwenye *CTB*. Nayo ina matatizo makubwa sana. Sasa ndiyo unakuja kwenye *CTB* ambayo inashughulikia mabilioni na mabilioni ya fedha na ni sehemu kubwa ya Bajeti hii ya shilingi trilioni 3.3 kwa mwaka wa fedha 2004/2005.

Tumeambiwa hapa Waziri aliliona hili na amefanya marekebisho fulani, sijui marekebisho gani. Kwa sababu kisheria hatukumpa nafasi hiyo. Sheria tumempa nafasi ndogo tu ya kufanya mabadiliko katika viwango. Viwango vya Wilaya, vyombo vya Mkoa, viwango vya *Ministerial Tender Board,* viwango vya *Central Tender Board.* Lakini tatizo ni muundo mbaya. Viwango ni jambo moja, miundo ni jambo tofauti.

Kwa hiyo, basi kama tukitaka Bajeti hii ambayo ni ya mwisho mwisho katika awamu yetu binafsi ningeomba Mheshimiwa Waziri afanye kila jitihada kabla hajaleta ile *Bill* yetu, *Finance Bill* mwishoni mwa Bajeti hii, tufanye kwanza Semina ya kutathmini *the Procurement Act of 2001. (Makofi)*

Tathmini hii ambayo wataalam wamefanya sisi Waheshimiwa Wabunge tuione, kwa sababu inaonekana tatizo ni kubwa zaidi kuliko tulivyotarajia wakati ule tunapitisha Sheria hii.

Haraka haraka Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo cha shilingi ya Tanzania sasa hivi ni dola ya Amerika. Hatujui imeanzia wapi, kwa sababu hatujafanya biashara kubwa sana na Amerika, na Amerika hawajawa watawala wetu.

Lakini sasa hivi hali ya dola ya Amerika ni mbaya sana. Mheshimiwa Waziri kama Msaidizi wako atakuwa anasafiri kwenda nje akakuchukulia noti za Amerika amekupa hasara kubwa sana. Kwa miaka mitano iliyopita dola ya Amerika ukilinganisha na Euro imeshuka sana na hii imetupa hasara kubwa katika biashara yetu yetu. Biashara yetu kwa asilimia kubwa tunafanya na nchi za Ulaya, siyo Amerika, kwani Benki Kuu haitambui hili?Kwa nini tuna-*peg* shilingi katika dola ya Marekani? Tungeelezwa kwa nini Benki Kuu haibadilishi vipimo hivi. Kwa sababu hasara tunayopata ni kubwa sana.

Lingine ambalo nataka nilisemee kwa haraka Mheshimiwa Naibu Spika, ni hili la mkataba wetu wa Afrika Mashariki kwa kuanzia na Mkataba wa Ushuru wa Forodha baadaye Soko la pamoja. Mimi sijawahi kushiriki katika mjadala huu. Lakini Serikali ya Kenya inaongozwa na wale wale ambao walikuwapo wakati tunavunja Jumuiya ya Afrika Mashariki na ni wale wale ambao katika mashauriano yanayoendelea sasa kule

Nairobi ambao walikuwa wameruhusu kihalali na Serikali yao kwamba dhahabu, almasi zichukuliwe Tanzania na nchi zingine zipelekwe Kenya halafu Kenya ijifanye ndiyo inauza dhahabu na almasi hiyo kana kwamba zimechimbwa nchini Kenya.

Sasa wengi wa hawa ndiyo wanaongoza Serikali, je, wamebadilika? Tuna takwimu za biashara yetu na Kenya? Wameacha magendo? Kwa sababu kazi hii ya kuunganisha soko la pamoja ni ngumu sana. Na ishara ni uchaguzi wa Jumuiya ya Ulaya juzi na jana jinsi ambavyo vyama vinavyotawala kule vilivyoshindwa. Kwa sababu wanajua, wananchi hasa wanajua kunatokea nini katika jamii.

Sasa hivi hatunajui kinachotokea mipakani, kuna biashara, na takwimu halali ambazo tunafanya na Kenya? Dhahabu yetu haipiti kwa kimagendo, ng'ombe hawapiti? Vyakula, mahindi, maharage, bila takwimu zozote?

Mwisho kabisa Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilisemee la mwisho. Hii Bajeti ni ya mkulima na mimi nakubaliana nayo. Lakini mkulima tunayemwongelea kwa Kiingereza anaitwa peasant, yule mdogo sana. Mwaka huu mkulima huyu kama amelima mahindi amepata mazao mengi sana. Lakini hawezi kufikia popote kwa sababu kuna magonjwa mengi sana ya wadudu waharibifu.

Dumuzi kwa mfano, katika eneo ninalotoka mimi wataharibu zaidi ya asilimia 70 kabla ya Desemba wasipouza haraka watauza kwa bei rahisi sana kwa nchi jirani kwa gunia shilingi 6,000/= na wao baadaye watatuuza shilingi elfu 30.

Dawa ya *acletic* ya kuua dumuzi kikiletwa pale haifanyi kazi. Hili limeshindikana kweli? Hatuwezi kujiwekea Bajeti, dawa ya kuua wadudu waharibifu wa mimea hasa dawa ambayo itatuwezesha kuhifadhi mahindi yetu ikipatikana.

Mwisho Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai tena kwa mara nyingine kwa sababu Bajeti hii itategemea sana *The Public Procurement Act, 2001.* Naomba ile Semina yetu ya tathmini ifanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABDULA S. LUTAVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru lakini nianze kwa kutoa salaamu zangu za pole kwa Ndugu zetu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kumpoteza mpenzi, mzazi wao baba. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awape subira hawa wafiwa na ampe makazi mema marehemu huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii na mimi niwapongeze ndugu zetu Wabunge ambao tuliwachugua hapa watuwakilishe katika Bunge la Afrika. Lakini hasa nizidishe pongezi hizi kwa Mheshimiwa Balozi Mongella, kwa heshima kubwa aliyoipata kule na akaileta ndani ya nchi yetu hii ya kuchaguliwa kuwa Rais wa kwanza wa Bunge hili la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii nimpongeze Ndugu yetu Danhi Makanga, kwa sababu mbili. Amerudi kundini na amerejea Bungeni kwa kishindo kikubwa sana. Nakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii kuhusiana na Bajeti na mpango huu niipongeze sana Serikali, niwapongeze Mawaziri hawa ndugu zetu, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Manaibu Waziri, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu na Mheshimiwa Dr. Festus Bulugu Limbu, pamoja na Watendaji kwenye Wizara hii na mahala pengine popote ambapo wamesaidia kwanza kusimamia utekelezaji wa mpango na Bajeti kwa mwaka huu uliotufikisha hapa, tunapoangalia sasa mwelekeo wa maendeleo ya nchi yetu kwa kutumia Dira hii ya Mpango na Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema mpango huu na Bajeti hii nia ni kutekeleza mkakati wa kupunguza umaskini na kuendeleza mafanikio ya uchumi, huu uchumi jumla yaliyopatikana hadi sasa. Mimi nataka kusema kwa moyo mweupe kabisa kwamba tunafanikiwa kwenye hili na nataka kuchukua nafasi hii niipongeze sana Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia kwamba Bajeti yetu ina utamaduni kuwa tegemezi sana. Jitihada ambayo imewekwa kwa miaka hii miwili, mitatu iliyopita imeonyesha ya kwamba tunapiga hatua kwenye jambo hili la uchumi. Mwaka wa 2002 kama inavyojionyesha kwenye maelezo hayo yaliyotolewa hapa ndani ya Bunge inaonyesha kwamba Bajeti yetu ilikuwa tegemezi lakini kwa kiwango kikubwa cha asilimia 47 kwamba kiwango cha asilimia 47 ya Bajeti yetu ilikuwa inachangiwa na ufadhili na uhisani kwa watu wa nje.

Lakini tulisema tumeazimia kupigana na hili na mwaka wa 2003/2004 tunasema tumefanikiwa kuishusha ile hadi asilimia 45. Sasa tunalenga kufika asilimia 41 tu ya utegemezi wa Bajeti hii. Nataka kusema kwa mwelekeo huu hakuna sababu ya sisi kuwa na wasiwasi kwamba na hili nalo pamoja na matatizo yanayojitokeza hapa na pale tunaweza tukalifikia lengo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti hii kama tunavyosema inalenga kupambana na umaskini na umaskini kwenye nchi hii uko kwa wananchi hawa wa kawaida. Umaskini kwa kifupi tunaweza kusema uko kwenye kilimo. Sasa kama tunalenga kupunguza *inflation* kama tunalenga kupunguza sijui upandaji wa bei kwa namna nyingine yoyote, lakini tunasema haya tunataka matokeo yake iwe kwamba yanamnufaisha huyu mkulima au mtu wa kawaida katika wale wanaotakiwa kunufaika na matokeo ya mipango na Bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiendelea kuiangalia unakuta kwamba kilimo kimekuwa tunakiita sekta kiongozi. Na mengi yanayotokea sasa hivi yanaonyesha kwamba kweli sekta kiongozi ni kilimo. Kwa sababu kama hatukuweka mkazo kwenye kilimo, basi athari kidogo ikijitokeza kwenye kilimo basi tunapigwa mahali pengi sana kwenye uendeshaji wa uchumi wetu.

Hapa taarifa tuliyoipata kwa sababu tu mwaka jana kulitokea ukame, basi kilimo tulilenga kikue kwa asilimia 5. Imeshindikana kimekuwa kwa asilimia nne tu imepungua asilimia 1 tu kwenye lengo letu. Lakini matokeo yake yamekuwa kwamba tumeshuka kwenye pato la Taifa. Malengo yetu hayakufikiwa, yametelemka badala ya kufikia pale tulipotegemea. Hata mapato yetu kwa maana ya *foreign reserves* pia yameshuka.

Sasa hii inatuambia kwamba kama tunataka kufanya lolote basi tunatafuta, kama tunataka ukuaji wa uchumi wetu basi uchumi wetu unatakiwa ukue kwenye eneo ambalo linawagusa wengi. Na mimi kwa mtazamo wangu eneo linalowagusa wengi ni kilimo.

Leo tunazungumza hapa kwamba pamoja na matokeo haya ya uchumi kwa miaka hii miwili mitatu iliyopita, tunalenga kwamba *inflation* yaani ukuaji yaani upandaji wa bei tuiache kwenye asilimia nne kwa mwaka 2005. Tunataka mapato ya ndani yafikie asilimia 13.8 ya pato la Taifa. Tunataka *foreign reserves* zituwezeshe sisi kukidhi mahitaji yetu ya bidhaa kutoka nje miezi sita. Tunasema tunazungumzia ukuwaji wa *GDP* tunaitaka uongezeke kufikia asilimia 6.3 ifikapo mwaka 2005.

Lakini tunasema kwamba haya yote yanategemea sasa kupatikane ukuaji katika *agriculture,* ukuaji katika *industrial production* na ukuaji katika *exports.* Sasa hivi vitu vyote vitatu tunavyovisema ndiyo misingi ya sisi kufanikiwa hili, yote hii iko kwenye kilimo.

Sasa na mimi nikiangalia kilimo hiki tunachokizungumza kwamba kinaajiri ya zaidi ya asilimia 85 ya wananchi wetu. Kinazalisha zaidi ya nusu ya pato la Taifa. Na nadhani kinachangia kwa kiwango kikubwa mapato yetu ya fedha za kigeni.

Hiki ndicho kinachotakiwa tukipe kipaumbele maana tunapozungumzia *growth* ya uchumi labda tuwe tunasema tunalenga kupata, wanaita *pro-poverty growth* na *pro-poverty growth* ni ile *growth* ambayo itatokana na kilimo kuwa chenyewe kuwa kimetiliwa mkazo mpaka kinawezeshwa kukua kwa kiwango ambacho kinaweza kikasukuma ukuaji mzima wa jumla wa uchumi wa nchi yetu hii.

Kwa hiyo, nilikuwa nataka nishauri kwamba kama tunataka kufanikiwa kwenye kilimo lazima tukiweke mbele kwa namna yoyote ile. Kwa sababu mwaka tulipopata tatizo hili la ukame hapa Waziri wa Nchi, anasema Serikali ilibidi ichukue hatua za haraka za dharura hapa.

Wanasema wametoa jumla ya shilingi bilioni 2 kwa ajili ya kufidia sehemu ya gharama ya usafirishaji. Asema wamefanya habari ya ukarabati wa vituo 17 vya utafiti. Wamesema wameongeza uwezo wa Mfuko wa Taifa wa pembejeo. Vitu hivi vyote vimefanyika kwenye eneo la kilimo na imani ni kwamba kwa sababu tumefanya haya basi athari kwenye uchumi itapungua kuliko kama tusingechukua hatua hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa nasema ili kuonyesha kwamba kilimo kina umuhimu wake na umuhimu lazima ujionyeshe kwenye mipango hii ambayo sisi tunaiweka hapa kwa mwaka huu na miaka ijayo. *(Makofi)*

Nilikuwa nazungumzia kwamba haya tuliyoyafanya kama *crisis management* kwenye kilimo mwaka huu kwa sababu ya ukame, basi tuyatengenezee utaratibu wa uendelevu ili iwe sehemu ya maendeleo ya shughuli mzima ya kilimo kwenye uchumi wetu ili uchumi wetu ambao umeegemea sana kwenye kilimo usiwe unaathirika kwa kukwaruzwa tu kama ilivyotokea ukame huu ulivyotuathiri katika kipindi hiki cha msimu uliyopita.

La pili kwenye kilimo, Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasema ili tuonyeshe kwamba kweli tuna nia ya kuendelea kwa kutumia kilimo basi *agro-procesing* lazima itiliwe mkazo. Viwanda hivi vinavyohusiana na mali hizi za asilia, pamba, korosho na vitu vingine vyote ni lazima tuhakikishe kwamba vitu hivi haviendelei kupelekwa ghafi katika nchi za nje. Tunapoteza mali nyingi. Tunapoteza fedha nyingi kwa sababu tunaendelea kupeleka ghafi. Tunachotaka ni kwamba pamba isiende pamba, tunataka ziende nguo, ziende *fabrics* na kadhalika.

Tunataka korosho isiende korosho tena ghafi, tunataka ziende *kernels* zile zikazoe pesa kule zilete nchini hapa. Samaki hatutaki tupeleke minofu ile tupeleke angalau iko *canned* vitu kama hivyo. Lakini humu ndani ukisoma sana unakuta hivi vitu havikutiliwa mkazo sana. Sasa haya sijui tunangoja mpaka baada ya miaka mitano kutoka leo au bado tunaendelea nayo. Lakini hayajionyeshi sana kwamba tumedhamiria kufanya jambo hili kama namna ya kujikwamua.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa najaribu kushauri kwamba kilimo lazima tukipe kipaumbele tuweze ku-*raise volume* na *value* ya mazao yenyewe ya kilimo haya ili angalau kwamba mimi sioni kabisa, leo tunazungumza habari ya *exports* kwamba imeongezeka lakini kilichosababisha nyongeza nyingi kwenye *export* *ni none traditional exports.*

Mimi sioni hata dhambi kwamba hizi *traditional exports* yangeendelea kuwa yanaongoza katika kutupatia pesa za kigeni kwa sababu kama tungelikuwa tuna kiwango kidogo cha *traditional exports* zinakwenda *raw* kwa sababu hatujamaliza kuhakikisha kwamba yote tunaweza kuya-*process* hapa hapa, basi na zile *processed products* za *agriculture* zikaenda. Basi tujue tutapata mapato makubwa sana kuliko kama tunavyoendelea sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumzie habari ya madini kidogo. Nilikuwa nataka niseme hivi kwamba madini ni sekta ambayo inakuwa kwa kasi kubwa sana. Mwaka huu tunazungumzia imekuwa kwa asilimia 17. Lakini nashangaa sana ukitazama takwimu zilizoko kwenye vitabu hivi tunaelezwa kwamba karibu nusu ya thamani ya bidhaa zilizouzwa nje, dola milioni 1,142 karibu nusu yake inatokana na *exports* za madini. Lakini mchango wa madini katika pato la Taifa ni asilimia 3 tu. Nazungumzia thamani ya mazao yaliyouzwa nje, siyo mapato yanayotokana na madini,

ahaa! Thamani ya mazao yaliyouzwa nje yakiwemo madini. Madini yanachangia dola 548 milioni hii ni karibu nusu ya mapato yote.

Lakini nina hakika kabisa kwamba inachangia asilimia 3 tu kwa sababu thamani hii siyo mapato kwa Taifa. Sasa nilikuwa nataka kushauri kwamba lazima ufanyike utaratibu hapa ambao utatuhakikishia, maana yake sisi lazima tujue kwamba kwa madini haya sisi Watanzania na nchi hii Tanzania ndiyo wamiliki asilia wa madini yaliyoko ndani ya ardhi hii.

Kwa hiyo, mtu akija na ufundi, akija na teknolojia, akija na uzoefu wake, akaja na *capital* yake basi akija hapa lazima ajue kwamba anakuja kwenye madini ambayo tayari yanamilikiwa. Lakini inaonekana kwamba kwa sababu wakati ule tulikuwa tuna tatizo la kuweza ku- hii mikataba na kuwapata watu ambao wanaweza kuja kufanya kazi hiyo. Labda tulikuwa tunawapa tu.

Lakini kwa utaratibu huu unaonekana kwamba thamani ni karibu nusu ya *exports* zote ndiyo tutapata asilimia 3 tu maana yake mimi ni kwamba tumetoa madini haya kwa watu wote waliokuja hapo kuja kuchimba madini kama vile tulikuwa tunaona madini haya ni ghasia na kwa hiyo kama wamekuja kuja kuchimba basi wanatuondolea ghasia hii. Ninadhani mtazamo huu si sahihi.

Lazima zichukuliwe hatua tuhakikishe kwamba sisi tunapata maslahi kama nchi kutokana na madini haya, kama suala tatizo ni mikataba, basi mikataba hii lazima ifanyiwe marekebisho mara moja. Kama suala ni Sheria basi ziletwe hapa Sheria hizo na tuzifanyie marekebisho. Kama ni suala la Sera na Taratibu basi na zibadilishwe mara moja ili mradi iwe maslahi ya nchi hii kutokana na madini tuyapate kama tunavyohitaji. *(Makofi)*

Nafarijika sana Mheshimiwa Naibu Spika, kusikia kwamba imeundwa Tume kwa ajili ya suala hili. Nategemea kwamba Tume itatufunulia mambo mengi na itatuwezesha sisi kufika mahala tukafanya marekebisho tunayohitaji katika jambo hili. Mimi kwa bahati mzuri au mbaya siyo miongoni mwa wale wanaohoji eti kwa nini yule Mwenyekiti wa ile Tume ni mmoja ya wale waliowahi kuwa Makatibu Wakuu kwenye Wizara tunayoihoji. Mimi sio miongoni mwao. Nategemea kwamba yeye ameteuliwa kuwa Mwenyekiti wa ile Tume kwa sababu ya uadilifu wake na nategemea uadilifu huo ndiyo utakaojitokeza kwenye ripoti ambayo ataiandika na *findings* zake kama atakavyotoa yeye kama Mwenyekiti na Tume yake na Wajumbe wake wote. *(Makofi)*

Nategemea na namwombea Mwenyezi Mungu awasaidie waje na ripoti hapa ambayo itatusaidia sisi katika kutazama upya mikataba hii na Sheria zetu na taratibu zetu ambazo zinahusu madini ili na sisi kama Taifa tupate kuneemeka na tupate kunufaika na matokeo ya uchimbaji na *processing* ya madini ndani ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo mawili tu. Nilikuwa nataka nichukue nafasi hii tena kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni yangu ndani ya Bunge hili. Lakini nimalizie kwa kusema hoja hii iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri

wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, naunga mkono mia kwa mia. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja mbili zilizo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa msiba walioupata. Vile vile nitoe pole kwa Waheshimiwa Wabunge waliopata matatizo walipokuwa njiani kuja katika kikao hiki cha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema kwamba naunga mkono hoja zote mbili mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa sababu siku zilizopita Mheshimiwa Waziri wa Fedha tulikuwa na hoja ya wastaafu na aliahidi kwamba tuiachie Serikali ilifanyie kazi na kwa kweli Serikali imelifanyia kazi na katika Bajeti hii imetamka kwamba wale wote waliolipwa kwa mkupuo sasa watarejeshwa kwenye Daftari la Pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tahadhari tu katika utaratibu wa kurejesha katika Daftari la Pensheni. Tumeanza kupokea malalamiko kwamba taratibu zilizotolewa ambazo ni lazima zifuatwe ili kumrejesha kila mtu kwenye Daftari la Pensheni inaonekana kwa njia moja au nyingine baadhi ya wastaafu walishapoteza baadhi ya nyaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, siamini kama Serikali haina takwimu zozote zinazohusu wastaafu. Serikali ikisisitiza kwamba kwa yeyote aliyepoteza nyaraka hatarejeshwa kwenye Daftari la Pensheni itakuwa sio sahihi kwa sababu natarajia Serikali inapowaambia wastaafu watoe nyaraka lazima baadaye inazo *documents* ambazo inatumia kulinganisha kuona je hizi nyaraka alizotoa huyu mstaafu na hizi *documents* tulizo nazo Serikalini ni sahihi? Kama hivyo ndivyo ilivyo hata kama mstaafu kwa bahati mbaya alipoteza nyaraka sio busara Serikali kutumia nafasi hiyo kuamua kutomrejesha katika Daftari la Pensheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo napenda nichangie ni ya Walimu. Imejitokeza katika maeneo mengi lakini napenda nitoe mifano ya Walimu watatu tu.

Katika Jimbo langu na Jimbo la Bukoba Vijijini kwa Mheshimiwa Nazir Karamagi, jumla ya Walimu 210 wanadai nyongeza ya mishahara yao ambapo walipopandishwa madaraja hawakulipwa.

Nitatoa mifano ya Walimu watatu tu kama kielelezo cha ushahidi. Mwalimu mmoja anaitwa Mwalimu Erasto Kishura, yeye anadai nyongeza ya mishahara ya miezi 89. Kwa maana hiyo kwa zaidi ya miaka 13 na miezi minne amekuwa akipandishwa cheo lakini hajawahi kulipwa hata shilingi. Mwalimu mwingine anaitwa Mwalimu Severine Mwenge na yeye vile vile anadai nyongeza ya mishahara ya miezi 89 na mwingine

anaitwa Mwalimu Julius Boniface, huyu anafundisha Shule ya Msingi Bubale na yeye anadai nyongeza ya mshahara ya miaka 13 na miezi miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapokuwa na Walimu wanaokuwa katika mazingira magumu ambapo mishahara yenyewe ni midogo, unamwongezea mshahara lakini inachukua miaka 13 hajapata nyongeza ya mshahara huo, nadhani hiyo sio haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika Bajeti yake amesema kwamba hilo atalifanyia kazi na ni matarajio yangu sio mbinu ya kutaka tupitishe Bajeti yake halafu baadaye tukishapitisha aweke mikono mfukoni. Tutaendelea kuomba Mwenyezi Mungu tuendelee kuwepo ili tutakapokuwa tunajadili Bajeti ijayo tuhoji ni kwa kiasi gani atakuwa ameondoa tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hoja zimejitokeza za kupanda kwa bei ya vitu mbalimbali. Katika eneo langu sukari imepanda kutoka zaidi ya shilingi 500 kwa kilo mpaka zaidi ya shilingi 1,000 kwa kilo, wananchi wanauliza kulikoni? Zipo sababu zinazotolewa mojawapo ni kupanda kwa gharama za uzalishaji na nyingine ikiwa ni kupanda kwa bei ya petroli. Lakini mimi nimekuwa nikijiuliza hii bei ya petroli ni sawa imepanda katika Soko la Dunia lakini je, yako mambo yaliyo ndani ya uwezo wetu ambayo tunaweza kuyafanya? Nimegundua lipo jambo ambalo tunaweza kulifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye ukurasa wa 10 anatoa pongezi kwamba anafurahi kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba hatua zilizochukuliwa kudhibiti ukwepaji wa kodi katika biashara ya mafuta ya petroli zimezaa matunda yaliyotarajiwa, anaeleza kwamba bilioni 226,036 zilikusanywa kwa kipindi cha mwaka 2003 hadi 2004 na anaeleza kwamba hiyo ni zaidi ya lengo ukilinganisha na kipindi kama hicho kilichopita kwa zaidi ya 25% yaani wamekusanya bilioni 18 zaidi ya zile ambazo wangekusanya. Hapa Mheshimiwa Waziri amefurahi na amepongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti tunatoa idhini ya kukusanya kiasi fulani na kutumia kiasi fulani kwa hiyo, unapokusanya sana kuliko kile tulichokuruhusu ukusanye ni tatizo, unaweza kuadhibiwa kwa hilo wakati mwingine. Kwa sababu gani ni tatizo? Nitatoa mfano mdogo tu ili hesabu hii ieleweke kwa kila mtu. Kama ukiwa unatoza 10% ya shilingi 100 kwa kitu chochote maana yake utakusanya shilingi 10 lakini ikitokea thamani ya kitu hicho ikapanda ikawa shilingi 200 ukaendelea kutoza 10% maana yake utakusanya shilingi 20.

Kwa hiyo, bei ya mafuta ilipopanda katika Soko la Dunia na sisi tukaendelea kutoza kodi viwango vile vile tulivyopitisha wakati tunafikiria bei itaendelea kuwa ile ile ni wazi kabisa kwa hesabu za mtoto wa Darasa la Kwanza kwamba lazima fedha zitakusanywa nyingi zaidi katika mafuta, iko wazi kabisa. Lakini madhara yake ni kupanda kwa gharama za uzalishaji na baadaye bei za sukari zinapanda, nauli zinapanda, *TANESCO* wanapandisha bei za umeme lakini kumbe tungeweza kulikerebisha hilo kwa kuwa na utaratibu wa kodi ambao ni *flexible* kwamba *in case* inatokea bei ya vile vitu

katika Soko la Dunia inapanda basi sisi tunaweza kurekebisha *percentage* zetu na tukaendelea kukusanya fedha ile ile ili tusilete madhara katika uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni ushauri wangu niombe wataalam walitazame hilo. Pia naomba nitofautiane na Mheshimiwa Waziri kwa pongezi alizotoa hapa kwamba kukusanya fedha nyingi zaidi kwenye mafuta ni kwa sababu ya kuboresha mianya ya kukwepa kodi bali hii ni matokeo ya kukusanya fedha nyingi zaidi ambazo hazikutakiwa kukusanywa ili kutoleta madhara katika uchumi. Nashauri walitazame suala hilo waone tunaweza kufanya nini ili kurekebisha hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine inayopelekea bei ya vitu kupanda ni kuendelea kushuka kwa thamani ya shilingi siku hadi siku. Kama thamani ya shilingi inashuka siku hadi siku maana yake wananchi itabidi watumie fedha nyingi zaidi kununua kile kile kwa sababu zile bidhaa unazinunua au unaziingiza nchini kwa kutumia fedha za kigeni. Sasa wataalam wetu wa Benki Kuu wana lugha nzuri wanasema kwamba bado pesa iko kwenye mkondo wake, shilingi bado iko kwenye mkondo wake wa kuendelea kushuka kwa hiyo, hawana wasiwasi sijui huo mkondo utaenda mpaka wapi, huo ndio wasiwasi wangu wao wanafahamu lakini mimi sijui.

Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuwa anajibu hoja atueleze huo mkondo wa shilingi kuendelea kushuka ambao unafanya Waziri wa Fedha asiwe na wasiwasi, wataalam *BOT* wasiwe na wasiwasi ni mpaka lini watakapoanza kuwa na wasiwasi, ningependa nijue hilo. Ni mpaka itakapofikia dola moja shilingi 2000, shilingi 10,000 maana naona wanakuwa *very comfortable* wanasema *the shilling is taking its own course.* Hawa wataalam wetu kama wanasema *it is taking its own course* lakini huku bei zinaendelea kupanda na tunaendelea kushindwa kutoa majibu nakuwa na wasiwasi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji ametoa hoja kwa kusema kwamba thamani ya shilingi inaporomoka na akasema sababu kubwa tunaagiza sana vitu kutoka nje kuliko tunavyopeleka vitu nje. Nakubaliana naye lakini hoja inafuata je ni kitu gani tunachoagiza sana nje maana unaweza kuwa unaagiza sana nje lakini unaagiza vitu ambavyo labda kulikuwa hakuna sababu ya kuviagiza na kwa sababu hiyo utaendelea kuwa na matatizo kama wewe unaagiza, unaagiza, unaagiza shilingi inaendelea kuporomoka na unakuja hapa unasema tunaagiza tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Nkenge maeneo yote ya vijijini nimepokea malalamiko, ziko dawa fulani Waziri amesema sio dawa za kulevya lakini wananchi wa vijijini wanasema ni dawa za kulevya kwa sababu ukionja kidogo basi wewe ama utatembea ukiwa uchi ama utaanza kucheza ngoma ambayo haieleweki. Huko Zanzibar kuna shule moja wanafunzi walionja wote wakavua nguo wakawa wanafanya mambo ambayo siwezi kuyazungumzia ndani ya Bunge hili.

Wananchi walipokuwa wakinieleza nikafikiri wanatania kwenye mkutano mmoja nikawaambia basi mninunulie mniletee hapo hapo wakaniletea na nikasema nitampelekea

Mheshimiwa Naibu Spika na yeye aonje aweze kushuhudia. Kwa hiyo, nimekuja nayo Mheshimiwa Naibu Spika hii ni zawadi yako toka Jimbo la Nkenge. Hii inaitwa Kuba. *(Kicheko)*

*(Hapa dawa husika ilionyeshwa mbele ya Bunge)*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kinachonifurahisha hapa sio kile ambacho mimi nafikiria kama Mbunge lakini ni kile ambacho wananchi wangu wananituma. Wananchi wangu wamenituma wasingependa hizi dawa ziendelee kuuzwa kwenye maduka. Hicho ndicho walichonituma na ndicho ninakisema hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Mipango...

**NAIBU SPIKA:** Mimi nikiipata nitampelekea Waziri wa Fedha, ukiniletea nitampelekea Waziri wa Fedha. *(Kicheko)*

**MHE. DR. DIODORUS B. KAMALA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu hapa ni kwamba unapokuwa na hoja huku shilingi inaporomoka unasema kwamba ni kwa sababu unaagiza bidhaa nyingi zaidi na huku una dawa za kulevya ambazo tunatumia fedha hizo hizo za kigeni kuendelea kuziagiza ndio maana nahoji ni bidhaa zipi hizi tunazoendelea kuagiza na shilingi yetu ikaanza kuporomoka. Sasa hiki ni kimoja na huenda kuna vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wananchi wangu wanauliza je, Serikali ya CCM ni kweli imeamua dawa hizi ziendelee kuuzwa? Mimi nimelifikisha mahali pake nadhani kazi yangu imemalizika, Serikali ipo na imesikia na nitashukuru nikipata majibu ili niweze kuwaelezea wananchi wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho hili tumeliongelea muda mrefu ni *STABEX.* Mwaka 2001 nilikuwa na hoja nyingi za ushirika na wakati mwingine nilikuwa naongea kwa hasira lakini sasa hivi sina sababu maana mambo mengi yamerekebishwa tunasema *Alhamdulilah. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado kuna hili dogo tu la *STABEX.* Serikali nzima hakuna anayetaka kutoa majibu sahihi. Ukimuuliza Waziri wa Fedha anasema fedha amepeleka kilimo, Waziri wa Kilimo ukimwuliza anasema amepeleka kwa Mheshimiwa wa barabara, Mheshimiwa wa barabara anasema hajaziona, Mheshimiwa *Sir* George, siku hizi amekaa kimya wala hataki kuziulizia tena. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali yote kwamba sio vizuri Mawaziri kutoka Serikali moja kila mtu anatoka na maoni yake. Nawashauri wakae tu na kama hawatakuwa na uwezo wa kukaa mimi nitawawezesha kuwaweka pamoja ili walau wawe na neno moja kuhusu *STABEX* ili na sisi tupate cha kuwaambia wananchi, tunachotaka ni msimamo wa Serikali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kusema hayo ndio machache niliyotumwa kusema na naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nitoe mchango wangu mfupi kwa hotuba hizi mbili ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na ile ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2004/2005 na mwelekeo wa mipango na maendeleo kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nami nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi jioni hii ili niweze kutoa mchango wangu. Pia napenda kuchukua nafasi hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na dada yake Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kufiwa na mzazi wao pamoja na wale Wabunge ambao hivi karibuni wamepata matatizo mbalimbali ya ajali.

Pamoja na pongezi hizi kwa kweli hotuba hizi mbili za Mawaziri hawa wawili safari hii sipigi sana kelele ni nzuri maana yake zina mwelekeo mzuri wa kujenga uchumi wa nchi yetu na hasa kuwafanya wananchi waishi vizuri zaidi ili waweze kutekeleza majukumu mbalimbali waliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau, niwapongeze wale Wabunge waliokwenda Bunge la Afrika. Pongezi za pekee ziende kwa Mheshimiwa Getrude Mongella ambaye amechaguliwa kuwa Rais na pia sifa zije kwa sisi Wabunge binafsi wote tuliomchagua Bunge la Tanzania, nchi yetu na wananchi kwa ujumla kwa kumpa Urais wa Bunge la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kuchaguliwa kuja kambi yetu ya CCM, karibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kutuwakilisha kwenye Jumuiya ya *SADC. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 16, kifungu cha 30 kuna maneno ya ukuzaji wa sekta binafsi na uwekezaji. Kuna maneno pale wanasema kukiwezesha kituo cha *TIC* na uwekezaji kuongeza ufanisi katika kuboresha mazingira ya uwekezaji. Naona kwa maneno yale ni vema vile vile tukasema lakini pia ni vema kuangalia maslahi bora ya Taifa *vis-à-vis* uwekezaji maana kukiwa na malalamiko upande mwingine wa wananchi sio jambo zuri na hili nafikiri Mawaziri hawa wawili ni makini watakuwa wanalielewa hivyo wanafuatilia kwa karibu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazipongeza tena Wizara hizi kwa kuwawezesha wawekezaji wa ndani na wa nje pia kwa ongezeko la mtaji wa kigeni *(foreign direct investment)* iliyofikiwa dola 300 toka 240.4 mwaka 2002 mpaka hivi sasa. Haya yanaonyesha ni jinsi gani hawa Mawaziri wanafanya kazi yao au uchumi wa nchi unakwendaje kwa ujumla. Hii pia imewezesha kutoa ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu unakuja juu ya ajira hizi za wawekezaji kama kanuni zile za kazi zinafuatwa mfano wafanyakazi kufanya kazi kwa saa ambazo zinakubalika. Sehemu nyingi imeonekana hawa wawekezaji wanawatumikisha sana wafanyakazi mtu anaingia asubuhi saa moja na nusu anatoka saa moja asubuhi kwenda nyumbani. Bila shaka Wizara inayohusika italiangalia hilo. Ni jambo zuri ume-*invest* kwetu lakini angalia pia afya ya wananchi wetu sio uwafanyishe kazi kupita kiasi kama kuna *shift* basi Ipungwe vizuri za kuwawezesha wapumzike siku mbalimbali. Hili bila shaka Wabunge mmelisikia na malalamiko yako mengi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kuanzishwa kwa Benki ya Kilimo, natofautiana na mwenzangu anayesema tuvunje Benki moja iwe ndio Benki ya Kilimo. Bila shaka Mheshimiwa Basil Mramba na mwenzake ni makini wataangalia suala hili vizuri zaidi ili Benki hii iwe mpya na iwe na mtazamo ambao tumeona tuanzishe ili kuhakikisha kuwa sekta ya kilimo pamoja na viwanda inasaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itashirikiana na wadau wengi na inaendeleza mfumo mpya wa utekelezaji wa sekta ya afya pamoja na ukarabati wa taasisi za afya zikiwemo hospitali ya Muhimbili na zile za Wilaya pia ongezeko la upatikanaji wa dawa za chanjo mbalimbali kama vile Kifaduro, Suria, Polio na Pepopunda.

Mimi nasema tuna ongezeko la watu sasa hivi tumefikia milioni 34 kama hatatuongeza vituo vya afya maeneo mengi wananchi watakuwa hawapati huduma nzuri au watakuwa wanalala vitanda vilivyo karibu zaidi kwa sababu vituo vya afya vingi vilijengwa siku nyingi. Kama kule kwangu kule nina kituo cha Mbuyuni nilishaleta swali hapa nikajibiwa kuwa kuna vigezo ambavyo vinatumika katika uanzishaji wake lakini ongezeko nalo? Kama vituo vile vilijengwa siku nyingi kwa nini kusiwe na umakini wa kuangalia upya jinsi gani tunaweza kuongeza vituo hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna jitihada za kupambana na magonjwa mbalimbali ikiwemo Malaria na pia misaada ya virutubisho vya virusi vya Ukimwi. Najiuliza je, kweli kutakuwepo na mpango mzuri wa kupeleka hizi dawa kule vijijini kwa sababu huduma nyingi zimeonekana zikiishia mjini.

Naomba Serikali iangalie kwa makini zaidi kuhakikisha hata wale wa vijijini ndani kabisa kusikopitika wapelekewe huduma hizo ili kuondokana na matatizo mbalimbali ambayo yamejitokeza. Ukifika maeneo hayo utakuta vitu kama *condom* au vitu muhimu ambavyo vingetumika kuzuia ugonjwa huu wa Ukimwi havifiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile ningependa kuongelea uwiano mzuri wa kugawana mapato ya Taifa. Yapo maeneo mbalimbali nchini yamekuwa *neglected,* ni visiwa. Ukiangalia eneo langu lile la katikati la Mpanda, Sikonge, Chunya, Sumbawanga, Kigoma, Itigi hakuna kinachoendelea pale na nilishawahi kusema hapa kuwa hivi watu hawa wanaofanya mipango hawaangalii maeneo kama haya, hakuna *infrastructure* yoyote kule. Hata barabara ile ya kutoka Mbalizi - Mkwajuni, Saza - Gua

- Mpanda ingeweza kurahisha au kuondoa matatizo ya usafiri. Mheshimiwa Basil Mramba anajua vile kwa sababu kule Ngwara ali-*introduce* zao la kahawa sasa Kahawa iko kule na kule kunajulikana kwa ulimaji wa tumbaku kwa wingi, barabara ni mbovu sana.

Eneo lingine ambalo liko kama kisiwa ni lile ambalo kila siku nauliza swali hapa barabara ya Galula - Namkukwe - Kamsamba - Sumbawanga. Sisi tumekazania zile barabara ambazo ziliwekwa na Wakoloni hizi barabara nyingine tumezisahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda naomba uimarishe kile Chuo cha Mipango ambacho kipo hapa Dodoma, mipango kule Wilayani bado haiendi, inalegalega au wanaoajiriwa Mikoani na Wilayani wangeweza kuwa wazuri zaidi kama wangekuwa wanatoka katika Chuo kile ambacho kipo hapa. Naelewa kina matatizo mbalimbali wewe unajua zaidi naomba sana kama kisaidiwe ili vijana wetu au Maafisa wale wa chini zaidi *VEO, WEO* wakapewa programu ya kuja kusoma na kuhakikisha wanafanya kazi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza *TRA* kama nilivyosema mambo mengine haturudii lakini kule Chunya naomba tupatiwe gari kwa sababu bila gari huwezi kuzunguka Wilaya ile na ukakusanya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina matatizo kidogo na Wizara ya Nishati na Madini waliniletea nguzo karibu miaka nane iliyopita na sasa mimi namaliza Ubunge sijui nguzo hizo zitawekwa lini. Nawaomba wakumbuke zile nguzo zinatakiwa ziingie kwenye mashimo walau Songwe tukawasha umeme kabla ya mwaka 2005. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kutuletea simu pale Chunya lakini Waziri kumbuka yako maeneo ambayo bado hatuna simu kwa mfano Makongorosi na Mkwajuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tupewe Wilaya kule Jimbo la Songwe pale Mkwajuni, *infrastructure* ni nzuri tu tulishajenga majengo na hizi huduma za simu na mengineyo ndio maana tunaziomba ili tuweze kuwa na Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau, napenda kumshukuru Waziri Edwrad Lowassa kwa visima vitano alivyonipatia lakini visima vile vimechimbwa tu bado sijapata pampu za kuweza kuviendesha. Naambiwa kuwa Wilaya labda ingeweza kusaidia lakini mara nyingi tumesema kuwa Wilaya hazina fedha za kutosha sasa ni jukumu ya Wizara hii kuangalia ni jinsi gani watafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo matatizo maeneo mengi ya visima nilishawapelekea barua ya kujieleza na nimeonana na watumishi wake wengine pengine kwenye Bajeti nitaona maeneo hayo ambayo nimeomba visima vichimbwe. Kuna maeneo *infrastructure* ya maji ilikuwepo lakini imeharibika inatakiwa itengenezwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hizi muhimu za Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Waziri wa Fedha, Mzee Basil Pesambili Mramba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa mchango wangu, naomba nichukue nafasi hii kutoa pole kwa familia ya rafiki yangu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na dada, Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na mzee wetu, mzee Omar Mohamed Kigoda. Kwa bahati nzuri mimi kwenye mazishi niliwakilisha Bunge kwa niaba yenu napenda niseme familia imefarijika sana kwa Waheshimiwa Wabunge baada ya kuelezea kwamba nimetumwa na Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo, nimewatolea salaam pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kupata ushindi wa kishindo kurudi katika Bunge. Mimi kama Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* nimefarijika kwa sababu huyo ndio Ronaldo wetu wa *Bunge Sports Club* kwa hiyo, kurudi kwake, kwangu ni faraja kwa sababu najua *center forward* wangu yupo, nafarijika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda pamoja na Mheshimiwa Basil Mramba kwa Bajeti nzuri ambayo wametuletea. Hawa hawa ndiyo waliotengeneza Bajeti ya mwaka uliopita na mwaka huu. Kwa kweli mimi nasema ni Bajeti ambayo imelenga na watu ambao wanaelewa tumetoka wapi, tuko wapi sasa na tunakwenda wapi.

Mimi nawapongeza kwa dhati kabisa wao pamoja na wataalam wote wa Wizara zote mbili kwa kazi nzuri ambazo wametufanyia. Duniani kote unapoongoza unapigana vita na maadui watatu, ujinga, maradhi na umaskini. Bajeti hii kwa kweli imelenga huko bila matatizo yoyote na mimi napenda niwapongeze kwa dhati kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nisisitize kitu ambacho kimeelezwa humu ambacho katika vile vipaumbele tulivyojiwekea sekta ya elimu tumeiwekea mkazo na mimi napenda niseme hivyo kwamba kwa kweli bado tuendelee kuipa sekta ya elimu umuhimu kwa sababu kama hukuelimisha wananchi wako wakawa wajinga hata hayo maradhi na umaskini hautaondoka.

Kwa hiyo, kwa kweli mimi napenda niipongeze kwamba msisitizo uendelee na mimi napenda nimwunge mkono Mheshimiwa Sophia Simba kwa kusema sasa ifikie mahali tuwe na *Universal Secondary Education,* haya mambo ya *primary education* sasa kwa kweli muda umepita. Kwa hiyo, juhudi hizo ziwekwe ili tuweze kuwa na watu ambao wanajua wanafanya nini. Aliyesoma atajua maradhi, umaskini na ataondoka navyo. Pia atalima vizuri, yote haya yatafutika na nchi zote duniani ambazo zimewekeza kwenye elimu haya yote tunayozungumza yameyeyuka. Kwa hiyo, naomba sana suala hilo tulitilie kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize kitu kimoja kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala ametoa mfano, mimi ninayo mifano lukuki

kwa kweli walimu wanaoajiriwa sasa mpaka wapate mishahara inachukua muda mrefu sana. Hebu tuwalipe hawa walimu, kwa kweli wanapata adha na wengine ni watoto wadogo, wanapata matatizo makubwa, wanakopa na wanaingia kwenye madimbwi ya matatizo.

Mimi naomba kwa kweli tulione hilo, tunauliza maswali kila siku hapa tunajibiwa suala hili lipo *Treasury,* liko Utumishi, hivi hamkai mkalimaliza! Naomba mlimalize hili tatizo ili walimu waweze kupata faraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kwenye Utawala Bora. Tunasema nchi yetu ni ya utawala wa sheria na demokrasia, lakini yapo matatizo makubwa sana kwenye Mahakama. Kuna kesi ambazo haziishi katika nchi hii, watu wanadhulumiwa, Mahakimu hakuna. Ukitazama katika hiki kitabu cha vipaumbele Mahakama ni sehemu ya kipaumbele ,lakini sijui kwa nini mpaka leo hii Mahakama ni chache mno, Mahakama zenyewe ni magofu mpaka leo. Sasa mimi naomba Serikali ione kama imetaka utawala bora basi lazima kuwa na haki, *justice delayed is justice denied,* ndivyo mnavyosema wenyewe, sasa kwa nini watu wanapata tabu?

Mimi nina mifano ya mtu mmoja ambaye ana kesi, yuko ndani kwa muda wa miaka saba sasa. Inatisha. Kila ninapokwenda kutembelea Magereza, nawaeleza lakini kesi haiishi. Sasa ni vizuri vitu kama hivi tuvirekebishe ili vituwekee heshima katika nchi yetu. Naomba suala la Mahakama litazamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika suala lingine ambalo wenzangu wamelizungumza, lakini halijaguswa sana. Zipo nchi katika dunia hii zinategemea bandari. Sisi tuna bandari kubwa tatu, tuna Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, tuzitumie basi hizi bandari kwa juhudi zetu zote, zitatuingizia kipato katika nchi yetu, lakini mpaka sasa bado hatujawekeza mkazo zaidi kwenye bandari. Kuna vitu ambavyo kidogo vinaleta dosari hasa katika bandari ya Tanga ambapo ningependa Mheshimiwa Waziri alione hilo. Bandari ya Tanga ni moja ya Bandari muhimu sana kwa sababu ingeweza kusaidia nchi ya Burundi, Rwanda na maeneo mengine badala ya watu kwenda Kenya wakapitia pale. Lakini kuna urasimu ambao ningeomba Mheshimiwa Waziri auchukue, kuna documents fulani ambazo lazima ziende Dar es Salaam ndiyo zirudishwe Tanga.

Sasa hili ni tatizo na naomba liyeyuke. Hicho ni kitu ambacho kinaweza kufanyika mara moja na bandari ile ikatupatia kipato kikubwa sana. Ni bandari ambayo watu wanaipenda kwa sababu inachukua muda mfupi, unaweza kukaa muda mrefu Dar es Salaam lakini Tanga ukakaa labda siku tatu au nne mzigo umetoka. Baadaye kukatokea mizengwe mizengwe ikaonekana kama ni bandari ya matatizo matatizo watu wakarudi Dar es Salaam.

Sasa naomba hilo lirekebishwe haraka sana inavyowezekana ili mambo yaende, tuweze kupata kipato na wengi waitumie bandari hiyo bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo nataka nilizungumze ni suala la kilimo. Wenzangu pia wamelizungumza lakini mimi nataka nijikite kwenye mazao haya

ya asili ambayo yanatupatia kipato. Katika vitabu vyote vinasema hatuuzi sana nje na ndiyo maana hatuwezi kukuza uchumi wetu. Mazao haya ya asili yakisimamiwa vizuri tunaweza kupata kipato kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama katika majedwali ambayo tumepewa mazao yote yameshuka ukilinganisha na miaka ya nyuma. Zao kama Kahawa, Pamba, Katani, Chai, Tumbaku na Korosho yangeweza kutupatia fedha nyingi lakini yanazidi kushuka siku hadi siku, sasa hili ndio tatizo la kilimo. Kwa nini hatujiulizi kwamba mazao tunayotegemea yatuingizie pato la nchi yanashuka, kulikoni?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Tanga ndio ambao tulipopata Uhuru miaka ya 1960 na 1970 ulikuwa unaongoza kwa zao la Mkonge katika dunia. Si suala la nchi nzima bali ni katika dunia, ikaja Brazil na baadaye Mexico. Sasa hivi ni Brazil ndio wanaongoza, wanakuja Mexico, halafu wanakuja Uchina.

Hata Uchina wametupita sisi ambao ndiyo tuna mashamba makubwa. Ule Mkoa mzima wa Tanga ni Mkonge mtupu, lakini sasa ni mapori. Mpaka leo ninapozungumzia suala hili bado watu hawana hata wazo la kufufua huu Mkonge, kuna nini, tumerogwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba nitoe ushauri maana nimesema nimechoka, sasa naomba nitoe ushauri. Sisi wananchi wa Mkoa wa Tanga sasa tunasema tunataka tulime Mkonge, tusaidieni. Sasa tutaulimaje, tutaulima kwa *style* ifuatayo, tunataka tuige *style* ya Morogoro ya kuwa *out growers* kama wenzetu kule wanavyolima chai na miwa. Kwa hiyo, yale mashamba yote ambayo wameshindwa naomba Mheshimiwa Waziri tupewe, wananchi wapewe haya mashamba, sisi tutalima mkonge na bahati nzuri *Katani Limited* wenyewe ambao ndiyo wana mashamba manono wamekiri kwamba wameshindwa kuendeleza Mkonge. Hao ndiyo wawekezaji tuliowapa.

Sasa kama tumewapa wameshindwa na wamekiri hawawezi, basi tupeni. Rais amekuja Tanga amekaa na wadau, ameongea tukatafuta mkakati, Mkuu wa Mkoa ametafuta mkakati, Wabunge tumetafuta mkakati, tumemwandikia Rais, bado hamsikii tu! Tupeni yale mashamba hatutaki kuona mapori. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tupewe, tunataka yale mashamba tuyalime na utaratibu tuliouomba ni huu ufuatao:-

(a) Wakulima wadogo wadogo wasaidiwe kuunda vikundi kwa shabaha ya kuwa na sauti ya pamoja.

(b) Kwa maeneo watakayogawiwa wapewe hati miliki. Tukipewa hekta sita ambayo ni heka 15 tupeni hati miliki. Tumetunga Sheria katika Bunge lililopita ya kukopa ili tukope, ili tuweze kusaidiwa kulima mashamba haya. *(Makofi)*

(c) Wakulima wadogo wadogo wawe na ubia katika *corona* ili wawe na sauti katika uendeshaji wa *corona* hizi. Kwa sababu tukiwaachia tu *Katani Limited* wawe na *corona* tumeumia lazima tuwe na ubia mle. *(Makofi)*

(d) Kuwe na mpango wa mbegu za Mkonge siyo za kuokota barabarani, lazima ziandaliwe. Tunaomba Serikali iandae mbegu safi za Mkonge ili tupande. *(Makofi)*

(e) Serikali isaidie huduma za ugani kama mazao mengine.

(f) Uwepo Mkataba unaofunga pande zote mbili baina ya wakulima na *corona* kwani ukataji wa Mkonge ni mgumu sana, uchukuaji ni mgumu sana, usindikaji na soko wale wakulima wadogo wadogo waweze kusaidiwa. Tutakomboa wananchi na tutapata pato kubwa, fedha zitaongezeka, wananchi wa Tanga na Mikoa mingine watakuwa wana uwezo wa kuweza kuondokana na umaskini kuliko kutuachia mapori, tunaongea miaka yote hakuna wa kutusaidia.

(g) Yale majumba yote ambayo yapo kule wapewe wananchi ambao mpaka leo hawajalipwa maslahi yao ili waishi mle ndani. Zile nyumba zinakuwa magofu, chonde naomba wapewe wananchi ili waweze kujikwamua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limezungumzwa na wengi ni hii benki ya wakulima. Naomba hii benki imlenge mkulima mdogo mdogo, siyo wa kati wala wakubwa kwani haitakuwa na maana yoyote. Kama mtu hana fedha wala mtaji hawezi kulima, kwa hiyo, hiyo benki iende kwa mkulima kule Kijijini au Wilayani ambako tutafaidika.

Hii ya kuwa na mabenki sijui tubadilishe tuwe na nani wanachukua fedha wale wale wa siku zote. Wale ambao ndiyo unawapigia debe humu ndani hawatapata na kilimo hakitaendelea. Naomba sana hiyo benki iwe na misingi hiyo, vinginevyo kwa kweli hakutakuwa na maana yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa naipongeza Serikali kwa kujenga uwanja wa kisasa. Naipongeza kwa dhati kabisa kwa kujenga uwanja wa kisasa. Hiyo itamaanisha kwamba tutaweza kupata angalau mashindano ya Kimataifa.

Lakini niiombe Serikali kwa suala la michezo, Serikali imeshindwa kutekeleza sera ya maendeleo ya michezo nchini ambayo imezinduliwa hapa na Bunge mwaka 1985, haijafanya chochote na kwamba zile Wizara zote zilizopewa jukumu la kuendeleza michezo hakuna. Huwezi kuwa na wachezaji wa kushindana Kimataifa na Mataifa kama huanzi kwenye *grass root,* Serikali imenyamaza, kuna nini? Tumeandika, tumesema, hakuna anayejali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. STANLEY H. KOLIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hizi mbili za Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba vile vile nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, kwa kufiwa na mzazi wetu. Tunaomba Mungu awape moyo wa subira, hayo ndiyo matatizo na wote tumeyapitia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo naona nichangie kidogo katika hotuba hii. Mimi naunga mkono moja kwa moja Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ataniuliza kwa nini wewe Kolimba unatoka Ludewa sasa unasema unaunga mkono Bajeti hii sababu zake ni nini? Naunga mkono Bajeti hii kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo mipango ndani ya Bajeti hii ya kupambana na umaskini. Katika Bajeti hii kuna mipango ya kuimarisha kilimo, sekta ya uzalishaji viwandani na madini.

Katika Bajeti hii kuna utaratibu wa kuongeza ufanisi katika huduma za jamii. Inalenga kumwezesha mwananchi wa kawaida kuweza kufanya biashara, iko mipango humu. Kwa hiyo, siwezi kuchelea kutoiunga mkono hii Bajeti kwa sababu inamtazama mwananchi wa Tanzania katika kumwendeleza. Kwa hiyo, hii ndiyo sababu iliyonifanya niunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo nina machache ya kuweza kuikumbusha Serikali. La kwanza, ukiona katika Bajeti hii unakuta kuna tatizo katika urari wa malipo ya nje *(balance of payment)* kati ya bidhaa tunazouza nje na bidhaa tunazoleta ndani. Utaona kwamba kuna ongezeko la asilimia 26 la bidhaa zinazoingizwa kutoka nje, lakini kuna ongezeko la asilimia 16 tu la bidhaa zinazotoka kwetu kwenda nje. Kwa hiyo, hata ile ziada ya dola za Kimarekani 246 utaona haikutokana hasa na *export* ya kwetu bali imetokana na hisani, mikopo, misaada na kadhalika.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri kwamba sasa mtazamo wa Serikali uweze kuwa zaidi katika kuongeza bidhaa zetu nje ya nchi hii ili tuweze kupata uwiano mzuri kati ya *export* na *import.* Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba kutokana na mpango wa *EPZ,* kampuni yoyote au kiwanda chochote kilichokuwemo katika nchi hii kipewe masharti yale yale na kufaidika na masharti yaliyotolewa na *EPZ* bila kujali kwamba kiwanda hiki kilianza mwaka juzi au mwaka jana mradi tu kinakuwa na *element exports* ndani basi kipewe *exemption,* kifaidi ile *condition* ambayo imewekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nilifikiri kwamba Serikali ifanye mambo ya kuthubutu, wathubutu kufanya mambo makubwa yafuatayo:-

Palikuwa na hoja inayozungumzia habari ya kusaidia kilimo katika Mikoa ya Nyanda za Juu ya Kusini. Tathmini tuliyoifanya katika Mkoa wa Iringa ni kwamba *operation* nzima ya ruzuku ile haikuleta manufaa yoyote kwa mkulima wa kawaida.

Kwanza, ruzuku ile haikuzingatia umbali wa Wilaya kutoka Wilaya moja hadi *godown,* kwa mfano Mkoa wa Iringa kwa Wilaya kama Makete, Ludewa na kadhalika *last destination* yake ilikuwa Makambako. Sasa kutoka Makambako mpaka kufika

Ludewa ni kilometa mia mbili na kitu. Sasa mkulima wa kawaida wa Ludewa atafaidi nini kama usafirishaji umeishia Makambako? Kwa hiyo, hiyo *last destination* ndiyo itakayo *determine* mkulima wa Ludewa aweze kufaidika na jambo hili. Vinginevyo kama unaweka ifikie Makambako hapa kati kati mbolea itakumbana na walanguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaiomba Serikali sasa *destination* yao ya mwisho kufikisha mbolea iwe Ludewa Mjini, tuna *capacity* ya kuweza kuweka kwenye ma-*godown.* Sisi Ludewa ni wakulima wazuri, tulikuwa tuna ma-*godown* karibu tumeweza kuweka tani 21,000, kwa hiyo ma-*godown* yale yapo kwa nini tusiweke hizo nanihi. Lakini kama alivyosema Mzee Lawrence Gama wakati wa asubuhi kwamba siasa ya kilimo kwa Mikoa ya Kusini ni mbolea tu. Ukituletea mbolea basi sisi tutafanya kazi. Tumewahi kupewa mbolea na tumewahi kuzalisha mazao na mazao mengine ilibidi tuchome moto kwa sababu hakuna jinsi ya kuyasafirisha, hakuna mnunuzi wala nini. Tunaomba tupeni mbolea ifike mpaka kwenye eneo linalohusika kwenye Wilaya zetu Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine lilikuwa kwamba hata wale wanaopeleka hiyo mbolea wale au Mawakala wanaopeleka si waaminifu, ni wafanyabiashara tu wanaofanya ulanguzi languzi tu. Nadhani Serikali kama ingetumia Wakala wanaoeleweka au hata Halmashauri zetu, sisi kwa mfano mkituambia Ludewa tufanye sisi Halmashauri yetu ipo tayari kufanya kuliko kutegemea hawa, hawa hawana huruma na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, lilikuwa kwamba mbolea yenyewe ilikuwa kwanza inachelewa. Kilimo tunaanza kukifanya mwezi wa kumi na moja, tunataka kupandia tunaletewa mwezi wa pili au wa tatu. Sasa tutapandaje?

Kwa hiyo, ninachotaka kusema hapa ni kwamba *operation* hii haikufanikiwa hata kidogo. Hata hivyo nimeona katika Bajeti hii mmesema kwamba mnataka kuendeleza wazo hili kwa maeneo mengine, mimi fikra zangu ni kwamba sasa tu-*consolidate* maeneo yale kwanza na tufanikiwe kuwa ni *pilot areas* ili tuweze kusonga mbele. Kwanza tufanikishe Nyanda za Juu za Kusini tumalize matatizo yote ndipo tusonge mbele kwa sababu matatizo pale yapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ya kuhusu kilimo vile vile kuna ukweli usiopingika kwamba wakulima wanahitaji pembejeo na Serikali yetu naipongeza sana iliunda Mfuko wa Pembejeo. Leo huo Mfuko una matatizo, hakuna mtu katika Wilaya zetu anayeweza ku-*qualify* kupata Mfuko wa Pembejeo wa Kilimo hakuna. Hata kama mtu aliyekuwa katika Wilaya zetu anaweza kuwa na mali ya kudumu, kwa mfano, nyumba yenye hati lakini masharti yake yapo arobaini kidogo.

Sasa masharti arobaini kidogo haya wataweza wapi, afadhali Halmashauri zetu zina mali ya kudumu zinaweza ku-*guarantee,* lakini bado haya mabenki nayo yana urasimu ule ule. Nadhani *terms of reference* zingetolewa kwa benki hizo kwamba mtu akiwa na mali ya kudumu nyumba ina hati, Halmashauri imem-*guarantee* mnataka nini zaidi ya hapo? Pawe na ka-*format* kazuri siyo kila mmoja ajiwekee atakavyo, hatutafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mmoja wetu aliwahi ku-*chance* kupewa mkopo lakini ilimchukua miaka miwili, mwaka wa kwanza hakuna kitu. Nimezunguka mimi kama Mbunge wake kumsaidia, mwaka wa pili karibu mwishoni anapewa ile, sijui kama anaweza kufanikiwa kurudisha hata huo mkopo kwa sababu alicheleweshwa sana kupewa hizo mbolea na kadhalika. Kwa hiyo, masharti ni magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni mipango ya kuendeleza kilimo katika ngazi ya Wilaya. Hili halijaeleweka, huu utaratibu wa zao moja la biashara na zao moja la chakula, haujaeleweka. Zao moja lipi, kwa nini, mtasaidia katika nini? Katika mbolea, katika zana au katika posho za *extension officers* halieleweki hili. Ni vizuri Serikali ikasema kabisa kwamba tunaposema kwamba zao moja katika Wilaya la biashara na hili la chakula tuna maana tutasaidia katika eneo hili. Sasa wengine pale tunaona kwamba basi tufanye tu *sunflower* lakini tuna Korosho tunataka kuweka, wakati huo huo tunataka kuendeleza kahawa na wakati huo huo tunataka kuendeleza Pareto. Kwa hiyo, nadhani mkitoa maelezo yanayoeleweka labda katika mbolea au katika dhana au katika nini pengine tunaweza kuelewa vizuri na watu wakafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni mikopo midogo midogo. Upo utaratibu sasa hivi wa sera ya mikopo midogo midogo, yaani kuna mpango ule wa kudhamini wawekezaji wadogo wadogo *(SME),* haujaanza huu nadhani lakini unataka kuanza. Hivi maelekezo yake yapo wapi maana yake sisi tunaokaa pembezoni hatutafikiwa na hiki kitu. Tunaomba utaratibu huu uelezwe kabisa kwamba uzingatie umaskini uliokithiri katika maeneo yanayohusika siyo kubaki tena Mjini tu, si kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho lakini bado moja. Nilimwomba Mheshimiwa Waziri kwamba Serikali yetu hii inawajali sana wananchi wake na kuna wakati Serikali iliamua kuchukua madeni yote. Sasa Halmashauri zetu za Wilaya zina madeni, madeni yanayohusu makato ya lazima kwa mfano mtu alikuwa anapelekewa kwenye *LAPF* au mwingine alikuwa anapelekewa *insurance,* Halmashauri zimeshindwa kulipa.

Kwa hiyo, tungeomba Serikali ichukue madeni hayo kama inavyochukua madeni mengine. Halmashauri za Wilaya haziwezi kulipia hii kwa kutegemea ruzuku ya Serikali haiwezi kulipa madeni ya zamani, wamezidiwa nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda la mwisho, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Ardhi aweze kutoa maelekezo zaidi yanayohusu Sheria ya Ardhi ambayo tuliifanyia marekebisho hapa.

Tunapozungumzia kwamba sasa ardhi mtu anaweza kuiwekeza akapata hela kutoka benki, wengi wananiuliza maswali haya, mimi kidogo napata kigugumizi maana ninaelewa kidogo zaidi, pengine mngetoa ufafanuzi wa namna hiyo ardhi hasa ni nani, huyo mtu anayetaka kuisajili atasajili wapi? Msajili mwenyewe ni nani, wakati gani, ukubwa gani, thamani yake ni nini, wananchi wengi wanasema ardhi tunayo, lakini sasa utaratibu mzima wa sheria ile nadhani bado haujaeleweka kwa wananchi wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba tena kuiunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie Bajeti hii. Naomba nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wote wawili kwamba Bajeti zao ni nzuri, kwa hiyo, naziunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue nafasi hii kuwapa pole ndugu zangu wote waliofiwa, ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Mheshimiwa Mbunge Dr. Aisha Kigoda na wale waliopata ajali katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote nikisimama humu ndani watu wanafahamu kwamba mimi kazi yangu kubwa ni kuzungumzia kilimo na sasa yapata miaka nane nazungumzia kilimo. Lakini niseme kwa bahati mbaya sana bado kilimo kipo likizo tena likizo ndefu. Sasa hilo ndilo tatizo kwamba kwa nini kilimo kinakuwa likizo, tatizo lake nini au kuna nini? Hii tumeshaelekezwa na Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Spika kwamba tunachochangia tutoe na ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mazingira ya kukibana kilimo ndiyo kuijengea hodhi pana ya rushwa kwa sababu wanaokuwa na vyakula ni hao wasiolima, wanaoonunua vyakula kwa wakulima. Huu wakati wa kiangazi wapo Vijijini wananunua vyakula debe shilingi 1,000/= mpaka shilingi 500/=. Mwezi wa kwanza watauza chakula kile debe moja shilingi 3,000/=, tuko pamoja? Hatuko pamoja. Uko na mkulima?

**MBUNGE FULANI:** Hapana.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haupo na mkulima. Wizara hii inashindwaje kununua chakula sasa hivi, kuweka mazingira mazuri ya masoko, wakulima hawa wakajua soko lao hadi wakaondoka kwenye umaskini au mnaagiza nje, hivi mnawatendea haki Watanzania hawa? Tatizo ni hilo tu haihitaji kwenda shule. Hawa wanaowachezea hawakwenda shule hata kidogo, nawafahamu mimi watu wenyewe na naweza kuwataja. Ndiyo hao akina Dewji, akina *Mohammed Enterprises,* ndiyo wanaonunua chakula na ndiyo wanaohodhi chakula na sasa ndiyo mnaowapa bei kubwa mnasema tumewakopesha nunueni vyakula, tunaendesha nchi namna hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyosema wapo kule Mbozi, Ifakara, Rukwa, au Kibaigwa hapa. Mnasema mnaweka mazingira mazuri ya kuweka masoko mtaweka mpaka lini? Hivi soko linahitaji kujengwa, wewe nenda pale na hela yako ya Serikali waambie jamani leo tunanunua gunia moja shilingi 15,000/=, soko tayari na sasa hivi hakuna mvua nendeni mkanunue chakula kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mnangoja kipindi hicho, tunaomba *supplement* ya chakula milioni ngapi, milioni 10, jamani, kweli safari hii hatutoi. Kweli. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama sitaona Serikali inanunua chakula cha maandalizi ya njaa sasa hivi, safari hii hatutoi, hatuwezi, tumefika mahali tumeelimika, hatutoi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo ndipo umaskini ulipo, hatuwezi kuzungumzia sehemu nyingine. Kilimo kinasema mkopeshe mkulima kwa kumsimamia na utaalam wa kilimo pamoja na kumpelekea pembejeo, akimaliza atakapovuna nunua chakula chake kama Serikali, kata deni lake. Sasa wewe unasema lete hati ya nyumba, mkulima gani ana hati ya nyumba, ndiyo sera tuliyonayo tunasema lete hati ya nyumba tukupe mkopo, utapata wapi, kama kule Songea kwa Waziri Mheshimiwa Pius Mbawala kweli Mngoni kabisa wa Namtumbo pale ana nyumba ya hati ya milioni 30? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ndiyo mazingira ya kumweka huyu mlanguzi aiue nchi kwa msingi huo huo. Kwa vyovyote vile Mhindi ukimwambia habari ya nyumba, Dewji yeye anayo ma-*godown,* si tumempa bwana, analeta hati moja ya *godown* zile alizonunua, anakwambia mimi hati ya nyumba ni hii, mnampa shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa *Exim Bank,* nasema hili nimetoka huko jana. Nyumba yangu mwisho sana sana nimejitahidi ni milioni 18 na deni langu la *total* milioni 35. Sasa wapi na wapi nina mwaka mmoja na nusu mwezi Septemba napewa kibali hicho mpaka leo sijapata. Halafu ndiyo mkulima ninayeonekana angalau.

Namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda alipokwenda juzi kwenye Jimbo langu tulikuwa pale na Mheshimiwa Abu Kiwanga hapo anasema jamani mnabeba hizi fedha bilioni 15. Mimi nikamwambia Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda kwamba pamoja na mipango mizuri hii tunapovuna miwa na kuiuza bilioni 15 tumenyimwa mkopo, akasema kwa nini hawakujali hata hili shamba tu, nikasema yote haya waliotujali hapa ni wawekezaji wa Afrika ya Kusini, tunakupongeza sana Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, uwekezaji huo endelea nao na Wizara hii naomba Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda asitoke mipango yake ni sahihi. Mheshimiwa Waziri alituuliza hizi fedha mna benki yoyote ya Ushirika, tukasema tumenyima benki, benki ziko Dar es Salaam haziwezi kukaa hapa benki ziko Dar es Salaam.

Kwa hiyo, niseme tu utawala, sera hii tunayosema ya CCM, Utawala Bora tunaousema sasa sielewi nisemeje hili neno la Utawala Bora kwa sababu Utawala Bora huu sasa mmeurundikia kila kitu kwenye Wizara hii ya TAMISEMI. Ukishahama Mkoani tu mambo yote yako kule, lakini mna uhakika na wataalamu wake, mmepangana vizuri kule chini. Kwa sababu ukishahama Mkoani ukienda Wilayani mambo yote yanapaswa yaanzie kijijini, yakitoka kijijini yaende kwenye kata, yakitoka kwenye kata yaende Wilayani hapo katikati wataalam wa mashambani wapo?

**MBUNGE FULANI:** Hakuna Wataalam.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Hao wataalam wote kwenye tarafa wapo, sasa ninavyoongea hivi pamba inapukutika Kilosa. Nilikuwa nazungumza jana na

Mamlaka ya Pamba, nimefuata pale dawa, bahati nzuri nikamkuta naye mtaalamu ametoka Kilosa, akasema kweli nimekuta maua ya pamba yanapukutika, nikasema nimeacha Bunge kufuata dawa, akasema kinachotokea ni kwamba pamba ya Kilosa ni nzuri sana, kwa hiyo imefunga matawi dawa haifiki chini, huo ni utaalamu? Anakubaliana na mimi kwamba yale maua yataendelea kupukutika, lakini kwa sababu ardhi ile ni nzuri haihitaji mbolea, sasa kwa hali hiyo haoni namna, yaani anakubaliana na yale maua yadondoke chini?

Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri kama inawezekana kesho twende tukaangalie pamba Kilosa ni hatari sana. Mheshimiwa Waziri hawezi kusafiri leo kwa sababu ni jioni, lakini naomba kesho twende Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko twende tukaangalie pamba Kilosa. Vinginevyo ile dawa mliyopeleka kule hatuwalipi, kwa sababu tuliishakubaliana kwamba tutawakata kwenye pamba.

Sasa nimeenda pale Wizarani jana hakuna dawa, wale wapigaji dawa wanasema majani yale yamefunga, haikupandwa kitaalamu na maneno ya ajabu ajabu na ya kutia hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba hili kwa maana yake nini, kwamba wataalamu hawapo vijijini. Mimi naamini sana Serikali yangu, lakini hatujapangana vizuri. Tunamheshimu sana Mheshimiwa Rais, lakini bado yupo peke yake hayuko na wenzake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili nataka niwahakikishie Waheshimiwa Mawaziri kwamba hakuna mtu anayehitaji Uwaziri, tunasema haya ni kweli tunahitaji Ubunge wetu na sisi mtulinde. Hakuna mtu anayetaka Uwaziri hata mmoja, haya tunayosema ndiyo ukweli wa mambo. Hatuwezi tukaendelea kusema kila siku halafu hatusikilizwi maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi naomba Pamba Kilosa kwa kweli baada ya siku mbili, tatu iwe imeeleweka kwamba dawa zimefika na hali nzuri inaendelea. Kesho tunaondoka na Mheshimiwa Waziri, ndugu zangu huko Kilosa tunaomba mtupokee tunakuja na Mheshimiwa Waziri haya mambo madogo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme jambo moja la msingi sana na nimelisema sana ndani ya Bunge hili ni kuhusu Utalii. Jambo ambalo tunasema ndiyo Wizara pekee ya kujivunia. Utalii Mikumi, Mikumi tunaomba ile barabara ihame yale matuta tulikubaliana kwamba tunayaweka kwa muda lakini juzi nimesikia ripoti kwenye vyombo vya habari kwamba wanyama bado kwa mwaka wamekufa 1,400.

Sasa sisi tunaomba barabara itoke Mikumi iende Kilosa, Dumila, mpaka Handeni. Mnaogopa nini? Mkikopa kwa dhamana ya mnyama kama Twiga hana tatizo, wewe unaogopa nini kukopa katika benki ya dunia. Mheshimiwa Waziri kazi gani sasa tunafanya? Wanyama wagongwe kila siku, hivi kweli inafika mahali hatulioni hata hilo! Barabara ile tunachohitaji pale kwa matuta yale tumeona wanyama wameongezeka wamezaliana sana lakini bado wanagongwa. *(Makofi)*

Sasa la pili, katika *Mikumi National Park* ni hoteli ile, namshukuru tena Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda amekwenda kuiangalia pale ile hoteli inatia huruma kwa sababu imekwisha. Zamani nilikuwa na tabia ya kuwaalika Waheshimiwa Wabunge wapumzike pale sasa naogopa nyumba inavunja yote. Sasa katika huduma hebu niwekeni ile hoteli kwenye huduma siyo biashara itoeni kwenye biashara iwekeni kwenye huduma, biashara ibaki kwenye utalii, tengenezeni ile hoteli ili watalii wakija iwe kwenye huduma na Mikumi ndiyo karibu na Dar es Salaam, na mimi pale ndiyo Dar es Salaam yangu, hivi mnataka Mbunge nipumzike wapi? Nyie wenzangu mnapumzika Dar es Salaam mimi nipumzike wapi sasa? Mimi napumzika *Mikumi National Park* sasa unakuta tena hii hoteli inavunja ni utaratibu gani huu haijapata kutokea. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sukari, juzi sukari ilikuwa imepanda bei, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula, namshukuru Mheshimiwa Abu Kiwanga, namshukuru Mheshimiwa Suleiman Sadiq, tumekaa tukaambizana waziwazi kwamba sukari tutaenda kila *godown* za wakubwa hawa, maana sukari ilipoisha sisi tulikuwa nazo *data* kwamba sukari tumetengeneza tani 240, mapungufu 60 haiwezi kupanda sasa imepandaje?

Hoja ilikuwa kwamba wao wamenunua sukari walipoona ya kwetu imeisha tuliyotengeneza hizi tani 240 waka-*stock* kwenye *godown,* sasa wakatafuta kupandisha bei, tukamwambia Mheshimiwa Waziri tupe siku mbili, tutazalisha sukari, tayari sukari inatoka Kilombero sasa, sasa tuna tani 11,000, sukari haijapanda na inaendelea kushuka. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. Hili ndiyo tatizo la mfanyabiashara na mkulima. Kilichotokea pale ni kwamba ilikuwa ipande na tuwaruhusu.

Tunaomba hata ile tuliyoruhusu tani 40, sasa walete kwa mpango. Hivi ngoja tuseme ukweli hivi hivi kama tatizo ni nini? Tunashindwa kuwa na *stock* tani 60 halafu inajigeuza inapanda bei. Hivi na hilo linahitaji mtu kwenda shule kuweka tani 60? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sukari ya kuzalisha tayari wenzetu wamefika tani 240 mwaka huu viwanda vyote vinakwenda vizuri, Kiwanda cha Kagera kinafanya kazi, *TPS* inafanya kazi, Mtibwa inafanya kazi, Kilombero ndiyo usiseme ndiyo bingwa wao. Sasa kuweka tu kusudi bei isijitokeze hizi tani 60 za akiba tu Serikali nayo inaona uwoga wapi? Tumejiondoa kwenye biashara kweli, lakini mengine ya huduma siyo kujiondoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara, nataka niseme mnisikilize vizuri Serikali kwenye barabara. Hivi mnaposema barabara za Mkoa mwisho maana yake ni tuishie Mkoani? Kwenye mashamba ya pamba tusiende, kwenye mashamba ya miwa tusiende, kwenye mashamba ya kahawa tusiende halafu tutasema tunaondoa umaskini, tunaomba barabara zitengenezwe mpaka vijijini. Kama daraja linaonyesha lina gharama kubwa fedha unataka itoke Serikali Kuu wapeni kwenye daraja la kijijini, sema hili siyo letu ni la Wilaya, Wilaya wana nini jamani? Tumefuta kodi zote kwa kujiamini kwamba sera ya CCM tunakusanya mapato na tunakusanya kweli kweli. Ajabu ni kwamba sasa tunapokusanya hatwendi pamoja, tunaomba twenda pamoja wananchi watuelewa.

Wananchi wanasema wao huku wametutuma sisi wawakilishi wao, wao ndiyo watawala wetu.

Sasa wale watu ni kuwaheshimu kwa msingi huo tulioweka kwenye sera ya Chama cha Mapinduzi. Tulisema mshikadau ndiye atakayekula. Sasa kama humtengenezei barabara hawezi kupata chakula, kama humpelekei pembejeo kwa wakati hawezi kupata chakula na huwezi kupeleka pembejeo kama huna mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inanipa taabu kidogo kuhusu elimu, Mheshimiwa Sophia Simba tunakupongeza umeanza toka kwenye swali la nyongeza. Kwa kweli tunapata shida tungeomba mlete *data* kabisa. Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni utakapokuwa unawasilisha hotuba yako ulete hesabu ni kitu gani kinakupa uwoga kutoa elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. MUSA A. LUPATU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nichukue nafasi hii jioni ya leo kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili nichangie kwenye hotuba hizi mbili za Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijachangia niwape pole ndugu zetu Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kuondokewa na mzazi wao. Tunaomba Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pili, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa ushindi aliopata na kunyakua tena kiti cha Bariadi kupitia Chama Tawala, CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nichukue nafasi hii kwanza kabisa niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote wawili ambao wamewasilisha hotuba nzuri ile hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafshaji naiona kama msingi ambao ndiyo umetengeneza hotuba ile ya Bajeti. Nimeziona hotuba zote mbili kwamba zina mipango mizuri na kwa kweli zina mwelekeo wa kumsaidia mnyonge hasa katika uwanja huu wa kuondoa umaskini. Nawapongeza sana kwa matayarisho hayo. *(Makofi)*

Vile vile nawapongeza Manaibu Mawaziri ambao wamemsaidia Waziri wa Fedha katika kutayarisha Bajeti hii pamoja na wataalamu, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu kwa kazi yao nzuri ya kuwasaidia Waheshimiwa Mawaziri wote wawili katika kuhakikisha kwamba bajeti hizi zinakuja kwa wakati na zinakuwa na mwelekeo mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie katika Bajeti hizi zote mbili kwa pamoja kwa sababu naona kwamba zinaoana sana. Kwa hiyo, sitatoa mchanganuo kwamba huu mchango ni wa hotuba ipi lakini nadhani Waheshimiwa Mawaziri watagundua kwamba maeneo nitakayokuwa nachangia yanahusiana na maeneo yapi katika hotuba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza sana kwamba katika miaka hii ambayo Waheshimiwa Mawaziri hawa wamekuwa Mawaziri katika Wizara hizi tumeona kwamba uchumi umeimarika hasa uchumi mpana, na tunaona kabisa umeimarika ukiangalia katika hotuba ile ya Mipango ukurasa wa 60 unaweza kuona kabisa ukuaji wa pato la Taifa jinsi ulivyobadilika kuanzia 1995 mpaka mwaka 2003.

Vile vile katika ukurasa wa 62 tunaweza kuona ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka ambao unahusika. Pale juu ilikuwa ni ukuaji halisi na hapa ni ukuaji wa pato wa kawaida. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwamba uchumi mpana umeimarika kama viashiria vya uchumi vilivyoonyeshwa, tumeonyeshwa katika akiba ya fedha za kigeni kwamba mwaka 2000 tumefikia kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa miezi karibu tisa. Mfumuko wa bei umeendelea kushuka kutoka asilimia 27 mwaka 1995 mpaka asilimia 4.4 mwaka 2003. Kwa hiyo, viashiria vyote hivi kwa wastani vinaonyesha jinsi uchumi mpana ulivyosimamiwa na Serikali. Kwa hiyo, nawapongeza kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme pamoja kuimarika kwa uchumi mpana bado mtu mmoja mmoja hajapata faida ya moja kwa moja kutokana na kuimarika kwa uchumi mpana. Kwa hiyo, ulioimarika zaidi ni uchumi mpana lakini ukichukua *Micro Economy* ama uchumi mdogo haukuimarika kwa mtu mmoja mmoja au kwa ngazi ya kaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi mpana hapa umeonekana kabisa barabara zimetengenezwa vizuri na zinaendelea kutengenezwa, ipo mipango mizuri ya barabara, shule zinajengwa za msingi, elimu ya msingi inaboreshwa, uandikishwaji watoto shule unaongezeka, ubora unaongezeka lakini haya ni ya jumla. Sasa tufanye nini ili uchumi huu ambao umeimarika uweze kusaidia mtu mmoja mmoja, kaya kwa maana ya kuongeza kipato na kuondoa umaskini wa kipato.

Sasa mimi nilikuwa ninayo mapendekezo, kwanza, nilikuwa napendekeza kwamba lazima sasa tubadili fikra, tubadili mtazamo, tubadili mwelekeo katika kupanga na tujiwekee vipaumbele vya kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja pamoja na kaya. Nitatoa mfano mdogo ambao unaweza kuonyesha ni jinsi gani tunaweza tukafanya ili tupate mabadiliko na tuweze kubadilisha mwelekeo huu wa uchumi mpana sasa kuupeleka kwenye kusaidia uchumi mdogo. Tumeona katika maelezo ya Waheshimiwa Mawaziri wote wawili kilimo kinachangia pato la Taifa kwa asilimia 48.

Kwa hiyo, kwa vyovyote vile kilimo kitaendelea kuwa mhimili wa maisha ya Watanzania walio wengi na vile vile kitakuwa mhimili kwa Pato la Taifa kwa maana ya mchango huu mkubwa wa asilimia 48. Sasa kama hatutatilia kilimo mkazo na kwa kweli kubadilika kutoka kwenye nadharia kwenda kwenye vitendo bado hatutakuwa tumeisaidia nchi hii na hatutakuwa tumewakomboa wananchi walio wengi ambao ni asilimia 78 ya Watanzania wanaotegemea kilimo. Kwa hiyo, lazima tu-*focus* sasa kwa mkulima mdogo na kupanua kilimo kwa njia nyingine nyingine ambazo nitazitolea mapendekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya mageuzi ya kilimo kunahitaji ujasiri mkubwa, kilimo hakina mvuto, mvuto wa kilimo ni unapovuna, lakini unapofanya kazi ya kilimo ni ngumu sana, kwa hiyo lazima tuingize mvuto katika kilimo. Moja ya njia za kuingiza mvuto katika kilimo ni kutumia mashine, matrekta yakitumika kwa wingi zaidi tunaweza kufanikisha kilimo chetu. Tunawezaje kupata matrekta. Nataka nitoe mfano, mwaka 1978 mpaka 1980 tulikuwa kwenye vita baina yetu na Nduli Idd Amini na marehemu Baba wa Taifa alituambia tufunge mkanda kwa miezi 18 lakini tulifunga mkanda kwa zaidi ya miaka 10 au zaidi. Kwa hiyo, Watanzania tunao uwezo wa kufunga mkanda, tunao uwezo wa kujinyima, hivi hatuwezi tukajinyima kwa mwaka mmoja au mawili kwa kuweka vipaumbele vyetu katika Bajeti na kuongeza fedha katika kilimo. Nilikuwa naiangalia Bajeti ya kilimo, Bajeti ya kilimo mwaka jana ile ya *recurrent expenditure* ilikuwa ni bilioni 14.9, ya *development* ilikuwa ni bilioni 30.8 kwa ujumla wake ilikuwa ni bilioni 45.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka huu katika Bajeti ya kilimo kwenye *recurrent* au matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 18.7 na Bajeti ya maendeleo ni bilioni 29.1 kwa ujumla wake ni bilioni 47.8, kwa hiyo, imeongezeka kidogo mwaka huu lakini ni katika *recurrent expenditure* au matumizi ya kawaida. Kwa hiyo, imepungua katika miradi ya maendeleo ambayo ndiyo tunategemea kwamba ingeibua uchumi zaidi.

Kwa hiyo, sasa nilikuwa napendekeza kwamba tukifunga mkanda mwaka mmoja, kwa mfano sasa hivi Bajeti ya nchi nzima ya matumizi ya kawaida ukiondoa mishahara ni bilioni 1.6 kama tukisema kwamba mwaka mmoja huu asilimia 50 ya Bajeti ya matumizi ya kawaida ukiacha mishahara ambayo ilikuwa ni trilioni 1.6 lakini nusu yake ni shilingi bilioni 800. Sasa tukifunga mkanda tukizitumia bilioni 800 kununua matrekta tutapata matrekta 32,300, ukiyagawa Kimkoa ni matrekta 1,536 kwa kila Mkoa hivi hatujabadilika! Kwa kufunga mkanda tu, hapo nimetazama item moja tu ya trekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tumeweza kwenda kwa miaka karibu 10 bila *OC* ya kutosha kwa nini mwaka mmoja tusiende na *OC* ndogo ili tubadilishe kilimo chetu. Nilikuwa tu natoa mfano huo mdogo kwamba kwa kweli tunaweza tukafanya mabadiliko katika kilimo kwa kuamua kutoa kipaumbele ku-*finance* kilimo.

Pili, tunaweza tukabadilisha mbinu za uzalishaji kwa kuweka mvuto zaidi katika kilimo, moja ya njia ambayo tunaweza kubadilisha ukiachilia mbali wakulima wadogo wadogo ambao hawatafaidika sana na kodi zilizofutwa, maana ziko kodi nyingi zilizofutwa sasa kwenye Bajeti hii zina mwelekeo wa kumsaidia mkulima anayeweka hesabu. Kwa hiyo, ni mkulima wa kati na mkulima mkubwa. Mkulima mdogo hatafaidika sana na marekebisho ya kodi hasa katika hizi kodi za mapato.

Kwa hiyo, ili tuweze kumvutia sasa mtu aingie kwenye ukulima hebu tuwe na kada mpya ya wakulima na wazalishaji wa viwanda tukiangalie kilimo kizalishe halafu tuwe na viwanda vya kilimo vitakavyochukua mazao hayo na kuyasindika ili yaweze kuongeza thamani yake katika soko la ndani na soko la nje. Sasa wakulima hawa tunaweza tukawapata vipi? Wako wahitimu wa Vyuo na Vyuo Vikuu ambao kama

tukibadilisha *syllabus* zetu zikawa na mwelekeo wa kujitegemea zaidi na kujiajiri na kisha tukawafanyia *attachment* kama ni wa kilim tukawafanyia *attachment* kwenye maeneo ya mashamba makubwa kwa mwaka mmoja ama mawili wakapata uzoefu halafu tukawapatia mashamba, halafu tukawapatia mtaji, halafu tukawasimamia katika wakati wa mpito, tunaweza tukapata kada ya wakulima wasomi na hii inaweza ikabadilisha kabisa kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba kwa njia hiyo tuwe na mafunzo lenga. Mafunzo ambayo yatalenga kujiajiri katika kilimo na katika kufanya biashara. Hii inaweza ikabadilisha kabisa mfumo wetu wa kulima na ukiangalia ule mfano wa kujinyima mwaka mmoja kuchukua asilimia 50 ya *OC* tunaweza tukafanya mabadiliko makubwa.

Kwa hiyo, mabadiliko haya yaendane pia na Ugani. Maana katika Ugani tunayo matatizo ya msingi kabisa yanayotokana na sera. Sera ile ambayo imewabadilisha watu wa mifugo, watu wa kilimo kuwa mabwana shamba na mabwana mifugo kwa pamoja kwa hiyo wanajua kidogo kidogo ya kila jambo lakini hawajui vya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hawawezi wakawa Maafisa Ugani wanaoweza kufanya vizuri na kushauri wakulima wetu. Kwa hiyo, lazima tuwe na mabadiliko pia katika mitaala yetu ya kufundisha kilimo na kufundisha mifugo ili ilenge katika utaalamu zaidi wa kina.

La mwisho, kilimo hakiwezi kwenda bila maji. Tumeona kabisa kwamba mvua zimepungua, hii dalili hakuna haja ya kuisema kila mtu ameiona, wakulima wameiona na sisi tumeiona na wataalam wameiona. Kwa hiyo, kwa makusudi hayo hayo ya kutenga fedha na kufunga mkanda basi tuwe na mkakati wa makusudi kabisa wa ujenzi wa mabwawa nchini kote kwa ajili ya umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema nitapendekeza mbinu na ndiyo hizo nimezipendekeza kwa uchache wake kwa sababu ya muda. Kwa hiyo, sasa naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza na mimi nitoe pole za dhati kabisa kwa familia ya mzee Kigoda kwa msiba mkubwa sana uliowapata. Vile vile niwape pole Waheshimiwa Wabunge waliopata matatizo njiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda kwa hii mipango ambayo ni mizuri na kwa kweli kama nchi lazima tuseme kwamba uchumi wetu unakua vizuri na lazima tujipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kukua huku lazima tusema kwamba je, swali tunalojiuliza uchumi huu unakua kama ambavyo ungetakiwa ukue? Je, ni kweli kwamba ukuaji wa uchumi katika nchi kama Msumbiji hatuwezi kuufikia ule ukuaji huo? Sasa mimi nataka niseme kwamba nadhani tuna matatizo ambayo yanafanya pamoja na ukuaji

huu mzuri tusiweze kufikia kasi ambayo wenzetu kama Msumbiji wamefikia kwa muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili la utekelezaji. Tunalo tatizo la utekelezaji na hili limezungumzwa sana ndani ya Bunge kwamba tuna mipango mizuri na mikakati mizuri lakini utekelezaji mara nyingi huwa si mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwamba hapa nchini tuna magonjwa mawili. Ugonjwa mmoja unaitwa poa sasa inawezakana ikawa ni mambo *POA,* lakini *POA* maana yake ni *Paralysis of Analysis,* tunachukua muda mrefu sana kuchambua, tunaichambua mikakati, miradi mpaka tunakuwa *paralysed, Paralysis of Analysis (POA).* Sasa tusiporekebisha hilo tuna matatizo.

Ugonjwa mwingine unaitwa *excusitis,* tunatoa *excuses,* sana sana huwa tunasema tuko mbioni, tuko mbioni kutekeleza, ule ugonjwa unaitwa *excusitis,* tunatoa *excuses.* Sasa ni lazima turekebisha hilo. Kwa sababu wazungu wanasema: *"A right decision at the wrong time becomes a wrong decision."* Sasa hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tutalizungumza na tutaendelea kulizungumza lingine ni suala la rushwa. Mimi naomba niliseme tena kwa sababu limekuwa likizungumzwa. Ukweli ni kwamba rushwa ipo nchini, tutakataa na tutaambiwa tutaje nimesikia hata Waheshimiwa Wabunge wengine wanasema tutaje, jamani rushwa ni kama ngono, humwoni mtu kirahisi anapofanya tendo lile. Kuna mahali ambapo kuna Wamisionari na ma-*sister* naijua hapa nchini, kuna wakati kila baada ya muda *sister* alikuwa anapata mimba, baada ya muda *sister* anapata mimba, lakini sasa huwezi ukasema umemwona lini *sister* akifanya ngono, lakini unaona mimba tu inakua. Sasa lazima uwe na hakika kwamba pamoja na kutomwona *sister* akifanya ngono huyu kafanya mimba imetoka wapi?

Sasa ndiyo tunasema ukiona watu wanajitajirisha tu nchini, ana majumba na vitu vikubwa vikubwa unajiuliza amevipataje kama siyo rushwa. Sasa ukisema nimtaje *sister* yule mbona nilishindwa kutaja kwamba ni siku gani nilimwona akifanya ngono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili lipo. Lipo kwa sababu juzi mimi nimekuwa Zambia na wenzangu katika ripoti ya wanasiasa nchi za nje wanaofanya utafiti wanasema Tanzania ni kati ya nchi kama ya tatu au ya nne Afrika kwa rushwa na hawatusingizii kwa hili, kwa nini wanatusifu katika uchumi unavyokua halafu rushwa watuonee. Kuna ukweli ndani yake. Mpaka tukaulizwa jamani *you people how comes Mr. Clean can lead such a corrupt country."* Wanashangaa Rais ni *clean* lakini nchi ni rushwa tupu. Tumeulizwa. Tukababaisha pale unajaribu kutetea nchi yako kwamba hapana tunachukua hatua, lakini ukweli ndio huo. Sasa mimi niseme kwamba Wizara ambayo unaweza kusema mambo makubwa ya rushwa yanapotokea au ni msimamizi wa masuala mengi kwenye upande huu ni Wizara ya Fedha. Wizara ya Fedha ndiyo inasimamia maeneo makubwa mawili yenye rushwa iliyokithiri hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza lilielezwa vizuri sana mambo ya *Procurement.* Maana yake Sheria ya *Procument* iko Wizara ya Fedha. Pale mimi siwezi kuelezea zaidi alivyoeleza Mheshimiwa Philip Marmo hapa leo. Lakini asilimia hii tunayokusanya ya 13.5% ya *GDP* inaonyesha kwamba tunao uwezo wa kufanya zaidi kama rushwa ingepungua. Kwenye *Procurement* tuna matatizo makubwa sana. Halafu hatuwi *serious* katika kuliangalia hilo. Kama juzi inateuliwa *Procurement Appeals Board,* Bodi ambayo ndiyo itakuwa inasimamia *appeals* kwenye *procurement.* Mle ndani hakuna *professional* mnunuzi katika ile *appeals boards.* Kweli *are we serious.* Sasa huu ni upendeleo ni *nepotism* au ni *complete disregard of professionalism. (Makofi)*

Sehemu nyingine ambayo inasimamiwa Wizara hiyo ni ukusanyaji wa mapato. Kwenye mapato *TRA* kwenye madini kuna rushwa kubwa sana. Na tusidanganye kwamba hakuna ndiyo unasikia juzi makontena yanaibwa. Hawawezi kuiba bila ushirikiano na wafanyakazi wa *TRA* wa Wizara ya Fedha. Lakini tukisema aah, mtu anasema bwana huyu ananisema sana. Lazima kama Viongozi tukubali kwamba *criticism* ni kitu ambacho kinagusiwa. Ukiwa *criticized* usilete *personal interests* za kuleta chuki za binafsi. Kwa sababu kama wazungu wanavyosema tunajua kwamba *although no one likes to be criticized but we learn and grow from honest criticisms.*

Kwa hiyo, lazima tujirekebishe tusiwe tu tunakuja hapa tuna-*brag* kwamba mambo yanakwenda vizuri wakati mambo yanakwenda si vizuri sana. *Afterall bragging about oneself is a sign of lack of confidence.* Ndiyo unaweza ukaji-*brag* hii ni *lack of confidence.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema kwamba tunalo tatizo. *PCB is very ineffective.* Hili limezungumzwa mara nyingi sana kwamba jamani kuna tatizo ndani ya *PCB.* Turekebishe muundo wake. Halafu unakuta pale Wakurugenzi wameruhusiwa kuendesha Uwakili binafsi. *PCB* ni kama Polisi, kama ambavyo Polisi, Hakimu hawezi kuruhusiwa kuendesha kuwa na sehemu yake ya Uwakili, *PCB* nayo ni kama Polisi. Utamruhusuje huyu unajuaje kwamba kesi anayekwenda kuchukua kumtetea mtu kuna rushwa ndani yake. Hawa ni Mapolisi jamani kwa nini umruhusu aendelee kuwa Wakili wa Kujitegemea wakati ni Mkurugenzi kwenye *PCB.* Haya ndiyo matatizo mengine ambayo lazima tuyarekebishe.

Sasa mimi nasema kwamba hilo ni tatizo na tujiangalie tukubali kabisa tusije tukawa kama yule Mfalme ambaye alikuwa uchi lakini bado anasema hayuko uchi kwa sababu anadanganywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mishahara. Mimi nilitaka nizungumzie suala hili kwa maana kwamba wafanyakazi wetu inaonekana kwamba hatuweki umuhimu katika *human resource.* Watu walivyosema kwamba: *"people are more valuable than capital or equipment. Actually people is the most valuable assets of any country."* Akaendelea kusema kwamba: *"people can be your biggest asset or your biggest liability."* Tusipotumia watu vizuri uchumi wetu utakwenda chini.

Kuna hii sera ya mapato na tija sijui tuliifunika wapi. Lakini mishahara ya Tanzania jamani ni midogo. Mimi namsifu kama wengine mlivyosikia juzi tarehe 4 Juni,

2004 Rais wa Uganda amesema kwamba atapandisha mishahara ya *scientists* wake kuwa kwenye *world class level.* Kwa sababu anaona kwamba wanaondoka wanapandisha uchumiwa nchi zingine lakini nchi yake inadidimia kwa sababu ya kutotilia maanani hawa wafanyakazi na mishahara. Sasa lazima tufike mahali na sisi tuamue kwamba uchumi unakua lazima tutenge fedha ya kupandisha mishahara ya wafanyakazi wetu na hasa wataalam ambao tukiwatumia vizuri tutapandisha uchumi wetu, tija itapanda. Mimi sina hakika kwamba utafiti wa ndani umefanyika kuangalia *correlation* kati ya mapato au tija na mishahara ya wanaotumika. Nadhani haijafanyika kwa sababu ikifanyika tutaona kabisa kwamba kuna *correlation* kubwa sana. Sasa tufanye huo utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchini kwetu mishahara ni midogo halafu bahati mbaya kuna *paradoxes* ambayo inavunja nguvu wakati wengine wanapata mishahara midogo kwenye Serikali hiyo hiyo wengine wanapata mishahara mikubwa hiyo *world class* tunayozungumza. Ndani ya Serikali na ndani ya Taasisi za Serikali. Tunaangalia na fedha wanazopata hizi hizi tunazokusanya kodi, zingine ni mikopo ambayo tunarudi kulipa kodi yetu.

Sasa angalia maeneo kama *TRA, BOT, TTC, PPF* angalia kwenye *agencies* zinazoanzishwa na Serikali. Leo mtu anatoka kwenye mfumo wa kawaida wa Serikali mtumishi kwa sababu kitengo kimeanzishwa sasa ni *agency* anapata mshahara mara nne au mara kumi na wengine wanapata mishahara midogo. Kweli *productivity* itakua kwenye eneo hilo. Nchi hii ni moja hiyo hiyo. Huwezi kuniambia kwamba hii *PSRC, TTC* hata kama *World Bank component* ipo tutailipa kwa mapato haya. Huyu anayezalisha kwa nini yeye haangaliwi. Tuondoe *paradox.* Si kwamba tuwashushe hawa wa mishahara ya juu lakini tuwapandishe hawa ambao mishahara iko chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliseme lingine la mwisho mwisho hili la kuondoa vyanzo vya mapato kwenye Halmashauri zetu. Tunakwenda kinyume na sheria yetu ya kupeleka madaraka chini. Unapopeleka madaraka chini kweli kama unataka *accountability* lazima umpe uwezo wa kukusanya na kutumia. Ukimpa uwezo wa kutumia tu yale madaraka hujayapeleka sawa sawa *accountability* bado. Sasa jamani ni kitu gani kilichoko huko. Tunaendelea kunyang'anya mapato ya Halmashauri zetu.

Ni kweli wanasema kutakuwa na ruzuku kufidia lakini kwanza haitatosha. Mimi nangojea sana kuangalia kwamba Wilaya yangu ya Ilala ambayo leseni tunapata 1.8 bilioni kwa mwaka kama tutaipata *full* moja hilo la kwanza. Lakini pili hata kama ukileta ruzuku inayotosha jamani bado hujaweka ile *responsibility* kwamba anao uwezo wa kukusanya na kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara ya Fedha kwa kweli mtakubali hii *global budget* lakini bilioni 8 Wizara ya Fedha itenge kwa ajili ya hatua ya kwanza ya kufidia wananchi wangu wa Kipawa. La sivyo pamoja na kupitisha hii *global budget* kule mbele ya safari itakuwa taabu kidogo humu ndani. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, nashukuru nadhani wamekubali kutenga kama bilioni moja lakini Wizara ya Fedha iangalie namna ya kuweka bilioni 8 ili iongezee awamu ya kwanza ya kufidia wananchi wa Kipawa ifanyike katika bajeti hii ya mwaka huu ili angalau awamu zingine basi tuweze kuzipeleka mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nangojea hiyo Bajeti kwamba Kipawa angalau wale wa Kipawa walipwe, Kigilagila na Kipunguni wanaweza kungojea lakini wa Kipawa waweze kuondoka katika Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kutoa pole za rambirambi kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda kwa kutokwa na mpendwa baba mzazi wao na Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, rafiki yangu kwa kutokwa na binti yake mpendwa, Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Pili, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kushinda kiti cha Ubunge Bariadi. Tatu, nawapongeza Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha kwa pamoja na timu zao kwa kazi nzuri walizozifanya kuandaa hotuba ambazo ziko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa ambavyo huenda si kawaida sana lakini wananchi wangu wa Vijiji kama vitatu au vinne, wamenituma *message* rasmi kwamba nifikishe salaam za shukrani kwa wafuatao:-

Kwanza ni Mheshimiwa Charles Keenja, Waziri wa Kilimo na Chakula kwa kuonyesha kwamba kumbe ngazi ya juu ya Serikali inafikiwa na wadogo na kusikilizwa, kwamba wanashukuru kuwapa matumaini ya kujiondolea umaskini na kwamba pia bado watamfuata. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Pili, Mheshimiwa George Kahama, Waziri wa Ushirika na Masoko kwa kuonyesha kwamba mnyonge anaweza kupata haki yake na kutupa matumaini ya soko la Tengeru. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mwingine ni Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa kutuondolea adha ya hatari ya kupofuka macho yao, wanakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Hao ni wananchi wa Vijiji vya Nkwaranga, Njani, Loliondo, Makiba, Majengo, Mbughuni na Patanombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nizungumzie suala la umaskini na hali ilivyo katika Jimbo langu. Katika mwaka huu tuna njaa. Nina Tarafa mbili ambazo hazikupata mvua ya kutosha. Matumaini yangu ni kwamba Bajeti hii itazingatia hilo suala na nina imani sio mimi peke yangu au sio Arumeru Mashariki peke yake, hili ni suala ambalo nina imani linawahusisha na wengine wengi.

Tuna ombi rasmi, kuna maeneo ambayo ni ya kumwagilia katika Tarafa ya Mbughuni tuna Mto mmoja unaoitwa Mto Kikuletwa. Mto Kikuletwa una watu ambao wana mashamba makubwa kidogo na ambao wana hatimiliki za maji.

Tunaomba kwa sasa hivi ili kunusuru mazao ambayo yako shambani kwa sheria ambayo ipo waweze ku-*suspend water rights* hiyo sheria inaruhusu kwamba *water rights* zinaweza kuwa *suspended* wakati ambapo hali ya hewa ni mbaya na kwa sasa hivi tunaomba kama inawezekana Serikali ione hiyo hali kwamba ni mbaya na kutunusuru maisha yetu. *Water rights* hizo ziwe *reviewed* na ikiwezekana ziwe *suspended* kunusuru maisha yetu kwenye huo Mto Kikuletwa, Tarafa ya Mbughuni kuanzia Majengo, Makiba *all the way* mpaka Mikongani, Tarafa ya Mbughuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la elimu katika mpango wa MMEM wananchi walikuwa wanahitajika kwamba wajenge mpaka kufikia *linter.* Ambao hawakuweza kufikia *linter* au kujenga msingi hawakupata mgao wa fedha za MMEM. Kwenye Bjeti hii pia kuna mpango unaofanana na huo kwenye Elimu ya Sekondari. Nina imani mtindo huo huo utakuwepo.

Kwa jamii ambazo ni vigumu kupata uwezo wa kujenga msingi licha ya kufikisha *linter* sijui watapataje hiyo fursa ya kupata msaada wa mpango kama huo. Ninachoomba hapa ni kwamba tunahitaji hii sera ya mgao kwa sehemu ambazo hazina uwezo kabisa wa kuweza kujenga msingi licha kufikia *linter* inayohitajika kwenye hiyo mipango ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ni kuhusu kodi kwenye mazao au *produce cess* ambayo imejitokeza kwenye Bajeti. Kwenye Bajeti mwaka jana tuliondoa kodi za kero na wananchi tulifurahi na tunashukuru sana. Lakini kuna hii kodi ya *cess* na imejitokeza tena ukurasa wa 29 wa Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Kodi inayotozwa kwenye mazao ya kilimo inasemekana kwamba isizidi asilimia 5 ya bei ya shambani yaani *farm gate price.* Pamoja na shukrani za kuondolewa kodi hizo lakini pia tunaomba Serikali ifanye yafuatayo:-

Kwanza Serikali irejee *produce cess* kwa nia ya kutambua na kuainisha faida na adha za kiuchumi na kijamii zinazotokana na kodi hiyo. Irejee mfumo mzima wa ukusanyaji na *share* au sehemu yake pamoja na matumizi kwenye Serikali za Mitaa. Serikali ione uwezekano wa kuondoa hiyo kodi moja kwa moja kwenye mazao ya chakula kama vile mahindi, maharage, ndizi na mchele kama kule Kyela. Kutegemea na zoezi hilo hiyo kodi iondolewe moja kwa moja mpaka hapo tutakapoweza kuondoa umaskini mwaka ambao umelengwa kama ndio *target* yetu ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la biashara ndogo ndogo. Suala kubwa na zito kuhusu sekta hii ya biashara ndogo ndogo ni jinsi gani iweze kutoka kwenye *informal sector* kwenda kwenye *formal sector.* Nadhani hili ndilo suala la muhimu kwa sababu asilimia 70 ya sekta binafsi ni sekta ya biashara ndogo ndogo. Kwa hiyo, hii ndiyo sekta ya pili kwa kukuza uchumi ikifuata sekta ya kilimo. Kui-*approach* kwa njia ya leseni kwa maana ya kila mwenye biashara ndogo awe na leseni hata kama hailipii mimi nadhani hakutatosha kuifanya sekta hiyo kuwa rasmi au kui-*organise* zaidi ya ilivyo sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo langu ni lifuatalo kwamba Serikali iunde timu ya wataalamu wa *private sector development* ambao wataifanyia *study.* Mimi nadhani kuna haja ya kuifanyia *study.* Halafu itoe mapendekezo ambayo Serikali

itayafanyia kazi. Hili suala na hasa *Machinga business,* imekuwa ikizungumziwa kwamba ni *timed bomb* kwa muda mrefu lakini yaelekea kwa kweli sijaona kazi yoyote ambayo imefanyika kuonyesha kwamba hili suala linachukuliwa *seriously. But at one time* itakuwa ni *timed bomb for real.*

Suala lingine ni kuhusu tofauti kati ya riba za mikopo ya Benki na riba za amana au *differential* kati ya *Savings rates* na *Lending rates.* Hili ni suala ambalo Wabunge na wananchi kwa ujumla tumekuwa tukilalamikia kwamba tofauti kati ya riba hizi ni kubwa mno. Kwa mfano, licha ya jitihada ambazo zimefanyika kupunguza zinazoitwa *structural rigidities* kwa mfano kutazama matatizo yaliyopo kwenye sheria fulani fulani ambazo zinakuwa *constraints* kwa *commercial banks.* Taarifa ya Benki Kuu inaonyesha kwamba imekuwa na tofauti ya 10.6% Juni, 2003. Mwezi Aprili, 2004 ilikuwepo tofauti ya 9.3%. Riba tofauti kati ya *Savings rate* na *Lending rate.* Hizo tofauti ni kubwa mno.

Kwa kweli inaonyesha kwamba imekuwa ikipungua kidogo hizo *percentage points* au hizo *differential* zimekuwa zikipungua kidogo. Lakini bado ukichukua *savings* ile *posted savings rates* ambazo *on average* zimekuwa zikibakia kwenye 2.4 au 2.5 kwa kweli haivutii. Serikali haiwezi kuendelea kuinyamazia hii hali kwa muda mrefu kama tunataka uchumi ukue kwa asilimia 8 ambayo tunaihitaji ili kuondoa umaskini.

Sera ya riba kwa mwaka wa fedha ujao ambayo imejitokeza kwenye kabrasha la Benki Kuu ni kwamba soko la hundi za Serikali au *Treasury Bills* litaendelea kuwa chanzo cha kutambua riba. Au kwamba *interests rate will be determined in the Treasury Bills Market.* Kwa hiyo, bado *Treasury Bills Markets* ndiyo *anchor* ya *interest rate.* Hapa ndipo tunapata sababu za riba za *savings* kuwa ndogo na *differential* hiyo inaendelea kuwa kubwa.

Kwanza riba za Benki za Biashara na Taasisi za Fedha haziendi sawa na yield kwenye *Treasury Bills Markets.* Hiyo hata ukitazama kwenye takwimu zilizopo haziendi *intendim.* Riba za biashara na Taasisi za fedha haziendi *intandem* na *Treasury Bill rates* ziwe *yield* kwenye *Treasury Bills Markets.*

Pili, sioni kwamba uwekezaji wa ndani una uhusiano na *yields* kwenye *Treasury Bills Markets.* Bado hiyo hatujaweza ku-*establish* na tungewaomba watu wa Benki Kuu na Wizara watusaidie kuonyesha kama kuna *relationship* yoyote hapo.

Tatu, riba za wenye fedha nyingi au wale *prime depositors* wanavyoitwa, zao karibu zinaendana kidogo na *yields* za *Treasury Bills* au hundi za Serikali, zinakwenda karibu sawa sawa. Tena ni kubwa ziko kwenye *average* ya kuanzia 5 na kuendelea ambapo *deposit rates* zetu sisi wananchi wa kawaida ziko kwenye 2. Kwa hiyo, inaonekana kwamba ni wale walio na uwezo ndio wanalipwa zaidi na sisi ambao hatuna chochote cha kuweka kwanza tunachopata kidogo ndicho ambacho kinalipwa kidogo zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonyesha kwamba tuna-*discourage* wale ambao wanahamasika kuwekeza kwenye *Banking sector* ili ziwe available kwa ajili ya uchumi.

Kwa hiyo, kwa kweli *contribution* yetu katika kukuza uchumi inakuwa *discouraged* na *Banking* na *interest rate constraints* za *Banking system.* Japo kwa kweli wanazungumza kwamba tatizo lililopo ni *structural constraints* za *Banking system* yenyewe mimi napendekeza kwamba bado inahitaji kufanyiwa kazi na ikiwezekana Serikali ione ni nini kinachoweza kufanyika ili kupunguza hii *differential* kati ya *savings rates* na *deposits rates* na *lending rates.* Nina maana ile *savings* za wananchi wa kawaida sio zile kuanzia *time deposits* na kuendelea juu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kunipa nafasi na mimi nichangie machache tu kwa Bajeti zetu hizo au Bajeti moja ya katika sehemu zake mbili Mipango na Fedha.

Kwanza kabisa nitoe pia shukrani kwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa *presentation* ya Kamati ya Fedha na Uchumi tuliyofanya kazi hiyo Dar es Salaam naye akaipeleka hapo. Akatoa *presentation* nzuri sana na ikaeleweka vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo nataka pia kuunga mkono wenzangu kuwapa pole Mheshimiwa Waziri Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao mzazi. Kwa hiyo, nami namwomba Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Sasa nadhani kabla sijaenda kwenye kuchangia hiyo nitoe pongezi zangu, pongezi hizo ziko kwa Wabunge waliokwenda Bunge la Afrika ambao walianza kazi yao Addis Ababa kwa kishindo na vizuri sana halafu na Mbunge aliyekwenda *SADC* nao pia wamefanya kazi nzuri mpaka sasa na tunataka waendelee hivyo Tanzania ijue kuwa tuna watu wenye siasa na tunaunda siasa sio kama tunajifunza tu.

Pongezi nyingine za pekee ziende kwa Mheshimiwa Danhi Makanga, kwa kurudi tena Bungeni kwa kupitia *the right door.* Kwa sababu alikwenda Bungeni kwa mara ya kwanza akaona amepita *the wrong door,* ikampa matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera maalum pia ziende kwa Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Bunge la Afrika *for the first time aah !! A lady. (Makofi)*

Baada ya kutoa pongezi hizo zote labda niongee kwa ufupi tu juu ya *speech* zenyewe. Kwanza nawapa pongezi Mawaziri wote wawili kwa kutoa Bajeti nzuri yenye ufasaha na yenye mwelekeo na kuwa tunakwenda mahali tunaweza kujua tunakwenda wapi tulipotoka na sasa tunakwenda huko mbele. Kwa hiyo, kwangu mimi naunga mkono bajeti zote mbili kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Baada ya kuunga mkono na kusema kuwa wameshatuonyesha milango kufanya nini na kuongea nini labda niongelee kwanza mipango. Waziri ameeleza kazi ya Wizara

yake ya Mipango na Ubinafsishaji kwa ufasaha na kwa kina na mimi nakubaliana naye ni nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nikaona kuwa labda tunaweza kuboresha zaidi Wizara yetu kama tutaweza kuifanya irudi kazi yake ile ya zamani. Kazi yake ya zamani ilikuwa ni *Economic Affairs and Planning.* Ile ilikuwa ya kudumu na ya muda mrefu. Lakini huo ubinafsishaji ipo ina kazi maalum lakini labda ifanywe na ikiisha itabaki kazi ya *Planning* peke yake na *Planning* haitakuwa ipo kama kweli haikutengenezewa mfumo ule ambao tulikuwa nao zamani. Ingawa kwa wakati ule ilikuwa ni *Planned economics* yaani siku hizi wanaita ya ukiritimba zaidi yalikuwa Mashirika na Serikali.

Lakini bado sasa tunahitaji zaidi *Planning* kwa ajili kuwa sio Mashirika yatakuwepo hayo yatakuwa yamekwisha. Sasa kutakuwa na *Private Sector. Private Sector* huwezi kuiendesha au kuacha inakwenda tu mwisho *investments* zote zinaweza kwenda kwenye bia na Coca-cola tu basi na tukapata fedha nyingi sana, lakini sidhani kama hiyo tutaita maendeleo.

Kwa hiyo, Wizara hiyo bado tunahitaji kutoa mwelekeo katika uchumi na katika *investment* yenyewe ndiyo hiyo itakuwa *Planning* hasa kuanzia kwenye kilimo, chini kabisa kwa wakulima mpaka kwa Makampuni makubwa *(Trans-national)* ambayo yanakuja sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu Amerika, *Europe* sasa hivi uchumi wao wa kikabaila umekuwa *so much* huoni kama wana *Planning* lakini *Planning* ipo inafanywa. Wana Idara zao zimejificha kule zinafanya kazi hiyo ya *Planning.* Sisi uchumi wetu haujakuwa ukabaila tunaelekea labda *one day* tutakuwa *full* kabaila kwa wakati huu tutahitaji *planning* na maelekezo ya Serikali katika *investments* na mambo mengine.

Kwa kusema hilo nilidhani kuwa ya kwanza kabisa, ushauri wangu ninautoa ni huu kuwa *planning* irudi kama zamani, badala ya ku-*plan public sector* itakuwa ina-*plan public,* ikiwa wakishughulikia zile zinazoitwa *Executive Agencies* sasa, lakini zaidi *private sector* kuingoza inakwenda *the right root* na baadaye itoe matunda, *the right* matunda. Hiyo ni kwa upande wa *planning.*

Kwa upande wa Hazina nimeshawapongeza pia, huko zaidi nitaongelea kitengo kile cha *TRA* peke yake kwa sasa. Kuwa *TRA* wamefanya kazi vizuri na wanaendelea kufanya kazi vizuri sana na ninawasifu. Ninawasifu kwa ubunifu wao pamoja na mbinu mpya wanazo anza kuzitekeleza kama hiyo *self assessment* ya kodi kuwa labda tutakuwa tunaji-*assess ourselves* sijui mpaka kufikia *level* gani. Mkulima mdogo sijui kama ataweza au Mmachinga sijui kama ataweza labda atasaidiwa kwa namna moja au nyingine. Hiyo ni moja.

Lingine ni kuwa ile ya kuweka mashine pale Dar es Salaam au na *Port or entry,* zinazoweza kuona *through the container.* Ile *Container* ni chuma, *very thick steel,* lakini wanasema sasa wanaweza kutazama ndani mle, wakaona vitu vyote vilivyomo ndani ya

*container* na wakalinganisha na *manifesto.* Wakiona kuwa kama alisema ameleta *spare,* kumbe ameleta Konyagi, watasema zile *spare* hazifanani na zinafanana kama ni pombe fulani *special* basi wataifungua na hii itaharakisha mambo yao ya *clearing* na kutoa mizigo Bandarini. Kwa hiyo, hizo mbinu ambazo wamezileta na wanazidi kuziendeleza.

Pamoja na sifa hizo na pongezi hizo za kuweza kukusanya fedha kwa wingi, bado ningependa kuwashauri kuwa waendele kuboresha *administration* ya kodi moja na la pili waendelee pia kuboresha *Public Relation* zao, kwa wale wanaowaita walipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mlipa Kodi na *TRA* ni mtu na mteja wake, ni *client.* Kama *client* ni lazima umheshimu pia. Mara nyingi *TRA* wanatumia mabavu kama Bwana Bush, yeye hasikii la mtu na anapiga. Kama ukishindwa kabisa wanafunga *Account* yako kwenye *Bank.* Sasa ukifunga *Account* wewe hukusanyi kodi na yule hazalishi. Sasa nani anayepata hasara, inayopata hasara ni nchi.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo ninayosema kuwa, labda kikubwa zaidi sasa hivi watilie mkazo mambo ya *administration* ya kodi iwe *TRA with a smile.* Hata ukiwa unampelekea *bill* ya *assessment* ya mtu wa kodi hata ikiwa ni mabilioni lakini wewe *smile,* mpe na yeye aone ile *smile* ataisoma baadaye ile *assessment* yako. Lakini atasema loo, siku hizi *TRA,* wanaweza kutoa *smile* wakileta *assessment* yao, watakuwa na *confidence* na wewe. *(Makofi)*

Kitu kingine kikubwa ni hiyo *Public Relations,* hii itabidi waanze toka *scratch* wa-*build up* jina la *TRA* kama kitu ambacho kina sura ya ubinadmu ndani yake ili waweze kuwaambia wateja wao. Wawa-*regard* wale wateja wao, maana sasa hivi unaweza ukafikiria kwamba kila mmoja anayefanya biashara ni *Tax Invader,* anakimbia kodi. Sasa ukiwa na *attitude* hiyo wale wateja wako huwaamini tena na wewe hawatakuamini. Kwa hiyo, mtavutana vibaya sana. Kwa hiyo, *Public Relations* iwe ndiyo kazi kubwa. *(Makofi)*

Suala lingine ilikuwa siyo hiyo Wizara hizo, labda Serikali nzima ni kuwa labda tuanze kufikiria hili suala la ukubwa wa Serikali. Sasa hivi Serikali imekuwa kubwa kulikoni mwaka ule tuliojaribu ku-*decentralize.* Mwaka 1972 tukasema tupeleke Madaraka Mikoani pamoja na Wilayani.

Sasa hali hiyo bado tunayo, barafu na hizo Wizara zimebakia na kurudi tena kuwa kubwa sana. Hata ukiangalia Bajeti pale utaona, ingawa sehemu ya hiyo itakwenda huko Mikoani, lakini bado Wizara ni kubwa na Wizara ni nyingi. Kwa hiyo, tungeweza kuifanya kuwa Serikali iwe ndogo, *effective* na *efficient,* iwe ndogo sana.

Sasa hivi tunajitoa kwenye biashara, tunajitoa kwenye uchumi, lakini bado tuko na Bajeti kubwa sana ziko zina-*hang* kwenye Wizara na yule mtu anayeitwa *DED* kule chini hana kitu, ni mkavu kabisa. Lakini kazi ndiyo tumempelekea yeye. Sehemu kubwa

ya kazi inafanyika kule katika Wilaya na kule *DED* ndiye anayehangaika, hana pesa, hana *resources,* lakini unamwambia achimbe barabara, ajenge madaraja, shule, *dispensaries* na mambo yote hayo bila hata kitu cha kusema kuwa watamsaidia na kama watamsaidia, ni kusaidia kidogo tu, yote afanye yeye mwenyewe.

Kwa hiyo, kama tukiweza kuwa na *structures* hizo za Serikali Kuu, za Mikoa na za *Councils* hizo, tuzi-*rationalize,* ziwe kuwa iliko kazi ndiyo *resources* iwe kule ya watu pamoja na pesa na huko juu tunakofanya *co-ordination* sera, labda tubakie na watu wachache pamoja na kazi chache na tuweze kufanya kwa ufasaha zaidi na kwa *efficient* inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia nadhani kuna haja ya kuandaa mfumo mpya wa Serikali, ambao utazingatia vitu vikubwa viwili. Kwanza Serikali imejitoa katika Biashara, Uchumi, mambo yote hayo, kwa hiyo imejitoa sasa, je, ibakie kuwa kubwa hivyo hivyo au nayo i-*down size* kwa kuweka *efficiency?*

Halafu ya tatu, Serikali ijiandae kuingi katika soko la utandawazi. Soko la utandawazi linahitaji *decision making,* haraka na kwa ufasaha zaidi. La sivyo watakuja wengi, watakuja hapa kwetu tumeanza kupiga kelele, wa Madini tu na Madini wenyewe wako watano, lakini tunaona ni kero kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado watakuja kwenye kilimo, utaona kuwa hata ile unayolima wewe hawawezi kununu ni *too expensive,* wao watalima *cheaper,* tutapiga kelele tena. Kwa hiyo, tujiandae na Serikali yenye *size* ya kuweza kuhimili huo utandawazi na inayoweza kuwa *small, efficient* na *effective.*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani kuwa mchango wangu uwe hivi kwa leo, lakini nitachangia tena, tutakapokuja kwenye *sector* mbali mbali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Muda uliobakia hautoshi kwa mtu kutoa mchango wake. Baada ya kufika hapa tulipofikia, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.37 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 16 Juni, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*